# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 14 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji na Hesabu za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Mwaka 2004/2005 *(The Annual Report on the Activities of the Open University of Tanzania for the year 2004/2005*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 157

**Ujenzi wa Hosteli – Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika bajeti ya mwaka 2006/2007 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli na kwa kuwa Jimbo la Kondoa Kusini, ni moja ya maeneo yaliyo na jamii ya wafugaji na watu wanao hamahama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi wa hosteli katika Jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wanafunzi wachache kati ya wanafunzi waliofaulu kwa alama za juu hupata nafasi katika shule za sekondari za kitaifa ambazo zina mabweni, wanafunzi wengi hupangwa kuendelea na masomo katika shule za sekondari za kata zilizopo kwenye maeneo yao ambayo kimsingi ni za kutwa. Maeneo ambayo makazi ya wananchi yametawanyika kiasi cha wengi kuwa mbali na ilipo shule wanashauriwa kujenga hosteli ili wanafunzi wakae katika mazingira ya shule. Serikali itachangia ujenzi wa hosteli pale uwezo wa fedha utakaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kondoa Kusini lina jamii ya wananchi ambao ni wafugaji na wananchi wanaohamahama kwa ajili ya kutafuta malisho kwa mifugo yao. Jimbo la Kondoa Kusini, lina jumla ya shule za Sekondari kumi na nne zilizojengwa kwa nguvu za wananchi. Kati ya shule hizo ni shule moja tu ya Msakwalo yenye hosteli ya wanafunzi wa kike iliyojengwa na shirika lisilo la Kiserikali la *(World Vision)* kwa kushirikiana na wananchi. Hosteli hiyo, inawahudumia wanafunzi wanaotoka katika Kwamtoro yenye Kata za Kwamtoro, Mpendo, Sanzawa, Ovada na Lalta. Jukumu la kujenga miundombinu katika shule za sekondari ni la wananchi na Serikali hutoa ruzuku kuchangia juhudi za wananchi pale ambapo wameonyesha juhudi hizo.

Kwa mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Kondoa haikupata mgao wa fedha za ujenzi wa hosteli bali ilipata fedha za ujenzi wa nyumba za walimu tatu na kati ya hizo zimejengwa katika shule za sekondari za Farkwa, Jangalo na Msakwalo na vyumba vya madarasa vitano katika shule za Soya, Mondo, Mrijo, Msakwalo na Songolo. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imetoa shilingi 968,000,000/= kwa Mkoa wa Dodoma kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Fedha hizo zilipangiwa kujenga vyumba vya madarasa 37, nyumba za walimu 70, maabara 4, Maktaba 1 na jengo la Utawala 1. Mgawanyo wa rasilimali hii uliwahusisha viongozi mbalimbali katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Kutokana na fedha zilizopatikana Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, imepewa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 13, nyumba za walimu 25 na maktaba moja. Kutokana na uwezo mdogo wa kifedha, namshauri Mheshimiwa Mbunge, kuwashawishi na kuwashirikisha wananchi wa Jimbo lake waweze kuanza ujenzi wa hosteli katika baadhi ya shule ili wanafunzi wengi waweze kupata elimu kikamilifu hasa kipindi ambacho wazazi wao wanahama kufuata malisho kwa mifugo yao.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

(a) Kwa kuwa Wilaya ya Kondoa mpaka sasa haijapata mgao wa kujenga hosteli. Je, Serikali katika Bajeti ijayo itakuwa tayari kutenga fedha ili angalau shule moja iweze kupata hosteli?

(b) Kwa kuwa shule za Sekondari za Msakwalo, Soya na Mondo sasa hivi zimeteuliwa kujengwa kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na kuendelea mpaka kidato cha sita. Je, Serikali itakuwa na mpango gani wa kusaidia hosteli kwa sababu hawa vijana hawatakaa nyumbani na kuja kufuatilia masomo kwa kuwa wanatoka maeneo ya mbali sana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Serikali kwa mwaka huu 2007 kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi imetenga hosteli 12 katika Tanzania nzima. Tunajua kabisa kwamba ni chache lakini ni kufuatana na uwezo wa Serikali. Hosteli hizo zimepelekwa katika Mikoa mbalimbali ambayo hawakupangiwa kupata majengo ya utawala.

Kwa hiyo, siwezi nikaahidi kwamba mwaka ujao tuna mpango gani lakini Serikali ina nia nzuri tu ya kuhakikisha kwamba zile sehemu ambazo ziko mbali na majengo haya ya Sekondari zingekuwa na hosteli lakini kulingana na uwezo mdogo ndiyo maana tunatoa kidogo kidogo kulingana na Bajeti yetu. *(Makofi)*

Kuhusu suala la pili, kuhusu shule za Sekondari za Msakwalo, Soya na Mondo huu ni utaratibu wa kila Wilaya kuangalia kwamba hizi shule za kata baadaye hawa wanafunzi wanakwenda wapi. Ni nia ya Serikali kwamba kila Wilaya iwe na shule za sekondari ambazo zita-*absorb* hawa wanafunzi ambao wameanza katika shule za kata. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Halmashauri kupanga mipango yao vizuri na Serikali pale itakapokuwa na uwezo itasaidia katika kuimarisha shule hizi ili kuwe na kidato cha tano na cha sita.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kama ilivyo Kondoa na Iramba Mashariki kuna wafugaji wanaohamahama hasa Wakhadzabe ambao sasa hivi wana njaa na watoto wao wameamua kusoma. Je, Serikali itasaidia kujenga hosteli ya Wakhadzabe kwenye shule ya sekondari ya Mwangeza ili waweze kupata elimu na waachane na maisha ya kuhamahama? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tatizo hili kama Serikali tunalifahamu kwamba kuna wenzetu ambao wako katika mazingira magumu ikiwa pamoja na wafugaji pamoja na Wakhadzabe, hilo Serikali tunalifahamu. Tunaliwekea mkakati na hapo mambo yatakapokuwa mazuri na kama tutakuwa tumeshatafuta utaratibu tutaangalia sehemu hizo ambazo zina mazingira magumu ili waweze kufikiriwa kiundani zaidi. Ni nzuri ya Serikali kwamba watu ambao wako katika mazingira magumu na kwa muda mrefu walikuwa nyuma kielimu kama vile Wakhadzabe wawe na mazingira mazuri ili waweze kuendana na hali iliyopo sasa hivi.

Na. 158

**Kupeleka Waganga na Wauguzi – Zahanati ya Kata ya Matanga**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Zahanati ya Kata ya Matanga- katika Manispaa ya Sumbawanga imefunguliwa tarehe 28/06/2006 pamoja na nyumba ya Mganga wakati wa mbio za mwenge, lakini hadi sasa haijapata mganga wala muuguzi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupeleka Mganga na Muuguzi ili wananchi wa Kata hiyo waweze kupatiwa matatibu badala ya kwenda sehemu nyingine kutaka huduma ya matibabu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua hali halisi ya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi wa Sumbawanga hususan Kata ya Matanga, kuwa si za kuridhisha. Kwa kuona umuhimu wa kusogeza huduma karibu na wananchi, Serikali ilijenga zahanati ya Matanga ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 28/06/2006. Wakati Zahanati hii inazinduliwa ilikuwa haina nyumba ya mganga wala ya muuguzi, ilikuwa haina vifaa vya kitaalam, samani na pia ilikuwa haijawekwa kwenye mgao wa dawa yaani *(Essential Drugs programmer)* kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa kitaifa na taratibu za hospitali za rufaa kwa ngazi zote uliotolewa na Wizara ya Afya mwezi Juni, 2004 umetamka wazi idadi ya watumishi wanaopaswa kuwepo katika ngazi ya Zahanati kulingana na mwongozo huu zahanati inapaswa kuwa maafisa tabibu 2, wauguzi wawili na mhudumu wa afya mmoja.Tarehe 18/8/2007 Zahanati hii ya Matanga ilianza kupata mgao wa dawa za *(Integrated Logistic System)* na vifaa kazi vya Kitalaam kutoka Serikali Kuu kwa kupitia *MSD Mbeya*, kwa sasa wananchi wa Matanga wanapata huduma katika Zahanati hiyo. Aidha, watumishi waliopo hivi sasa ni wauguzi watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua upungufu wa watumishi uliopo katika Zahanati hii hususan kutokuwepo kwa matabibu wawili, zahanati hii imeingizwa katika orodha ya kupatiwa madawa na watumishi katika Bajeti ya Afya ya mwaka 2007/2008, pindi watalaam hao wakapopatikana zahanati ya Matanga itapewa kipaumbele.

**MHE. ANNA RICHARD LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo ameyajibu.

Kwa kuwa Zahanati ya Matanga mpaka sasa hivi ninavyoongea hakuna muuguzi, wala hakuna mganga ile *dispensary* imefungwa. Je, Serikali ina mikakati gani na wananchi wa Matanga wanavyotangatanga maana yake hawana pa kwenda na ile *dispensary* wamejenga kwa nguvu zao na kwa kuwa Wilaya ya Mpanda ina zahanati kama 12 hazina wauguzi wala hazina waganga zimefungwa na vile vile Mpanda kuna Chuo cha Wauguzi na hivi karibuni nilimsikia Waziri wa Afya, akisema kile chuo kina mipangilio ya kuanza kufanyakazi. Mpaka sasa hivi hakina mpango wowote mpaka mganga wangu wa Wilaya aliniuliza vipi mbona nasikia Waziri anasema eti kuwa Chuo kinafanyakazi. Je, Serikali ina mipango gani na hizi zahanati kwa sababu wananchi wanapata tabu sana? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu maswali ya nyongeza kwa niaba ya Waziri Mkuu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

**NAIBU SPIKA:** Sauti inakuja kwa tabu, labda uongeze *volume* pia.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sauti yangu ni ya upole lakini nitajitahidi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Lupembe kwa niaba ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Tumelieleza Bunge lako mara nyingi kuhusu uhaba mkubwa wa watumishi tulionao katika sekta ya afya. Tumeleeza vile vile mipango ambayo tumeiandaa ili kujaribu kupunguza tatizo linalowapata wananchi hasa katika maeneo ambayo zahanati zimejengwa kwa nguvu za wananchi pamoja na misaada ya *TASAF*. Hivi ninavyoongea kuna zahanati zaidi ya 500 ambazo zimejengwa na zimekuwa hazifanyi kazi. Katika Bajeti ya mwaka huu tuliahidi hapa kwamba tumeweka kipaumbele katika kuajiri wafanyakazi ambao walikuwa hawajaajiriwa. Lakini vile vile kuongeza usaili wa hawa watumishi katika vyuo vyetu. Tumeongeza kwa asilimia 40 kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha. Kuhusu kituo cha Mpanda ripoti ni kwamba tulikuwa na vyuo vya namna hii ambavyo vilikuwa vimefungwa na katika mwaka huu wa fedha tumedhamiria kufungua vituo viwili kikiwemo cha Mpanda na cha Kagera. Naomba Mheshimiwa Lupembe aelewe kwamba hicho kituo kilikuwa hakijafanyi kazi kwa muda mrefu. Kwa hiyo, unahitajika ukarabati ili tujiweke sawa hasa kuhusu wafanyakazi walimu na vitendea kazi. Lakini katika Bajeti hicho chuo kipo na kwamba hakijafunguliwa sasa haina maana kwamba hakitafunguliwa na naahidi kitafunguliwa katika mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu ya upole wa sauti ya Waziri tunaendelea.

Na. 159

### Kuingia kwa Wafugaji – Kilwa

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO (K.n.y. MHE. HASNAIN G. DEWJI**) aliuliza:-

Kwa kuwa, wafugaji mbalimbali wameingia Wilayani Kilwa kwa ajili ya malisho ya wanyama wao hali iliyosababisha matatizo kati yao na wakulima:-

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa wafugaji hao wasiongezwe katika Wilaya ya Kilwa, ili kuzuia tatizo la migogoro ya wafugaji na wakulima litakalozuka hapo baadaye hadi miundombinu iboreshwe na kuongeza majosho na malambo ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua adha na matatizo yanayoweza kutokea iwapo uingizaji wa mifugo katika maeneo yoyote mapya hautazingatia uwezo wa ardhi na upatikanaji wa huduma muhimu kama vile maji, majosho na minada. Kutokana na ukweli huu, Serikali katika mkutano wake na wakuu wa Mikoa minane (8) ukiwemo Mkoa wa Lindi, uliofanyika Mjini Dodoma tarehe 8/9/2006, iliainisha Wilaya zenye maeneo yanayofaa na yenye uwezo wa ardhi kupokea mifugo hususan ile ili yotokea Ihefu. Katika mkutano huo, ilibainishwa kuwa Mkoa wa Lindi ulikuwa na uwezo wa kuchukua mifugo hadi ng’ombe 163,000 kwa mchanganuo ufuatao: Lindi vijijini 38,500, Nachingwe 50,000 na Kilwa 74,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu tulizonazo Wilaya ya Kilwa kwa sasa ina ng’ombe wapatao 5,849, mbuzi 1,027, Kondoo 144 na punda 19. Idadi hii ni ndogo mno ukilinganisha na uwezo wa ardhi yake ambao umekadiriwa kuwa mifugo 74,500. Kwa hali hii Wilaya bado ina uwezo wa kupokea mifugo ya ziada takribani 67,441. Hata hivyo ili kuepukana na migogoro inayoweza kutokea kati ya watumiaji ardhi, uongozi wa Wilaya ya Kilwa, umetenga maeneo ya wafugaji katika vijiji vya Kisangi A, Kimbarambara, Matandu, Mauji, Liwiti, Nainopwe, Kiranjeranje, Mbwemkuru, Marendego na Somanga. Maeneo hayo yanakadiriwa kuwa na jumla ya hekta 150,000 na upimaji wa kuhakiki umeanza na unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wilaya imeanza kuweka miundombinu muhimu katika maeneo haya. Kwa mfano mwezi Oktoba, 2006 Wizara ilituma jumla ya shilingi milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa malambo katika vijiji vya Marendego na Matandu na kazi imekamilika. Aidha, mwezi Mei, 2007 Wizara ilituma jumla ya shilingi milioni 60 milioni 30 zikiwa ni za ujenzi wa lambo moja la

Miteja na milioni 30 zingine kwa ajili ya ukarabati wa josho la Marendego na ujenzi wa josho jipya la Matandu. Lengo ni kuweka miundombinu muhimu ya mifugo kwa kila kijiji kilichoainisha maeneo ya ufugaji.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa ufafanuzi wa kiasi. Lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa swali la msingi linaelezea kuwepo kwa migogoro inayoashiria uvunjaji wa amani kati ya wakulima na wafugaji. Serikali imechukua hatua gani za dharura za kurekebisha hali hiyo?

(b) Kwa kuwa wafugaji bora ni pamoja na kuwa na malambo ya maji ya kutosha pamoja na matumizi ya dawa za kuzuia magonjwa kama vile Ndiganakali na kwa kuwa Wilaya ya Kilwa ina majosho machache likiwepo lile linalofahamika kwa sasa kwamba linatumika la Malandegu. Ni hatua gani za Serikali za dharura za kurekebisha hali hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Njwayo kama ifuatavyo:-

Wakati mwingine tunakuwa na hisia tu kwamba kutatokea migogoro ya kijamii hususan wakulima na wafugaji pale ambapo wafugaji wanaingia au wanatarajia kuingia. Kwa kawaida wafugaji walio wengi ni wakulima pia. Kwa hiyo, wanaheshimu sana mazao na mara nyingi wanakuwa siyo chanzo cha migogoro. Lakini kama ambavyo watumiaji wengine wa ardhi wanavyoweza wakaenda kinyume cha sheria na kanuni mbalimbali zinazoongoza basi sheria huwa zinachukuliwa za kuhakikisha kuwa migogoro hiyo inatatuliwa ili kusudi wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi wakae kwa amani na usalama. Suala la pili, hatua za dharura za kuhakikisha kuwa majosho na Malambo nimezieleza kwenye jibu langu la msingi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Wilaya ya Kilwa kama ilivyo kwenye Wilaya zingine inakuwa na majosho pamoja na huduma zingine ili kuhakikisha kuwa mifugo inaogeshwa. Nimesema kwa sasa kuna mifugo iliyokwishaingia takribani 5,000 katika Wilaya ya Kilwa kutoka Ihefu. Katika hali ya kawaida josho moja linahudumia mifugo 5,000. Lakini kuna majosho zaidi ya mawili katika Wilaya ya Kilwa na kwa hiyo, kwa kuwa tunatarajia wafugaji wengi wanaweza wakaingia Serikali itaendelea kujenga majosho ili kuhakikisha kuwa Wilaya ya Kilwa inajitosheleza kwa majosho. (*Makofi*)

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la majosho katika Wilaya ya Kilwa yanafanana kabisa na matatizo ya majosho katika Jimbo la Solwa. Kwa kuwa Jimbo la Solwa lina ng’ombe zaidi ya 300,000 na kutokana na majibu ya Naibu Waziri sasa hivi anasema kwamba josho moja linatakiwa kuhudumia ng’ombe 5,000 ina maana tunahitaji majosho 60 na sasa hivi katika jimbo la Solwa tuna majosho labda manane (8) tu. Ningependa kumwomba Naibu Waziri atueleze ni kwa sababu gani ama mpango wa *DASP* au wananchi hawaelewi utekelezaji wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ningemwomba atujibu na atueleze ni kwa nini na atatusaidia nini ili jimbo la Solwa lipate majosho ya kutosha?

**NAIBU SPIKA:** Ingawa hapafanani, kule Kilwa ng'ombe wachache kwenu ng'ombe wengi, lakini Waziri wa Mifugo jibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Salum, pamoja na majibu ya msingi yaliyotolewa na Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Suala la majosho kwenye Wilaya linaonekana kuwa ni tatizo kwa sababu Wilaya karibu nyingi nchi hii, nikitoa mfano Mkoa wa Dodoma wameshindwa kuibua miradi chini ya mpango wa *ASDP*. Kwa hiyo, wanachokikumbukwa ni kilimo, lakini upande wa mifugo, Wilaya nyingi sana hawakumbuki kwa sababu hii miradi inatakiwa itokane na mipango ya Wilaya. Wanaibua miradi wanataka majosho mangapi, sehemu gani, fedha ziko pale lakini hawaleti hiyo miradi ili iweze kuwekwa kwenye mipango.

Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kuwaomba hasa Waheshimiwa Wabunge ambao pia wanahusika kwenye vikao vya Halmashauri za Wilaya, waweke msisitizo zaidi ili tatizo hili la majosho na malambo liweze kutatuliwa kupitia mipango ya Wilaya chini ya program ya kilimo *ASDP*. (*Makofi*)

Na. 160

**Uhaba wa Maji na Mnada kwa Wafugaji**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y.MHE. RICHARD S. NYAULAWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna wafugaji wengi katika Kata ya Mshewe- Wilaya ya Mbeya Vijijini, ambao ndio chanzo cha nyama Wilayani humo na kwa kuwa, wafugaji hao wana matatizo ya uhaba wa maji na kutokuwepo na mnada.

(a) Je, Serikali inaweza kuwasaidia wafugaji hao kwa kujenga bwawa la maji kwa ajili ya mifugo yao?

(b) Je, kama mpango huo upo utatekelezwa lini?

(c) Je, Serikali inaweza kujenga mnada wa kisasa ili kufanya kazi ya uuzaji wa ng'ombe uwe rahisi na kurahisisha ukusanyaji wa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitoe maelezo yafuatayo ya utangulizi kabla ya kujibu swali la

Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Kata ya Mshewe katika Wilaya ya Mbeya Vijijini ina vijiji vinane na inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo na ndicho chanzo kikubwa cha nyama Wilayani humo. Kata hii ina mifugo ipatayo 14,013 ikijumlisha ng'ombe 9,218, mbuzi 2,249. Kondoo 766, punda 79 na nguruwe 1,318. Aidha Kijiji cha Mshewe kinaongoza kwa kuwa na mifugo mingi kuliko vijiji vingine na pia kuna kituo cha kupokea mifugo inayosafirishwa. Upo pia mnada katika Kata hii wa muda mrefu wa ng'ombe unaotumiwa na wafugaji kuuzia mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Richard Saidi Nyaulawa Mbunge wa Mbeya Vijijini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mipango ya Maendeleo ya kilimo Wilayani kwa kifupi kwa Kiingereza *(DADPs)* ilianza mchakato wa ujenzi wa lambo la maji kijijini Mshewe mwaka 2006/2007 na utakamilika mwaka huu wa fedha 2007/2008 kwa gharama ya shilingi 57,740,000/= Serikali inachangia asilimia 80 ya gharama yote na wananchi wakiwemo wafugaji wanachangia asilimia 20, hii ni sawa na shilingi milioni 11,540/= (milioni 11 laki tano na arobaini elfu). Halmashauri ya Wilaya kwa upande wake itaendesha mafunzo kuhusu hifadhi ya ardhi kuzunguka maeneo ya lambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa 2007/2008 Serikali kuptia *DADPs* itatoa shilingi milioni 11,500,000/= kwa ajili ya kuboresha mnada wa mifugo uliopo katika kijiji cha Chang'ombe, Kata ya Mshewe, kwa kuujengea uzio. Kazi hii ikikamilika itarahisisha pia ukusanyaji wa kodi itokanayo na mauzo ya mifugo kwa Halmashauri ya Wilaya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika sehemu (a) mipango yote miwili ya mnada na lambo itakamilika katika mwaka huu wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali katika kuendeleza masoko na biashara ya mifugo nchini ni kupanua na kujenga minada kulingana na mahitaji ya maeneo yenye mifugo ili kuwawezesha wafugaji kuvuna kwa kuuza mifugo yao na wafanyabiashara nao kununua mifugo katika mazingira ya uwazi na ushindani unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa azma hii unafanywa ama na Wizara yangu au Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kupitia Halmashauri za Wilaya. Napenda kuupongeza uongozi wa Wilaya ya Mbeya Vijijini kwa kuchukua hatua za kukarabati mnada uliopo kijiji cha Chang'ombe kwa kuujengea uzio kama nilivyokwishasema ili

kuboresha uuzaji wa mifugo na kurahisisha ukusanyaji wa kodi itokanavyo na biashara hiyo. Napenda kumhakikishia tena Mheshimiwa Mbunge kwamba mnada utakapokamilika utatoa huduma inayohitajika kwa Kata ya Mshewe na maeneo ya jirani.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na bila wananchi hawa wa Mshewe watakuwa wamefarijika na majibu hayo. Lakini nina swali moja tu la nyongeza. Kwa sababu Wilaya ya Mbeya Vijijini inapakana na Wilaya ya Mbozi ambayo na jimbo langu lipo huko na kwa sababu pia Wilaya ya Mbozi tunafuga sana lakini tatizo lililopo ambalo Mheshimiwa alitaja katika majibu yake ya msingi linafanana sana na matatizo yaliyopo Wilaya ya Mbozi kwa maana ya kwamba mabwawa ya maji kwa maana ya malambo hususan jimbo la Mbozi Magharibi inakabiliwa na tatizo hilo kubwa sana hasa Tarafa ya Kamsamba na Msangano. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anatuahidi nini na hususan wafugaji wale wa maeneo niliyoyataja kuwasaidia ili waweze kupata malambo ya kisasa ili mifugo yao isiweze kupata shida na kwa maana hiyo kupunguza uhamaji wa wafugaji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyokwishasema Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwenye swali la kwanza, suala hili la ujenzi wa malambo, majosho linategemea wananchi wenyewe kuibua miradi itakayoweza kufadhiliwa na Serikali kupitia mpango wa maendeleo ya Kilimo Wilayani *DADPs* na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo ametoa wito kwetu sisi Wabunge kuwasaidia wananchi ili kuibua miradi hiyo na kuibua kwa lugha rahisi ni wananchi pale kuelewa kuwa hili ndiyo tatizo walilonalo na wanalipa kipaumbele.

Kwa hiyo, wanasema basi kama kuna fedha sisi tunahitaji kujengewa lambo. Kwa hiyo, nitoe wito tena kwamba wananchi wa Mbozi Mashariki kwa kushirikiana na wewe Mheshimiwa Mbunge muone haja ya kuibua mradi huu kuona kwamba ndiyo kipaumbele ili kusudi hatimaye muweze kujengewa lambo au malambo kadri ya mahitaji ya Wilaya. Ni azma ya Serikali kupitia Wizara yetu kuona kuwa wafugaji wanajitosheleza kwa majosho, malambo na huduma zingine ili kuboresha Sekta ya Mifugo nchini.

Na. 161

**Uhaba wa Nyumba za Majaji/Mahakimu**

**MHE. MARGRETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa nyumba za kuishi Majaji na Mahakimu nchini kiasi kwamba wengine wanalazimika kupanga nyumba uraiani:-

Je, Serikali ina mikakati gani endelevu katika kukabiliana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa kuna uhaba mkubwa wa nyumba za kuishi Majaji na Mahakimu nchini kiasi kwamba wengine wanalazimika kupanga nyumba uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu, ambayo ndio yenye jukumu la kujenga nyumba za watumishi wa Serikali wakiwemo Majaji na Mahakimu, inayo mikakati endelevu ya kuangalia uwezekano wa kutenga fedha za kutosha ili nyumba hizo zijengwe mapema na kuliondoa tatizo hili sugu. Katika kutekeleza mkakati huo baadhi ya Kanda za Mahakama Kuu tayari zina viwanja vya ujenzi wa nyumba hizo ili kushirikiana na Wizara ya Miundombinu.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza nina swali moja tu. Pamoja na majibu ya kutia moyo nilikuwa tu napenda kuuliza sasa hivyo viwanja ambavyo vimeshakuwa *identified* kwenye hayo maeneo ya Kanda ya mambo ya Sheria vitajengwa lini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ni mategemeo yangu kwamba kama Mheshimiwa Mbunge alivyopata matumaini Majaji na Mahakimu nao watakuwa nao wamepata matumaini na wananchi kutegemea huduma mzuri kutoka kwa Majaji na Mahakimu wetu. Viwanja hivyo vimeainishwa kwa niaba ya kujenga kwa ushirikiano na Wizara ya Miundombinu pamoja na mradi wetu wa maboresho. Tutajitahidi sana kwa kadri ya uwezo wa rasilimali za Serikali kujenga hizo nyumba ili kutokuwa na nyumba za Mahakimu na Majaji iwe historia nchini mwetu.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Ahsantesana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:- Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yenye kuwa na matumaini, naomba niulize swali moja dogo kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hivi sasa Majaji wengi wanakaa mahotelini na hutumia gharama kubwa sana. Kwa mfano sasa hivi Mkoa wa Tabora ambao kuna Mahakama Kuu ya Kanda, Majaji asilimia kubwa hukaa hotelini. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha angalau hawa Majaji wanajengewa nyumba za dharura ili kuondokana na adha waliokuwa nayo na usalama wao kwa sababu wao sasa hivi wanashughulikia kesi nzito sana? Je, Serikali inaniambia nini kwenye Bajeti hii ili tuone ni jinsi gani wanaweza kufanya hiyo kazi? Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna Majaji na Mahakimu ambao wanakaa mahotelini na kwamba ni gharama kwa wao kukaa hotelini. Lakini pengine niseme kwamba si wengi sana ingawa hata kama ni mmoja ni gharama na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba usalama wao

utakuwa hatarini. Mimi naliahidi Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inalijua tatizo hili na ndiyo maana nimesema kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu pamoja na kupitia mradi wetu wa maboresho ambapo kuna hela kidogo ya kujenga nyumba za Majaji na nyumba za Mahakimu basi tutafanya hivyo kwa kutambua tatizo hili na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kuona kwamba hili ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Na. 162

***Extended Acts Application to Tanzania Zanzibar***

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo sheria nyingine zinazotungwa na Bunge ambazo hutumika pia kwa Tanzania Zanzibar *Extended Acts Application to Tanzania Zanzibar* lakini ndani ya sheria hiyo kukawa na *cross references* kwa sheria nyingine isiyo ya Muungano:-

(a) Je, hiyo sheria Nyingine inayofanyiwa *cross references* nayo pia itatumika Tanzania Zanzibar hata kama jambo si la Muungano?

(b) Ikiwa sheria hiyo itatumika huko Zanzibar. Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo itakuwa inazifuta sheria zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi juu ya jambo hilo ambalo si la Muungano?

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka wa kuacha kutumia *cross reference* katika sheria za Muungano kwa mambo yasiyo ya Muungano, au kama *cross reference* ikilazimika kufanyika basi itambue pia sheria za Baraza la Wawakilishi juu ya jambo hilo lisilo la Muungano?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, naomba nitoe maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi hapa Tanzania kumekuwa na Sheria kadhaa zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na zikatumika hadi Tanzania Zanzibar. Sheria hizo zinatumika Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa katika Katiba. Sheria hizo huweka fungu ambalo huitwa *Application Clause* ambayo huainisha eneo ambamo sheria itafanya kazi. Kwa mujibu wa Katiba sheria zinazotumika pande mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni lazima ziwe zimetamka bayana chini ya kifungu cha matumizi ya sheria hizo au kwa lugha ya Kiingereza *(Application Clause)* kuwa zitatumika Tanzania Bara na vile vile Tanzania Zanzibar. Utaratibu huu unaoweka masharti ya matumizi ya sheria hizi umefafanuliwa chini ya Ibara ya Katiba ya 64(4)(a) na (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kitaaluma *cross reference* haina maana ya kutunga sheria, isipokuwa inafanya tu

marejeo ya sheria zinazofanana na sheria husika. Kwa kufanya hivyo, mwandishi wa sheria analinganisha misingi, dhana, hoja na maudhui ya kanuni inayodhamiriwa. Matumizi haya rejea kama ilivyo katika maandishi ya kiutafiti wa mada za kitaaluma, yanarahisisha uelewa kwa msomaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayofanyiwa *cross reference* haiwezi kutumika Tanzania Zanzibar kama sheria hiyo sio ya Muungano kwa sababu tu kwamba imefanyiwa *cross reference.* Ili sheria ya aina hiyo iweze kutumika sharti utungaji wake ufuate utaratibu wa kikatiba ambao umeainishwa katika Ibara ya 64(4)(a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Ibara ya 132 ya Katiba ya Zanzibar; 1984. Ibara ndogo (1) ya Ibara ya 132 ya Katiba ya Zanzibar inaelekeza kama ifuatavyo:-

Hakuna sheria yeyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza katika jibu langu la sehemu (a) la swali hili Sheria hiyo haiwezi kutumika huko Zanzibar mpaka ikidhi masharti ya Katiba zote mbili kama nilivyoeleza. Hivyo hakuna sheria itakayofutwa kwa kufanyiwa *cross reference* Sheria nyingine.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya rejea katika sheria yoyote iwe ya Muungano au kwa mambo yasiyo ya Muungano ni muhimu kwa ajili ya kurahisisha marejeo na uelewa. Kufanya hivyo, ni kwa manufaa ya Serikali zote mbili na kwa kuzingatia maelezo niliyotoa hapo mwanzoni. Sheria hiyo itatumika Zanzibar pale tu utaratibu uliouelezwa na Katiba zote mbili ambao nikwishaueleza awali, yaani Ibara za 64(4)(a) na (b) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 na Ibara 132 ya Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba kwa kutumia utaratibu huo wa kitaaluma hakuna wakati wowote ambapo Serikali imekiuka masharti ya Katiba zote kwa kutunga sheria ambazo zinavunja sheria za Zanzibar au Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kama ingetumika sheria hiyo Zanzibar faida yake ingekuwa nini Mheshimiwa Waziri na kama ingetumika faida yake ingelikuwa nini na kama kutokutumika hasara yake nini Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vuai ameuliza kama ingetumika sheria hiyo Zanzibar faida yake ingekuwa

ni nini na kama haitatumika hasara yake itakuwa nini? Sasa hakufafanua ni sheria gani. Lakini kwa ujumla *cross reference* ni kuongeza uelewa wa shauri lenyewe au la sheria yenyewe kwa kulinganisha na sheria ama Tanzania Zanzibar au Tanzania Bara.

Faida yake ni kwamba shauri hilo sasa litaeleweka zaidi kuliko kama *cross reference* isingetumika. Lakini kutokutumia maana yake ni kwamba utakuwa na mtazamo mfinyu kwa maoni yangu ninavyoona lakini sidhani kama *cross reference* siyo mbadala ya sheria ya Zanzibar wala sheria ya Muungano. Kwa hivyo *cross reference* haina madhara yoyote wakati wowote itakapotumika na wale wanaohusika.

Na. 163

**Fidia ya Maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa mji wa Ushirombo ni moja kati ya miji inayopanuka kwa kasi kubwa pamoja na maeneo ya Uyovu na Masumbwe Wilayani Bukombe, na kwa kuwa Sheria ya Ardhi Na. 4 na 5 ya mwaka 1999 inawataka wananchi wanaoondolewa kwenye maeneo yao lazima walipwe fidia; na kwa kuwa wapo wananchi wanahangaika na tatizo la kuchukuliwa kwa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za maendeleo kama vile Butambala, Maganzo na sehemu nyingine za Bukombe:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje wananchi hao hasa ikitiliwa maanani kuwa Halmashauri haina uwezo wa kulipa fidia zao?

(b) Kwa kuwa mpango wa Serikali ni kuboresha maisha ya Mtanzania. Je, kwa mwananchi wa kawaida anayetegemea kilimo, halafu shamba lake likikumbwa na upanuzi wa mji ataborekaje kimaisha, je huko si kumdidimiza kimaendeleo na Serikali inasemaje juu ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi Na. 4 na sheria ya Ardhi ya Vijiji No. 5 ya mwaka 1999 katika vifungu vya 3 vinaelekeza bayana ulipaji wa fidia kwa kufuata utaratibu. Sheria inatamka wazi kuwa fidia italipwa kwa yule atayechukuliwa ardhi yake. Kwa misingi hiyo Halmashauri husika inatakiwa kutenga fedha kupitia Bajeti yao kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yanachukuliwa kwa ajili ya upanuzi wa mji.

Serikali Kuu inaweza kusaidia Halmashauri pale ambapo Halmashauri husika itaomba mkopo wa fedha za kupima viwanja kwa kupitia Mfuko wa *Plot Development Revolving Fund (PDRF)* au Mfuko wa Upimaji Viwanja ulioanzishwa na Wizara ya Ardhi kupitia Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kupanua mji ni uamuzi wa wananchi, kupitia Halmashauri zao. Hakuna sababu ya kupanua miji kama upanuzi huo hauna manufaa kwa wakazi wa Halmshauri hiyo. Manufaa ya kawaida kwa wannchi yanayopatikana kutokana na upanuzi wa miji ni pamoja na huduma za kijamii zinazotolewa baada ya upanuzi wa mji huo kama vile, barabara, shule, hospitali, maeneo ya soko na kadhalika. Huduma kama kilimo kilichokuwa kikifanywa na watu hao hukoma baada ya miji kutangazwa na endapo wananchi hao watataka kuendelea na kilimo basi wanaweza kwenda katika maeneo mengine yasiyofikiwa na Maendeleo ya kimji.

Maeneo ya Butambala (Ushirombo) Wilaya ya Bukombe yaliandaliwa mchoro wa mipangomiji na kupitishwa na Halmashauri ya Wilaya tarehe 15/10/2001 na mchoro huo uliidhinishwa na Wizara ya Ardhi tarehe 9/11/2002. Kama Sheria za Ardhi zitazingatiwa na Halmashauri husika maisha ya Watanzania watakaoguswa na zoezi hilo yatakuwa yameboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu tulizo nazo zinaonyesha kuwa Mkuu wa Wilaya wakati huo aliagiza wananchi waliokumbwa na zoezi hilo wapewe viwanja na waligawiwa viwanja katika maeneo jirani. Uthamini pia wa mali zao ulifanyika mwaka 2005 na fidia ikalipwa kwa awamu kuanzia mwezi Desemba mwaka 2006.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali. Lakini nataka kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mfuko wa upimaji viwanja wamesema ulioko Serikali Kuu unaweza ukasaidia katika Wilaya husika endapo itaomba. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anakubali kupokea ombi la Wilaya ya Bukombe kwamba tupatiwe pesa hiyo tutakapowasilisha rasmi ili tuweze kulipa fidia kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iko tayari kupokea maombi kutoka Halmashauri yoyote kwa ajili ya kupima viwanja kupitia mifuko miwili ambayo nimeitaja katika jibu langu la msingi. Ila kinachotakiwa muandike mchanganuo unaokubalika na mlete katika Wizara yetu mapema iwezekanavyo tutakagua kupitia na ukikubalika tutawapatia mkopo wa kupima viwanja. *(Makofi)*

Na. 164

**Miradi ya Visima Virefu**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika kuendeleza mpango wake wa miradi ya maji ambayo fedha yake inatoka *World Bank* ina malengo ya kuchimba Visima Virefu katika Wilaya, na kwa kuwa kutokana na mradi huo Serikali ina mpango wa kuchimba visima kumi katika Wilaya ya Pangani kwa masharti kuwa wananchi wachangie asilimia tano (5%) ya gharama za mradi, na kwa kuwa Kata za Kinanga, Pangani Mjini, Madanga na Mwera zimeshatimiza masharti ya mradi:-

(a) Je, ni lini miradi hiyo itaanza kutekelezwa?

(b) Je, ni sababu zipi zinazofanya miradi hiyo kuchelewa kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya Maendeleo ya sekta ya maji chini ya programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira vijijini imeanza kutekelezwa katika Wilaya zote nchini kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2007/2008. Fedha kwa ajili ya kutekeleza Programu zinatokana na Bajeti ya Serikali na misaada ya Wahisani ambapo Benki ya Dunia ni mojawapo.

Miradi iliyotekelezwa ni ile iliyopewa kupaumbele katika mipango ya Halmashauri ya Wilaya kulingana na mahitaji ya vijiji husika. Kila Wilaya imechagua vijiji 10 ambavyo miradi yake ya maji itatekelezwa baada ya kufanyiwa usanifu na wahandisi washauri. Aidha, kila Wilaya imechagua miradi midogo midogo ya kuondoa kero za wananchi *(quickwins)* ambayo inatekelezwa hivi sasa kabla ya wahandisi washauri kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Pangani miradi midogo midogo ya kuondoa kero kwa wananchi iliyopendekezwa na Halmashauri ya Wilaya ni Kipumbwi, Kibinda, Mwera, Mikinguni, Kimanga na Langoni. Kazi zilizopangwa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu, ununuzi wa pampu na kukarabati miundombinu.

Pia utekelezaji wa miradi hiyo unaendelea vizuri. Miradi ya miji ya Pangani na Madanga itaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa 2007/2008 baada ya kupatikana wahandisi washauri wa kuifanyia usanifu.

(c) Mheshimiwa Spika, miradi yote iliyopangwa kutekelezwa chini ya programu Maendeleo ya Sekta ya Maji ilitarajiwa kuanza mwaka 2006/2007. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi umechelewa kutokana na muda mrefu uliotumika katika mchakato mzima wa kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali.

Wakati huo, Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Wizara na Sekretarieti za Mikoa ziliendelea na taratibu za maandalizi ya miradi ikiwa ni pamoja na kutayarisha na kuainisha maeneo ya uchimbaji wa visima virefu au vifupi, kuandaa mahitaji na aina ya vifaa na mitambo mbalimbali *(specifications)* pamoja na makabrasha ya zabuni. Matangazo ya kuwapata Wahandisi Washauri wa kusanifu miradi yametolewa kwenye magazeti ya mwezi Oktoba, 2007. Kazi ya kuwapata washauri itakamilika mwanzoni mwa mwaka 2008.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Pamoja na kwamba miradi hiyo imechelewa na wananchi wamekwishachangia asilimia 5 ya miradi hiyo, baadhi ya miradi hiyo sasa hivi imeingia kwenye *quickwins* nini hatima ya miradi hiyo pindi zile pesa ambazo zilikuwa zinatarajiwa kutoka *World Bank* zianze kutumika? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa kuna maeneo mengi ambayo miradi hiyo itatekelezwa kuna tatizo la kuweka *transforma* za umeme katika maeneo hayo, je, Serikali kwa maana ya Wizara ya Maji iko tayari kushirikiana na Halmashauri zetu kuwaandikia Wizara ya Nishati na Madini kutoa kipaumbele katika miradi hiyo ili *transforma* zifungwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba siyo Halmashauri ya Pangani peke yake hata zingine pia kuna baadhi ya miradi ambayo ilikuwa kwenye *quickwins* lakini pia wakati huo huo ipo katika miradi 10 ya vijiji vya maji. Hatua ya kufanya ni:-

Miradi ya *quickwins* ni miradi ya kuondoa kero, ni miradi ambayo ya kufufua miradi ya zamani ambayo angalau wananchi wanaweza wakatumia hadi watakapopata mradi mkubwa wa uhakika na pale ambapo mradi wa *quickwins* ni mradi ambao baada ya kufufuliwa umeonekana ni wa kudumu na ni mzuri basi tunawashauri Halmashauri husika kwamba watuletee marekebisho ya vijiji vyao 10 kabla ya Mshauri Mkuu hajaenda kukagua ni miradi gani ambayo ataifanyia usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la kuhusu mambo ya *transforma* kama jinsi ambavyo inaonekana kwamba baadhi ya miradi mingi itatumia umeme na ameomba kwamba tuweze kushirikiana na Wizara husika na *TANESCO* kutoa kipaumbele.

Hilo nimepokea ushauri lakini na pia hata hivyo kwa sasa hivi *TANESCO* wanatupa ushirikiano mzuri sana katika kutekeleza kazi hiyo na baadhi ambao tayari miradi yao ya *quickwins* inahitaji umeme *TANESCO* wanatoa ushirikiano na yote inatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwamba kwa miradi yote ambayo itahitaji umeme Halmashauri iweke kipaumbele cha kupangia Bajeti ya shughuli, kwa ajili ya kuvuta umeme.

Na. 165

**Shirika la National Milling**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ndio msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika mapinduzi *(reform)* ya uchumi wa Tanzania, na kwa kuwa miaka ya nyuma kulikuwa na Shirika la *National Milling Corporation* ambalo lilisaidia sana wananchi na hasa wafanyakazi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na chombo kama hicho au kinachofanana na hicho kipo nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza Shirika la *National Milling Corporation* lililopo Iringa Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Shirika la Usagishaji la Taifa yaani *NMC* lilianzishwa kwa Sheria Na. 19 ya mwaka 1968 na lilikuwa na majukumu yafuatayo:-

Kufanya makadirio ya ununuzi wa mazao ya chakula kwa kushirikiana na vyama vya ushirika na Wizara ya Kilimo au taasisi na kadhalika;

Kununua mazao kutoka kwenye vyama vya ushirika

Kusaga nafaka;

Kufuatilia hali ya chakula nchini na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu hatua za kuchukukuliwa; na

Aidha *NMC* ilikuwa inajishughulisha na kusimamia hifadhi ya chakula cha Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mali za *NMC* zilizokuwepo katika kila Mkoa zilijumuisha vinu vya kukobolea, kusagisha nafaka, maghala, vihenge vya kuhifadhia nafaka, nyumba za kuishi pamoja na Ofisi.

Kufuatia Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Shirika la Usagaji la Taifa liliwekwa chini ya *PSRC* kwa ajili ya kubinafsishwa mwaka 1996. Ubinafsishaji wa mali za Shirika ulianza mwaka wa 1997 na bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatia kuvunjwa kwa Shirika la Usagishaji la Taifa ambalo lilisaidia sana wananchi, Serikali imeona umuhimu wa kuwa na Bodi ambayo itasimamia masoko ya mazao mchanganyiko yakiwemo yale yaliyokuwa yakishughulikiwa na *National Milling Corporation*. Bodi itakuwa na jukumu la kusimamia taratibu za kuhudumia mazao hayo. Mchakato wa kuunda Bodi hiyo ambayo itakuwa inajulikana kama Bodi ya Mazao Mchanganyiko bado unaendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kinu cha mahindi kilichoko Iringa, kilikuwa ni sehemu tu ya mali zilizokuwa zinamilikiwa na *National Milling Corporation* na kina uwezo wa kusagisha tani 60 za mahindi kwa saa 24. Mali nyingine zilizoko Iringa ni pamoja na maghala na vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 18,000 za nafaka.

Mpango wa Serikali wa kuziendeleza mali hizo ni pamoja na kuzikabidhi kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko itakapoundwa kama sehemu ya mtaji wake.

**MHE. PINDI H. CHANA:** hsante Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali na Waziri na kwa kuwa, amesema katika jibu lake la msingi kwamba kutaundwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, na kwa kuwa, hatufahamu lini Bodi hiyo itaanza kufanya kazi. Na hivi sasa katika Mkoa wa Iringa wapo wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza katika sekta ya kilimo wakiwa ni pamoja na Wakulima, Vyama vya Ushirika na Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa wako tayari kuwekeza.

Waziri atakubali kufanya mazungumzo na wawekezaji hawa ili kuangalia jinsi ya kuendeleza sekta hii ya kilimo na hususan *National Milling Corporation (NMC)?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pindi Chana, kama ifuatavyo:-

Vihenge na maghala ya *National Milling Corporation* yale ya Iringa, yaliacha kutumika mwaka 2000. Maghala yana marekebisho madogo pamoja na deni la *TANESCO.*

Kwa hiyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari kuruhusu mtu yeyote, mwekezaji yeyote anayetaka kuwekeza katika vihenge hivyo na maghala hayo kusudi waweze kuyaendeleza lakini waendeleze wananchi katika kilimo na kuhifadhi mazao yao au kusagisha mazao yao hadi hapo ambapo Bodi ya Mazao Mchangayiko itakapoanzishwa basi tutarudisha.

Kwa hiyo kama ni mikataba itakuwa ni mifupimifupi mpaka hapo tutakapokuwa na Bodi ya mazao mchanganyiko. Kwa hiyo, ruhusa hiyo ipo, Mheshimiwa Mbunge na wenzako mnaweza mkawasiliana na Serikali, tunaweza tukalimalizia hilo suala.

Lakini kwa sasa hivi kuna mwekezaji mmoja ambaye ameshajitokeza ambaye anataka kusagisha tani 57,000 kwa mwaka pale Iringa, lakini mchakato bado unaendelea, kama atashindwa basi kama wapo wengine basi tunawakaribisha.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kama nakumbuka vizuri ni kwamba mimi ndio nilikuwa mtu wa kwanza kuuliza Serikali juu ya kuunda kwa Bodi hii miaka 4 iliyopita. Sasa nataka leo Serikali iniambie ni lini itaunda Bodi hii?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malangalila kama ifuatavyo :-

Bodi ya Mazao Mchanganyiko ina mahusiano na sera ya masoko, kwa hiyo tunasubiri kwanza wizara ya Viwanda na Biashara imalize mchakato wa kuandaa sera ya masoko ndipo ambapo tutaandaa na sisi hiyo Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

Na. 166

**Mikakati ya Kuinua Kilimo Nchini**

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, na kwa kuwa wananchi wengi bado wanatumia mbinu za zamani za kilimo, hali inayosababisha wakulima kubaki katika dimbwi la umasikini :-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuanzisha Benki ya Wakulima ambayo itatoa mikopo kwa wakulima hasa wakulima wadogo ?

(b) Je, serikali haioni kuwa kuna haja ya kujenga Kiwanda cha Matrekta na zana zingine za kilimo ili wakulima wabadilishe kilimo chao ?

(c) Kama Serikali haina uwezo wa kuanzisha kiwanda hicho. Je, iko tayari kutafuta mwekezaji kutoka nchi rafiki ili aweze kujenga kiwanda hicho ?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo taasisi za fedha ambazo zitatoa mikopo kwa wakulima wakiwemo pia wakulima wadogo wadogo. Kwa kutambua hilo, kuanzia mwaka 2006/2007, Serikali iliamua kuibadili Benki ya Rasilimali yaani *Tanzania Investiment Bank (TIB),* kuwa benki ya Maendeleo. Benki hii ndiyo inayojishughulisha na maendeleo ya sekta zote za uzalishaji zikiwemo za kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuanzia mwaka 2007/2008 jukumu kubwa la serikali ni kuendelea kuimarisha Benki hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha inapata mtaji wa kutosha ili kuiwezesha kutoa mikopo kwa ufanisi zaidi. Wadau mbalimbali wataendelea kuhamasishwa kuchangia mtaji katika benki hii kwa njia ya hisa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu kujenga Kiwanda cha Matrekta hapa nchini, Serikali inatambua umuhimu wake ikizingatiwa kuwa ni moja ya nyenzo zitakazowezesha kubadili kilimo chetu kuwa cha kisasa zaidi na chenye tija. Kutokana na umuhimu huo, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji cha Taifa yaani *Tanzania Investiment Centre (TIC),* inaendelea kutafuta wawekezaji mbalimbali wanaoweza kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya matrekta na zana nyingine za kilimo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na uwezo mdogo wa Serikali wa kujenga viwanda vya zana za kilimo yakiwemo matrekta, na kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Uwekezaji, Wizara yangu kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa, yaani *TIC*, inatafuta wawekezaji katika uzalishaji wa zana za kilimo.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri:-

Kwa kuwa, suala hili la uboreshaji wa kilimo katika nchi yetu ni la muda mrefu, na kwa kuwa, amesema kwamba Benki ya *TIB* imepewa jukumu hili. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja kubwa ya kuzungumza na mabenki maengine ili iweze kutoa mikopo kwa wakulima wadogo na kwa mazungumzo maalum ambayo yatajenga mazingira muafaka ya kumsaidia Mkulima na mabenki yenyewe yapate faida?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kumchaya, la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwamba niseme sasahivi sio *TIB* inayohusika, sasa hivi ni benki ya Maendeleo ndio inayohusika sasa kusaidia kwenye kilimo pamoja na ufugaji pamoja na sekta zingine, ziko kama 13 hivi. Na sekta hii ya kilimo kwa mwaka huu imepata bilioni 10 yaani mwaka 2007 bilioni 10. Mwaka jana ilikuwa bilioni, ilikuwa ni pungufu, niseme ilikuwa ni pungufu. Kwa hiyo, benki hii ya Maendeleo inajali zaidi na imejikita zaidi kwenye kilimo kuliko sekta zingine.

Niseme tu kwamba sheria hii ya *lease finance* ikishakamilishwa, ikishapitishwa na Bunge hili nadhani ndio itawezesha hata benki zingine kujiingiza katika biashara hii ya wakulima kukopa na kuweza kusaidiwa katika kilimo hasa katika kununua pembejeo na zana za kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niongeze maelezo kidogo tu kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu waziri, mwenzangu kwamba juzi Mheshimiwa *Senator* William shellukindo, aliwasilisha hoja hapa Bungeni, iliyokuwa na sura mbili. Moja ulikuwa ni mtizamo wa jinsi gani benki ya rasilimali inavyoweza kuwakopesha wakulima wadogo na ikiwa inaonesha kwamba kwa kweli benki hii haiwakopeshi wakulima wadogo, inajali wakulima wakubwa kama *TPC*, na wengine. Sura ya pili, aliwasilisha hoja ya kutaka kuwe na benki mbadala ambayo ni benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Sasa Mheshimiwa, nakumbuka Naibu Waziri, alisema kwa kuwa katika suala la uwezeshaji wa wakulima wadogo, tunazungumzia *Micro Finance*, kuna *options* kama mbili au tatu. Moja ni mabenki haya kuwa na idara itakayoshughulika na wakulima wadogo wadogo makusudi. Lakini ya pili ikawa ni suala ya kuanzisha benki ya wakulima wadogo. Wizara ya Fedha iliahidi kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu, itakuwa imeshafanya mchakato huu na itatuletea majawabu hapa Bungeni, nini kitakachofanyika kuhusu kuanzisha benki itakayoshughulika na wakulima wadogo.

Na. 167

### *Allowance* **Maalum kwa Walimu Wanaofundisha Vijijini**

**MHE. FUYA G. KIMBITA (K.n.y. AGGREY D. J. MWANRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, walimu katika Jimbo la Siha wametoa michango mikubwa katika kutekeleza mpango wa *MMEM* na katika mazingira magumu hasa ikizingatiwa kuwa wengi wanatembea mwendo mrefu kwenda shuleni kuwahudumia wanafunzi:-

Je, kwa nini serikali isitoe *allowance* maalumu kwa ajili ya Walimu wote Tanzania ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu hasa ya Vijijini kama ilivyo katika Jimbo la Siha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja na matatizo waliyonayo, walimu wametoa mchango mkubwa sana katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, *MMEM.* Serikali inatambua na kuthamini sana mchango wa walimu wote nchini. Bado inalifanyia kazi pendekezo la kuwapatia walimu posho maalum ya mazingira magumu ikiwa ni pamoja na kuangalia upya mfumo wa ajira ya walimu na uwezekano wa kuundwa kwa chombo kimoja cha Ajira na huduma kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa walimu. Aidha, serikali inautazama upya mfumo wa mishahara ya watumishi wote wa Serikali wakiwemo walimu kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Maslahi ya Wafanyakazi. Napenda nitumie fursa hii kuwashukuru walimu wote nchini kwa uvumilivu wao wa kufanya kazi katika mazingira magumu.

**MHE. FUYA G. KIMBITA (K.n.y. AGGREY D. J. MWANRI):** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ninaomba niulize swali moja la nyongeza.

Je, ni lini kile chombo tulichokipendekeza cha kuwahudumia walimu kwa maana kwamba walimu wahudumiwe na chombo kimoja, kitaanza?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niongezee kwa yale mazuri aliyokwisha kujibu Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuhusu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fuya, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwa sasa hivi Serikali inafanyia kazi suala la kuangalia jinsi ya kuwahudumia walimu kwa vizuri zaidi na kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba kuna chombo ambacho tunaangalia, ambacho tunadhani pengine kinaweza kikasaidia zaidi kwanza kusogeza huduma kwa walimu lakini pia kuleta ufanisi zaidi. Mpaka sasahivi tulishafanya utafiti, tulishawapa watafiti wakafanya hiyo kazi, vikao mbalimbali vya wadau vimeshafanyika, lakini zaidi ya hapo tulishaita *National Education Advisory Council*, yaani Baraza la Ushauri la Kielimu la Taifa ambalo nalo lilipitia. Sasa hivi iko kwenye ngazi ya juu zaidi ili kuangalia yale mapendekezo yaliyotokana na utafiti na maoni ya wadau mbalimbali yanafanyiwa kazi ili tuone hatima yake.Lakini nilitaka kumhakikishia kwamba ni jambo ambalo limefikia ngazi ya juu, linafanyiwa kazi. Tunaloomba tu, ni kwamba avute subira ili kile kitakachopatikana kiwe kweli kinaweza kuwasaidia walimu katika njia ambayo amezungumzia ya kuimarisha huduma kwa walimu.

Na. 168

**Maboresho ya Shule za Sekondari**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, sekondari nyingi zilizojengwa kwa mpango shirikishi zoko vijijini na zinakabiliwa na matatizo mengi kama barabara, nyumb za walimu, maji, zahanati na kadhalika; na kwa kuwa, uboreshaji unaofanywa na Serikali katika shule hizo wa kupeleka huduma muhimu utachukua muda mrefu:-

Je, Serikali inasema nini juu ya kuwapa posho ya mazingira magumu walimu wanaopangwa huko ili wakubali kwenda kufundisha huko kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa shule za sekondari za kata nyingi zinakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa huduma muhimu kama vile barabara, nyumba za walimu, maji na zahanati, hivyo walimu katika maeneo hayo wanafanya kazi katika mazingira magumu. Pendekezo la kuwapatia waalimu posho maalum ya mazingira magumu bado linafanyiwa kazi na Serikali ikiwa ni pamoja na kuangalia mfumo mzima wa ajira na uwezekano wa kuundwa chombo kimoja cha ajira ili kusogeza huduma karibu na walimu. Aidha, serikali inautazama upya mfumo wa mishahara ya watumishi wote wa Serikali wakiwemo walimu, kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Maslahi ya Wafanyakazi. Napenda nitumie fursa hii kuwashukuru walimu wote nchini kwa uvumilivu wao na kufanya kazi katika mazingira magumu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo mazuri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(a) La kwanza, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu waziri, amekiri kwamba kuna chombo kinachoshughulikia maslahi ya walimu wakati huu. Na kwa kuwa, walimu wana Chama chao cha Walimu; Je, Chama hicho cha walimu kimeshirikishwa kiasi gani katika chombo hicho kinachoangalia maslahi ya walimu?

(b) Kwa kuwa, katika matatizo yanayowakabili walimu wanaofundisha shule za kata zilizopo vijijini, yaliyo makubwa zaidi ni nyumba za walimu pamoja na umeme. Je, kwa kuwa, wananchi wako tayari kujenga nyumba za walimu. Je, serikali itashirikiana na wananchi kwa kiwango gani ili huduma ya kujenga nyumba za walimu iende haraka zaidi ili walimu waweze kupata nyumba kulingana na ikama ya walimu iliyoko vijijini pamoja na kuwapelekea umeme wa sola?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ili niongezee kwa yale ambayo ameyajibu vizuri sana Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kuhusu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Chilolo, ningependa kujibu kama ifuatavyo:-

(a) La kwanza amezungumzia kuhusu uundwaji wa chombo cha ajira na huduma kwa walimu kama kimeshirikisha Chama cha Walimu Tanzania. Ningependa kuhakikishia Bunge hili Tukufu kwamba tangu tulipoanza mchakato wa kushughulikia chombo kinachoweza kuhudumia walimu, Chama cha Walimu kimeshirikishwa kikamilifu kuanzia vikao vya awali kabisa.

Katika utafiti, katika matokeo ya utafiti, Chama cha Walimu kimeshirikishwa. Na pia tuliunda Kamati ndogo iliyokwenda nchi jirani kwenda kujifunza wenzetu wanafanyaje katika kuhudumia walimu, Chama cha Walimu pia kilituma Mwakilishi. Mpaka sasahivi Chama cha Walimu kimeshirikishwa vizuri kabisa, tunakwenda nao pamoja.

(b) La pili, ni kuhusu nyumba za walimu. Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuhakikishia Bunge hili kwamba Serikali ina nia nzuri sana katika kuangalia nyumba za walimu. Kama mnavyokumbuka Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha 2007/2008 katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi bilioni 20, bilioni 13.5 zimetumika katika kujenga nyumba za walimu 1500.

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba kila mkoa umepewa jumla ya nyumba 70 kwaajili ya kujengea nyumba za walimu, jambo ambalo ninaamini halijawahi kutendeka. Yaani kujenga nyumba 1500 kwa mwaka mmoja wa fedha haijawahi kutokea. Ikiwa ni ishara nzuri kabisa ya nia ya Serikali ya awamu ya nne

kuwajali walimu ili waweze kukaa katika maeneo ambayo hayana nyumba za walimu. Na kwa kufanya hivyo naamini kabisa kwamba serikali imechangia nguvu za wananchi.

Hizo nyumba 70 kwa kweli ni mchango tu wa serikali kwa nguvu za wananchi, pale ambapo itawezekana tutashukuru wakijenga hata 100 kwa sababu Serikali ilichofanya ni kuchangia tu nguvu za wananchi.

Lakini kila tutakapopata fedha basi tutachangia nguvu za wananchi. Naomba tuendelee na moyo huo na Mheshimiwa Mbunge na wengine wote nawaombeni kwa heshima na taadhima tushirikiane katika suala la upatikanaji wa umeme, kwa kuhusisha pia Wizara husika na Mheshimiwa Waziri mhusika anasikia. Hili linahitaji kushirikiana wote kwa pamoja, ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kupata umeme wa sola. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Na. 169

**Kupunguza ajali za Barabarani**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa, ajali za barabarani zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka, kwa mfano mwaka 2005 ziliripotiwa ajali 17,220 na mwaka 2006 zikaripotiwa ajali 18,187 ikiwa ni ongezeko la ajali 967; na kwa kuwa, ajali hizo husababisha maafa na hasara kubwa kwa Taifa:-

Je, Serikali sasa itachukua hatua gani za makusudi ili kuondosha tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mujibu wa Takwimu za mwaka 2005/2006 ajali za barabarani zimeongezeka. Sababu za kuongezeka kwa ajali za barabarani ni pamoja na ubovu wa magari, uzembe wa madereva, leseni za kughushi, uelewa mdogo wa watumiaji wa barabara juu ya sheria za usalama barabarani, ubovu wa barabara, mwendo wa kasi wa magari na kadhalika.

Hivyo ili kutatua tatizo hili, wadau wote wa usalama barabarani wanatakiwa kushirikiana katika kutokomeza ajali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na ajali hizi za barabarani Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(i) Serikali imetoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi kuyakamata magari yote mabovu na kuyachukulia hatua za kisheria.

(ii) Katika kudhibiti mwendo kasi, Serikali pia imeweka vituo vya kukagua ratiba za mabasi zitolewazo na *SUMATRA*. Kila basi lina ratiba inayoonesha muda wa kufika katika kituo husika.

(iii) Serikali inakusudia kutoa Leseni mpya za udereva ambazo ni *computarized*. Madereva wote watalazimika kupata mafunzo maalum kabla ya kupata leseni hizo. Mpango huo kwa kiasi kikubwa utasaidia kudhibiti leseni za kughushi.

(iv) Jeshi la Polisi limetakiwa kusimamia vizuri faini za papo kwa papo pamoja na kuwafikisha mahakamani wale wote wanaofanya makosa ya usalama barabarani.

(v) Kuweka kumbukumbu za makosa ya usalama barabarani, *Data Base*, mpango huu utasaidia kujua madereva wanaoongoza kwa makosa ya barabarani hivyo kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria ikiwemo kufungiwa leseni zao za udereva.

(vi) Serikali itaendelea kuzifanyia ukarabati sehemu korofi katika barabara zote na kuweka alama za usalama barabarani

(vii) Kutoa elimu kwa watumiaji wote wa barabara ili kuzielewa sheria za usalama barabarani. Kikosi cha usalama barabarani kimeanzisha kitengo cha elimu kwa lengo la utoaji wa elimu hiyo katika shule za msingi, sekondari na kwa watumiaji wengine wa barabara.

(viii) Jeshi la Polisi litaendelea kufanya doria katika barabara kuu ili kuyakamata magari yote yanayokiuka sheria za usalama barabarani.

Na. 170

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi - Ilembula**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kiko kilio kikubwa cha uhitaji wa kituo cha Polisi katika Jimbo la Njombe Magharibi:-

(a) Je, ni lini kituo hicho kitajengwa kwenye eneo la Ilembula ambako kuna uhalifu mkubwa?

(b) Kwa kuwa, ilifanyika Sensa ya wizi wa mifugo hasa ng'ombe katika Tarafa ya Wanging'ombe – wilaya ya Njome lakini matokeo ya zoezi hilo hayajatolewa; na kwa nini wale wezi waliopigiwa kwa hawajafikishwa kwenye vyombo vya Dola?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa huduma ya Polisi katika eneo hilo Jeshi la Polisi lina mpango wa kujenga kituo hicho ambao umeainishwa katika mkakati wa maendeleo wa muda mrefu wa Jeshi la Polisi na utatekelezwa kwa awamu kadiri hali ya bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo wakati tunasubiri kupatikana kwa fedha za ujenzi wa kituo hicho, uongozi wa kijiji cha Ilembula umelipatia Jeshi la polisi jengo la ofisi ya kijiji ambalo linahitaji kukarabatiwa ili liweze kutumika kama kituo cha Polisi. Hivi sasa taratibu za dharura zinachukuliwa ili kukamilisha ukarabati huo.

Jengo hilo litatumika kwa muda huku tukiendelea na ujenzi wa Kituo kipya cha kisasa kwa kushirikiana na wananchi wa eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sensa ya wezi wa mifugo ilifanyika katika Tarafa ya Wanging'ombe, wilaya ya Njombe mwezi Juni, 2004. Lakini baada ya uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi, hakukuwa na ushahidi wa kutosha kuthibitisha tuhuma hizo.

Hivyo, watu hao waliotajwa katika sensa hiyo hawakuweza kufikishwa Mahakamani, kwani matokeo pekee ya kura za maoni ya wananchi sio ushahidi unaoweza kupokelewa moja kwa moja na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kura hizo za maoni zinalisaidia sana Jeshi la Polisi kupata taarifa za awali za uhalifu na wahalifu hivyo kuwezesha harakati na mikakati ya Jeshi la Polisi kupambana na uhalifu katika eneo husika.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa usalama wa Raia. Pamoja na majibu mazuri nilikuwa naomba niulize maswali madogo ya nyongeza mawili:-

(a) Swali la kwanza, kwa kuwa, Serikali ya kijiji imeshatoa ofisi na imesha karabati ofisi pamoja na nyumba ya kukaa polisi. Je, ni lini polisi watapelekwa pale kwa sababu tayari ukarabati umeshatayarishwa?

(b) Swali la pili, kwa vile hii barabara inayotoka Dar-Es-Salaam kwenda Mbeya, kuna tatizo kubwa linajitokeza pale Halali – Iyai, kuna magari mengi yanaenda kasi pale na zinatokea ajali mbaya za kutisha mpaka inafikia hatua watu wanakatwa vichwa na magari yanayoenda kasi kwenda huko Mbeya. Je, ni lini Serikali itajenga matuta pale ili kuondokana na tatizo hili la ajali hizi za kutisha pale Halali – Njombe?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu maswali ya nyongeza yenye (a) na (b) ya Mheshimiwa Yono, kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusiana na lini tutapeleka askari katika jengo hilo, mara taratibu zote zitakapokamilika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa kuwa tutapeleka askari mapema iwezekananvyo. Kuna mambo kidogo yanahitajiwa kumalizika na yakishakuwa sawa basi tutawapeleka askari katika eneo hilo ili kahakikisha usalama wa eneo hilo unatekelezwa ipasavyo.

(b) Kuhusu magari yanayokwenda kwa kasi na kutaka kujengwa matuta katika sehemu hiyo, tutawasiliana na Wizara husika tuhakikishe kwamba kama kuna uhitaji wa kufanya hivyo, hatua zitachukuliwa.

Na. 171

**Magari Chakavu ya Serikali**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo ya ofisi za Serikali yamezungukwa na magari mabovu yaliyoegeshwa; na kwa kuwa, magari hayo yanakuwa kivutio na kishawishi kwa wahalifu kuiba vipuri au kujificha kwa uhalifu; na kwa kuwa magari hayo yanazuia nafasi na pia hayapendezi machoni:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni busara kutoa tamko la kuondoa magari hayo kwa kuyauza kwa mnada au kuyatoa kwa bei nafuu kwa wafanyakazi wao?

(b) Kwa kuwa, kuna sheria inayoruhusu magari mapya kununuliwa kila baada ya miaka mitano (5). Je, Serikali haioni kuwa ni vema kila baada ya muda huo kuuza magari machakavu yaliyodumu kwa muda huo?

(c) Je, Serikali haioni kuwa magari hayo kubaki Wizarani, Mikoani au Wilayani ni kuiletea mzigo mzito wa matumizi ya fedha za walipa kodi?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikian na Wizara ya Fedha kila mwaka hupata orodha ya magari machakavu kutoka Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea pamoja na Mikoa na Wilaya.

Baadaye Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara yangu huunda Kamati ya kufuta magari hayo na kisha kuyauza kwa mnada kwa hadhara kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

Lengo la hatua hii ni kupunguza idadi ya magari ya Serikali yaliyochakaa na ambayo hayatumiki tena kwa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Hata hivyo Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea kupeleka orodha ya magari machakavu kila mwaka Wizara ya Fedha ili magari hayo yaweze kufutwa kutoka katika vitabu vya Serikali na kisha kuuzwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo kwani kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, magari hayo yanakuwa kivutio na kishawishi kwa wahalifu kuiba na kujificha. *(Makofi)*

Pia yanazuia nafasi na hayapendezi machoni. Vilevile kuyauza magari hayo kabla hayajachakaa sana inasaidia Serikali kuokoa kiasi cha fedha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa naomba kuuliza hivi Serikali ina *data* za magari yake yanayoingia na kutoka kila baada ya miaka mitano kama alivyoeleza Naibu Waziri?

Je, ni kwanini basi magari yanayochakaa yanatoka kwa aliyemkubwa zaidi huko Serikalini na yanakwenda kwenye idara ambazo yanatumika kwa gharama kubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI MINDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba data za magari yanayoingia zote zipo na ninahakika kila Wizara na taasisi inayo idadi ya magari yanayoingia na kutoka. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama kuna magari yanatoka sehemu nyingine kwenda sehemu nyingine kufanya kazi ni kutoka tu na ukosefu tu wa fedha wa kununua magari mapya. Lakini si busara magari ambayo yamefika muda wake wa kufanya kazi yakapelekwa sehemu nyingine kufanya kazi ambayo itakuwa ni hasara kwa Serikali.

Na. 172

**Ubovu wa Vivuko vya Kigamboni**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuharibika kwa kivuko cha Kigamboni kumekuwa ni tatizo sugu kunakoweza kuhatalisha usalama wa watu na mali zao:-

Je, Serikal itakubali sasa kubinafsisha vivuko hivyo ili kupunguza usumbufu au tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU ( MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Katika Kivuko cha Kigamboni kuna Pantoni mbili *Mv. Kigamboni* na *Mv. Alina* zinazotoa huduma ya kuvusha abiria na mgari kuanzia saa 11 alfajiri hadi saa 7 usiku. Pantoni ya *Mv. Kigamboni* ina uwezo wa kubeba tani 160 na *Mv Alina* ina uwezo wa kubeba tani 100. Katika kuboresha huduma za Vivuko vya Kigamboni Wizara tayari imeanza kufanya yafuatayo; Ununuzi wa Injini mpya mbili kwa ajili ya Kivuko cha *Mv Alina* tayari umekamilika na injini zimefungwa. kivuko cha *Mv Kigamboni* kitafanyiwa matengenezo makubwa na mkandarasi wa kufanya kazi hiyo tayari amepatikana na kazi hiyo itakamilika ndani ya miezi 12, Ujenzi wa kivuko kipya chenye uwezo wa kubeba tani 500 tayari umeanza na utakamilika mwezi Mei, 2008 na taratibu za kukodi kivuko kingine kutoka nje ya nchi bado zinaendelea kukamilishwa na kivuko kinategemewa kuanza kazi mwishoni mwa mwezi Desemba, 2007.

Baada ya kusema hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Wizara haina mpango wa kubinafsisha vivuko hivyo kwa sasa badala yake inaviimarisha vivuko hivyo kwa kuvifanyia matengenezo makubwa pamoja na kununua vivuko vipya ili kuboresha huduma hiyo kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu ya utangulizi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri kasema kwamba Serikali haina mpango wa kubinafsisha vivuko hivi na kwa kuwa tatizo hili limekuwa sugu ni kwanini Serikali isichukue juhudi za dharura kuhakikisha kwamba inakipa kipaumbele kuweza kuhakikisha kwamba vivuko hivi vinakuwa katika hali usalama badala ya kuja kuchukua juhudi ya dharura baada ya wananchi kupoteza maisha kama ilivyotokea *Mv Bukoba.*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Sakaya juhudi zinafanywa za kuhakikisha kwamba vivuko hivyo vinakuwa salama wakati wote. Na wakati wote mle mnakuwa mna watu ambao wanakwenda navyo na tunahakikisha maboya na kile kinachohitajika katika vivuko vile viko katika hali inayohitajika, wakati juhudi zinafanywa ya kuhakikisha kwamba tunapata kivuko cha kukodi ambacho kitafika pale na kile kivuko kikubwa cha Kigamboni kipelekwe kwa matengenezo makubwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge saa ya imekwisha na maswali yamekwisha sasa kwanza naomba niwatambulishe wageni tulionao ambao nimeletewa taarifa zao hapa. Tunao vijana toka ya taasisi ya *TAYOA* Dar es Salaam wanaendelea na ziara ya mafunzo hapa Bungeni popote walipo wasimame, karibuni sana. (*Makofi*)

Ninao wageni wa Mheshimiwa Nuru Bafadhili, ni familia yake. Popote walipo wasimame, yupo mtoto wake, yupo mtoto wa mdogo wake, yuko na wifi yake. Halafu ninao wageni wa Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo ambao ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi. Tafadhali naomba wasimame kule ndani lazima niwataje. Kuna Spika wa Bunge hilo, kuna Naibu Spika, na Katibu Mkuu wa Bunge la Wanafunzi. Kwa hiyo, imekamilika Serikali. Basi karibuni sana, nadhani tutaongea mambo ikitakiwa. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa Msaidizi wa Spika anatangaza kwamba wale wajumbe wa Kamati teule ya kuchunguza *Richmond Development Corporation* wakutane na Mheshimiwa Spika kesho tarehe 15 Novemba, 2007 saa saba na nusu katika ukumbi wa Spika. Mheshimiwa ameagiza kwamba kabla ya hapo Kamati hiyo iwe imekutana na kuchagua Mwenyekiti wa Kamati yao. Halafu ameeleza kwamba Kamati hiyo teule inapewa wiki nne kukamilisha kazi zake na hivyo kukabidhi taarifa yao kwa Spika ifikapo tarehe 15 Desemba, 2007 siku ya Jumamosi. Kwa hiyo, kesho kuna kikao na kwamba muda wa kufanya kazi ni wiki nne.

Tangazo lingine ambalo ni muhimu Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kukamilisha kanuni zetu za kuendesha shughuli hapa Bungeni sasa zimepitia hatua mbalimbali lakini leo ndiyo hatua yake ya mwisho ya *consultation* ya kushauriana.

Kwa hiyo, Katibu wa Bunge anaomba niwakumbushe wajumbe wa Kamati ya Uongozi maana yake Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu wajumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge na Kamati ndogo iliyopewa jukumu la kuandaa mapendekezo ya kanuni wao watakutana saa tano hii katika ukumbi wa Spika. Kwa hiyo, ni makundi matatu Kamati ya Uongozi, Kamati ya Kanuni, na ile Kamati iliyoandaa mapendekezo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Ndugai inakutana saa tano hii katika ukumbi wa Spika. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Abdallah Kigoda anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo tarehe 14 kutakuwa na kikao cha Kamati kuanzia saa nne na nusu asubuhi hii katika ukumbi Na. 133 gorofa ya kwanza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa William Shellukindo, anawatangazia pia wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 14 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika saa saba mchana katika ukumbi Na. 432 gorofa ya nne, nadhani anajua kwamba kuna Kamati ile ya Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo anasema kikao hicho kitakuwa kifupi sana na ni dakika thelathini kwa hiyo ni muhimu wajumbe wake wawahi kusudi wawahi kikao hiki cha uwekezaji halafu waendelee na mkutano ule mwingine.

Kuna Kamati Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Shaban Kwaagw', yeye anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala na Kamati ya Huduma za Jamii kuwa kutakuwa na kikao cha pamoja katika ukumbi wa Msekwa saa tano asubuhi. Kwa hiyo, kuna wageni hapa naona wanagongana lakini wata *sort out* wenyewe itakavyokuwa, kwa hiyo kuna Kamati mbili zinakutana pamoja Kamati ya Katiba Sheria na Utawala na Kamati ya Huduma za Jamii watakutana katika ukumbi wa Msekwa saa tano hii.

Baada ya hapo tunaendelea na shughuli zingine za Bunge, Katibu, endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mkiangalia *Order Paper* ya leo utakuta tuna maazimio matatu, maazimio mawili yako katika Wizara ya Maliasili na Utalii na Azimio lingine liko katika Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia, sasa yale maazimio yaliyochini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kiwango kikubwa yanafanana isipokuwa jiografia tu nyingine iko hifadhi mpya ya Mkomazi, mwingine hifadhi ya taifa ya Ruaha. Kwa hiyo, Waziri atayawasilisha kwa pamoja wasemaji wa Kamati

zilizohusika watajibu kwa pamoja, wasemaji wa Kambi ya Upinzani watajibu kwa pamoja tutaendelea kujadili kwa pamoja, isipokuwa tutakapofika kwenye maamuzi tutaamua azimio moja baada ya jingine.
Kwa hiyo basi kabla ya hapo namwita Mheshimiwa Blandes ametoa huduma ya kusaini fomu zile za Maadili katika ofisi tutakayompangia sisi kwa Wabunge wanaotaka kupata *signature* ya Mwanasheria yeye ni Mwanasheria wa kujitegemea mnapewa huduma hizo *free,* kwa hiyo anawapeni huduma *free*, tutawaambia ni ofisi gani anakuwa anapatikan. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**Azimio la Kuridhia Kupanuliwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha**

**Na**

**Azimio la Kuridhia kuanzisha Hifadhi Mpya ya Taifa ya Mkomazi**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuhusu kupanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuanzisha Hifadhi Mpya ya Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maelezo mafupi kuhusu maazimio ya kuridhia upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na uanzishwaji wa Hifadhi Mpya ya Mkomazi naomba kuungana na Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa Bunge lako Tukufu, wananchi kwa Mkoa wa Kilimanjaro, familia na taifa kwa ujumla kwa kuondekewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba Mwenyezi Mungu Mtukufu wa Rehema ailaze mahali pema peponi Roho ya Marehemu. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoa salaam za pole kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Nchinga, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mbunge wa Urambo na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, kwa ajali ambazo wamezipata. Mwenyezi Mungu awajalie wapone mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam za pole, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Taifa. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge na wana CCM wengine walioshinda na kupewa nyadhifa mbalimbali katika chama chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo na kabla ya kuliomba Bunge lako Tukufu kuridhia maazimio ya Serikali ya kupanua hifadhi za Ruaha na kuanzisha hifadhi mpya ya Mkomazi, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu hifadhi hizo kama ifuatavyo:-

Kwanza kupanua hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Pori la Akiba Usangu lina ukubwa wa kilomita za mraba 4148 na maeneo muhimu ya ardhi oevu kwa mtiririko wa maji ya

mto Ruaha *(Great Ruaha)* yana ukubwa wa kilomita za mraba 15,500. Kati ya ardhi yoevu muhimu ipo pia ardhi oevu ya Ihefu. Hoja hii inapendekeza pori la Akiba la Usangu pamoja na ardhi yoevu muhimu zenye ukubwa wa kilomita za mraba 5778 ikiwemo Ihefu ziunganishwe na hifadhi ya taifa ya Ruaha. Pori la Akiba la Usangu kwa sasa linasimamiwa na Sheria ya Hifadhi ya Wanyapori, sura 283 iliyorekebishwa mwaka 2002. Maeneo muhimu ya ardhi oevu nje ya hifadhi hiyo yamo kwenye ardhi za vijiji na ardhi za jumla. Hoja hii ikikubalika itafanya hifadhi ya Taifa ya Ruaha iwe na ukubwa wa kilomita za mraba 20,226,000 na hivyo kuifanya iwe kubwa kuliko hifadhi zote barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba la Usangu na maeneo ya Ardhi Oevu za Usangu ni muhimu sana katika kutunza na kuhifadhi maji kwa ajili ya Bwawa la Mtera. Hoja ya Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha inalenga katika kuhifadhi vyanzo vya maji na kuongeza maji kwenye Bonde la Usangu kutoka kiwango cha sasa hadi kiwango kitakachohakikisha kwamba Mto Ruaha Mkubwa unaweza kutiririka maji mwaka mzima.

Kuongeza uwingi na ubora wa maji ya Mto Ruaha na Bwawa la Mtera, kuwezesha ardhi oevu zenye kazi ya uchujaji wa kemikali zinazotumika katika mashamba ya mpunga kama mbolea na dawa mbalimbali, kupunguza magugu na hivyo kuongeza usalama wa maji kutoka kwenye vyanzo vya ardhi oevu hiyo. Kupanua uwigo wa ajira kwa wananchi kwa kupanua shughuli za utalii na kuhakikisha kuwa maji yanapatikana wakati wote kwa ajili ya kuzalisha umeme katika Bwawa la Mtera na mwisho kuboresha shughuli za uvuvi katika Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukubalika kwa hoja hii kutavigusa vijiji 11 na vitongoji 5 ambavyo inabidi vipewe fidia na kuhamia maeneo mengine. Mkakati umewekwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mbeya, kuhakikisha kwamba wananchi wanalipwa fidia inayostahili na kwamba wale wanaohamishwa wanapatiwa huduma muhimu za jamii. Tayari wananchi wanaoguswa na maamuzi haya wameanza kulipwa fidia kupitia benki ya *NMB* ya Wilaya ya Mbarali. Jumla ya shilingi bilioni 2.75 zimekwishalipwa na wananchi wengine wataendelea kulipwa fidia na Wizara yangu imelenga kuwa zoezi la malipo likamilike katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa wapo watumishi 142 katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Watumishi 120 zaidi wanahitajika kusimamia ukubwa wa kilomita za mraba 9926 zinazoongezeka katika hifadhi ya taifa ya Ruaha. Mahitaji haya yamo katika Bajeti na yataendelea kutengwa katika Bajeti za *TANAPA* mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko yanayokusudiwa yatalazimu kufanyika marekebisho ya jedwali lililopo katika tangazo la Serikali namba 436 A la mwaka 1998 lililotangaza Pori la Akiba la Usanga na jedwali lililotangaza Hifadhi ya Taifa la Ruaha katika Sheria ya Hifadhi za Taifa sura 282 kuhusiana na kuhamisha usimamizi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulinda maeneo yatakayounganishwa na hifadhi ya Taifa ya Ruaha inahitajika pia kulinda mazingira nje ya eneo hilo. Wizara yangu itafanya kazi kwa karibu na wadau wengine ambao wameshabainishwa katika kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi, kutekeleza sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004, kutekeleza sheria ya maji katika kugawa haki ya kutumia na kusimamia maji, kuandaa programu ya ujirani mwema ya *TANAPA* na kuitekeleza na kupitia mpango wa usimamizi na uendelezaji wa Hifadhi ya Ruaha ikiwa inajumuisha maeneo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe maelezo mafupi kuhusu hifadhi mpya inayopendekezwa ya Mkomazi. Hifadhi Mpya ya Mkomazi inayopendekezwa inatokana na mapori ya Akiba ya Mkomazi na Umba ambayo yanasimamiwa na Wizara ya Maliasili na utalii kwa sheria ya Hifadhi za Wanyamapori sura 283 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002.

Mapori haya mawili yana ukubwa wa jumla ya kilomita za mraba 3245. Hivyo hoja hii inapendekeza kuanzisha hifadhi mpya ya Taifa ya Mkomazi yenye ukubwa wa kilomita za mraba 3245.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapori ya Mkomazi na Umba yalitokana na Pori Kubwa la Akiba la Ruvu lililoanzishwa mwaka 1951. Pori la Akiba la Ruvu lilimegwa kwa nyakati tofauti ili kupisha shughuli za kibinadamu hususan kilimo na ufugaji. Sera ya madaraka ya Mikoani ya mwaka 1972 mpaka 1973 ilisababisha pori la Akiba la Mkomazi kugawanywa hivyo sehemu ya pori iliyopo Mkoa wa Kilimanjaro ikaitwa Mkomazi na sehemu ya Mkoa wa Tanga ikawa Pori la Akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za binadamu katika mapori haya kwa miaka mingi zilifanya *specie* mbalimbali za wanyamapori kuathirika na hata kutoweka kutokana na ujangili. Tembo walipungua kutoka mwaka 1969 hadi kufikia tembo 93, mwaka 1988, ujangili, kilimo na ufugaji vilisababisha wanyama wengine kama faru mweusi, nyumbu mashariki, tandala mkubwa, palahala, taya kusi na mbega mweupe kutoweka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 1988 Serikali iliweka usimamizi wa mapori haya chini ya Serikali kuu na kuanzisha miradi ya ukarabati na ushirikishaji jamii inayozunguka kwenye hifadhi ya mapori hayo. Mikakati hiyo iliwezesha tembo kuongezeka hadi kufikia 195 mwaka 1999, kuanzia mwaka 1997 mpaka 2001 faru weusi nane walipandikizwa kwenye pori la Mkomazi. Hivi sasa faru hao wameongezeka kufikia kumi na wawili. Hoja hii inalenga katika kuboresha zaidi uhifadhi kwenye mapori ya Mkomazi na Umba ili kulinda *bioanuwai* za pekee za eneo hilo hususan *species* za wanyama pori zilizo adimu au zilizo katika hatari ya kutoweka na kukuza rasilimali ya wanyama pori kwa ajili ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja kutapanua wigo wa ajira kwa wananchi kutokana na kupanuka kwa shughuli za utalii na kutoa ulinzi wa *bioanuwai*.

Wizara yangu itashirikiana na wadau katika usimamizi wa hifadhi mpya inayozunguka mapori hayo mapya kwa kuandaa mpango wa uendelezaji rasimali nje ya hifadhi. Kuanzisha mpango wa usimamizi na uendelezaji wa hifadhi hiyo mpya. Kuweka sheria na Kanuni na taratibu za usimamizi wa hifadhi na kuandaa programu ya ujirani mwema kwa kuweka miundombinu inayofaa na yenye viwango vinavyokubalika ndani na nje ya hifadhi kwa ajili ya uendelezaji utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko yanayokusudiwa yatailazimu kuifanyia marekebisho jedwali Na. 6 na 17 ya tangazo la Serikali Na. 275 la Mwaka 1974 lililotayarishwa chini ya sheria ya hifadhi ya wanyama pori sura 283 na vilevile katika sheria ya hifadhi ya taifa sura 282 kuhusiana na kuhamisha usimamizi wa maeneo ya Mkomazi na Umba chini ya Hifadhi ya Taifa.

Mwisho naomba Bunge lako Tukufu liliridhie maazimio haya ili kuwezesha uhifadhi endelevu wa maeneo haya na kuendeleza utalii katika eneo la Mkomazi na Umba na vilevile kuboresha mtiririko wa maji ndani ya Bwawa la Mtera kutokana na uhifadhi endelevu wa ardhi oevu ya Bonde la Usangu kwa kupanua Hifadhi ya Ruaha. Sasa nitayasoma Maazimio yenyewe moja hadi jingine.

Kwanza, Azimio la Bunge la Kuridhai Kupanua kwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

KWA KUWA Sera ya Hifadhi ya Taifa ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda *bioanuwai* katika mtandao wa Hifadhi ya Taifa.

NA KWA KUWA, Serikali imeweka mkakati wa hifadhi ya mazingira ya ardhi, utunzaji wa ardhi oevu na vyanzo vya maji ambapo maeneya ardhi oevu ya Usangu yamepewe kipaumbele;

NA KWA KUWA, Ardhi oevu ya Usangu ni muhimu katika hifadhi ya maji kwa ajili ya Bwawa la Mtera na kwamba hifadhi hiyo ni muhimu ikisimamiwa na sheria ya Hifadhi za Taifa;

NA KWA KUWA, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha lipo maeneo ya ardhi oevu, haikidhi mahitaji ya uhifadhi endelevu kwa kutoa ulinzi madhubuti kwa maeneo ya ardhi oevu ya Usangu;

NA KWA KUWA, pori la akiba la Usangu na maeneo mengine ya ardhi oevu ya Usangu yakipandishwa hadhi ya kujumuishwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, hali ya utunzaji wa ardhi oevu na uhifadhi endelevu utaimarika.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa mafungu ya tatu na nne ya sheria ya Hifadhi ya Taifa sura 282 ni sharti kupata ridhaa ya Bunge ili kuweza kuyapandisha hadhi na kuyajumuisha katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ardhi oevu ya Usangu na pori la akiba la Usangu;

HIVYO BASI, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wake Tisa sasa linaridhia Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupanuliwa kutoka kilomita za mraba 10,300 hadi kufikia 20,226 na kuipandisha hadhi ya kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili kujumuisha pori la akiba la Usangu lenye kilomita za mraba 4,148 na ardhi oevu ya Bonde la Usangu na maeneo ya miinuko yenye kilometa za mraba 5,778 ili Hifadhi ya Taifa ya Ruaha sasa kuwa na mipaka kama ilivyoainishwa katika jedwali ambalo limeambatanishwa kwa ajili ya upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge Kuridhia Kuanzishwa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

NA KWA KUWA, Sera ya Hifadhi ya Taifa ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhi na kulinda *bioanuwai* katika mtandao wa Hifadhi za Taifa na kwa kuwa mapori ya akiba ya Mkomazi na Umba ni muhimu kwa kuhifadhi *bioanuwai* za kipekee, hususan wanyama na mimea.

NA KWA KUWA, hadhi ya pori ya akiba la Hifadhi ya Taifa ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhi na kulinda *bioanuwai* katika mtandao wa hifadhi za Taifa na kwa kuwa mapori ya akiba na mkomazi na Umba ni muhimu kwa kuhifadhi *bioanuwai* za kipekee, hususan wanyama na mimea ya ukanda wa Sudan au Somalia;

NA KWA KUWA, hadhi ya pori la akiba haikidhi mahitaji ya kutumia rasilimali za asili kwa kuendeleza utalii waikolojia kwa kutazama viumbe na maeneo asilia;

NA KWA KUWA, mapori ya akiba ya Mkomazi na Umba yakipandishwa hadhi na kuunganishwa kuwa eneo moja la hifadhi haja ya kutoa ulinzi *species* zilizoko katika hatari ya kutoweka *bioanuwai* muhimu na uendeleza wa utalii itatimia;

NA KWA KUWA, ili mapori ya akiba ya Mkomazi na Umba yapandishwe hadhi na kuwa hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano la Tanzania inahitajika;

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi kwa kuzingatia manufaa ambayo Tanzania itapata kutokana na kuanzishwa kwa Hifadhi mpya ya Mkomazi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa fungu namba tatu na namba nne ya Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura 282, katika Mkutano wake wa Tisa, sasa linaazimia kuridhia kuanzishwa kwa Hifadhi mpya ya Taifa ya Mkomazi yenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,245 na yenye mipaka kama ilivyoanishwa katika jedwali lililoambatanishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Hifadhi mpya ya Taifa ya Ruaha, kwa kuongezwa katika hifadhi ya sasa ya Ruaha kwa Pori la Akiba la Usangu na eneo la Ihefu. Pia kuanzishwa kwa Hifadhi mpya ya Mkomazi kutokana na Pori la akiba la Mkomazi na Umba, kwa mujibu wa Kanuni Na.101(2)(ii) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, Kamati imeshughulikia mapendekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha maoni haya, kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa salamu zetu za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Tunaomba Mwenyenzi Mungu ailaze Roho ya marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa salaam za pole kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum na wengine wote ambao kwa namna moja au nyingine walikumbwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu za pole, pia kwa niaba ya Kamati yangu tunapenda kutoa pongezi zetu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kwa kunipa heshima ya kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo nao ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti na Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula na Mheshimiwa Lucy Mayenga. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed R. Soud, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Juma S. Nhunga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa sababu kubwa na umuhimu wa kuridhia Maazimio haya ni pamoja na:-

(i) Kuhifadhi vyanzo vya maji na na kuongeza maji kwenye Bonde la Usangu kutoka kiwango cha sasa, hadi kiwango kitakachohakikisha kwamba Mto Ruaha Mkubwa unaweza kutiririka kwa mwaka mzima;

(ii) Kuongeza wingi na ubora wa maji ya Mto Ruaha Mkubwa na Bwawa la Mtera, ili kuhakikisha Taifa linapata Umeme wa hakika;

(iii) Kuwezesha ardhi oevu zifanye kazi ya uchujaji wa kemikali zinazotumika katika mashamba ya mpunga kama mbolea na dawa za kupunguza magugu, hiyvo, kuongeza usalama wa maji kutoka kwenye vyanzo hivyo;

(iv) Kupanua wigo wa ajira kwa wananchi kwa kupanua shughuli za utalii;

(v) Kuhakikisha kuwa maji yanapatikana wakati wote kwa ajili ya kuzalisha umeme katika Bwawa la Mtera na Kidatu;

(vi) Kuboresha shughuli za uvuvi katika Bwawa la Mtera;

(vii) Kutoa nafasi kwa *TANAPA* kuhakikisha kuwepo kwa vyanzo vya maji vya uhakika katika hifadhi ya Mkomazi kama mabwawa ya uhakika ili yawepo maji kwa ajili ya wanyamapori kwa kipindi chote cha mwaka mzima kwa vile Mkomazi ina tatizo kubwa la ukame;

(viii) Ili kuimarisha ulinzi katika hifadhi hii tarajiwa, Kamati inashauri Serikali iongeze idadi ya askari wahifadhi kwa sababu waliopo hawakidhi mahitaji ya kupambana na ujangili, moto kichaa na uvamizi wa mifugo kwenye hifadhi;

(ix) Serikali ione umuhimu hapo baadaye kuliingiza katika mfumo wa Hifadhi za Taifa eneo la msitu wa hifadhi wa Shengena ambao ni chanzo cha maji kwa meneo ya tambarare ya Same Magharibi na Mashariki;

(x) Serikali ione umuhimu wa kuyaangalia maeneo yote nchini yaliyohifadhiwa kama *Forest Reserves*, *Game Reserves, Marine Reserves* na *National Parks* ili kuyapanga vema na kuyapa hadhi ambayo itasaidia uhifadhi endelevu na kukuza utalii; na

(xi) Serikali iliangalie kipekee Pori la Akiba la *Selous*, ambalo lina Tembo wengi sana kuliko pori jingine lolote Afrika kwa kulianzishia Mamlaka pekee ya kulihifadhi pori hilo lenye Bodi ya Uendeshaji ili kuliwezesha kuchukua nafasi yake katika uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati, baada ya kujadili Azimio hili kwa kina, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:

1. Ili kuondoa kero miongoni mwa Wananchi ambao itabidi wahame eneo la Ihefu kupisha upanuzi wa hifadhi ya Ruaha, suala la malipo ya fidia kwa mali na mashamba lifanywe kwa uangalifu mkubwa kuepusha malalamiko na usumbufu kwa wananchi. Wananchi wahusika wote walipwe kabla ya kuhama;

2. Kwa vile eneo la hifadhi litaongezeka kutoka kilomita za mraba 10,300 hadi kufikia kilomita za mraba 20,226 ni vema utaratibu mzuri uandaliwe kuhahakikisha watumishi wa kutosha wanaajiriwa na hususani Askari wa kulinda eneo hilo.

   Aidha, mipaka iangaliwe vema katika kuanzisha Hifadhi za Taifa na mapori ya akiba ili kuondoa utata wa mipaka;

3. Mfumo wa Hifadhi za Misitu, Wanyamapori (Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba) uangaliwe upya na ikiwezekana Shirika jipya la Mapori ya Akiba (*Tanzania Wildlife Reserves* - *TAWIRE*) lianzishwe ambalo litakuwa na Bodi yake itakayofanya kazi kwa utaalam, kibiashara na ufanisi zaidi; na

4. Kamati inashauri Serikali iipunguzie *TANAPA* kodi (*Corporation Tax*) kwa vile tunaiongezea majukumu makubwa ya uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kumpongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maofisa wengine kwa kuwasilisha maazimio haya mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni haya, Kamati katika ujumla wake haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa maazimio haya na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru tena Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kwa maoni na ushauri waliotoa kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni haya, Kamati inaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa shukrani zangu kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu uanzishwaji wa Hifadhi mpya ya Taifa ya Mkomazi na kupanua hifadhi ya Ruaha kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(5)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wake kwa ujasiri waliouonyesha kwa kuleta Maazimio haya ambayo ni muhimu sana kwa uhifadhi wa maliasili za Watanzania ili Bunge lako Tukufu liweze kuyaridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyapitia Maazimio haya kwa pamoja na taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri aliwasilisha kwenye Kamati ya Maliasili na Mazingira, Kambi ya Upinzani haina pingamizi dhidi ya uridhiwaji wa Maazimio hayo, ila inasisitiza kuwapo angalizo kuhusiana na taratibu nzima zitakazotumika kwa manufaa ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri amezitoa kuhusu ukubwa wa hifadhi mpya ya Ruaha kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 20,226 na hivyo kuwa hifadhi kubwa kuliko zote katika Bara la Afrika, ni dhahiri kuwa usimamizi wake utakuwa mgumu sana ikizingatiwa hifadhi ya Ruaha kwa sasa hivi kabla haijaongezwa eneo la Ihefu na Bonde la Usangu ni Kilomita za mraba 10,300 na bado wimbi la ujangili ni kubwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze Bunge hili ni mikakati gani ya dhati iliyoandaliwa ya kusimamia hifadhi hii kwa ufanisi ili kukidhi malengo yaliyokusudiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inashauri katika suala la ajira, ziangalie vijana wenye uwezo wanaozunguka hifadhi hizi ili kuimarisha mahusiano mazuri na wananchi na hivyo kushiriki kinakamilifu katika kutunza hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upanuaji mzima wa hifadhi ya Ruaha kuna wananchi waliohamishwa na pia katika kuanzisha hifadhi mpya ya Mkomazi kuna wananchi wataohamishwa kutoka katika maeneo ambayo yalikuwa ndizo ofisi zao, maana kwamba maisha yao ya kila siku yalikuwa yanategemea ardhi ambayo imetengwa kuwa hifadhi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wote waliohamishwa wanapatiwa stahili zao mapema na kutengewa maeneo mengine ambayo watayatumia kuendeshea maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uanzishwaji wa Hifadhi hizi za Taifa, kuna faida nyingi ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja katika taarifa yake kwa Kamati kwa kulinganisha na kuwa na mapori ya akiba (*game reserves*), ila pamoja na hayo suala la kushirikisha jamii ambazo zimezunguka hifadhi hizo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hadi hivi sasa Tanzania ina jumla ya Hifadhi za Taifa (*National Parks*) 14 na Mapori ya Akiba (*Game Reserves*) zaidi ya 20,

jambo la kujiuliza kwa kufanya ulinganisho ni eneo gani kati ya hayo wananchi wa jamii zilizozunguka maeneo husika zinanufaika? Kwa uhakika ni wazi kuwa kwenye Hifadhi za Taifa (*National Parks*) kuna faida nyingi kwa Taifa na jamii zinazozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia ukweli kuwa ukubwa wa pori moja tu la *Selous* ni zaidi ya muungano wa hifadhi zote za Taifa na mbuga hiyo ya *Selous* inamilikiwa na makampuni yasiozidi kumi. Sisi kama Watanzania tunapata mapato kiasi gani kutokana na mbuga hiyo kwa kulinganisha na hifadhi zote za Taifa?

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iangalie maeneo yote ya mapori ya akiba yanayoweza kupandishwa hadhi kuwa hifadhi za Taifa (*National Parks*) ili kuhakikisha rasilimali za Watanzania zinakuwa katika uhifadhi endelevu, kuongeza pato la Taifa na kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuziweka mbuga zetu kwenye uhalisia wake, Kambi ya Upinzani inashauri hoteli za kitalii zijengwe nje ya mbuga na kama hapana budi kujengwa ndani ya mbuga, Serikali ichukue tahadhari za kutosha wanapokuja wawekezaji wanataka kujenga hoteli mpya ni lazima kuzingatia *GMPs* (*General Management Plans*) pamoja na tathmini ya athari za mazingira (*EIA*) ya maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa makini na maliasili za Watanzania kwani isije kuwa mambo haya ambayo yanapewa baraka za Bunge hili baadaye kinakuwa kibali kwa watu fulani kuweza kujimilikisha kwa urahisi kwani tayari wananchi watakuwa wamekwishaondolewa katika maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninawashukuruni wote kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge hizi ni hoja mbili tunajadili kwa pamoja na mpaka sasa nina wasemaji nane walioomba na nafasi nadhani bado ipo. Kwa hiyo nitawaita Waheshimiwa wawili wa wanyamapori lakini pia ni kwa sababu ni Wenyeviti wa Kamati za Bunge ni Kamati ya Uongozi. Kwanza nitamwita Mheshimiwa Job Ndugai, halafu nitamwita Mheshimiwa Mgana Msindai, wenyewe wote ni wataalam wa wanyamapori.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kwanza ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya kupandisha hadhi Pori la Mkomazi ili liwe Hifadhi ya Taifa lakini pili kuliongezea eneo Hifadhi ya Ruaha ikihusisha Pori la Usangu na maeneo ya Ihefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri, kama ulivyosema mimi ni mdau wa karibu, ninayafahamu mapori haya mawili vizuri sana. Kwa mara ya kwanza nilienda kule Mkomazi nikiwa mwanafunzi wa Mweka miaka 20 iliyopita, tulitembea kwa miguu,

tulitembea kwa gari na tulienda kwa ndege pia. Kwa hiyo, ninalikumbuka vizuri sana pori lile. Pia nimeenda mara kadhaa hata mwezi uliopita nilipita pale Mkomazi, nilikuwa nikipita maeneo hayo nikawakuta vijana nikawasalimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza sana wahifadhi wa Idara ya Wanyamapori ambao wamekuwa wakihifadhi mapori yote haya mawili tunayoyapandisha hadhi leo Pori la Mkomazi, Umba, *Game Reserve* na lile la Usangu na maeneo yaliyokuwa nje ya Ihefu. Ninawapongeza sana kwa vile ambavyo wamefanya kazi kwa miaka mingi katika hali ngumu sana ya bajeti ndogo za Kiserikali, kukosekana kwa magari na nyenzo …

**NAIBU SPIKA:** Tafadhali nikukatishe, wajumbe wa Kamati ya Uongozi mnatakiwa kwenye kikao, ninawaona kina Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa George Lubeleje, nadhani labda hawakusikia nilipotangaza.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa hiyo, naunga mkono hoja iliyo mbele yetu aliyoileta Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ya kuyapandisha hadhi mapori haya ili yawe Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na Pori la Mkomazi linalopakana na Hifadhi ya Savo upande wa Kenya ambapo ndio mbuga kubwa kwa upande wa Kenya kuliko zote, yenye hifadhi kubwa sana ya tembo. Kwa hiyo, ni eneo muhimu ni eneo zuri sana kiuhifadhi na kwa Mkomazi ndiyo eneo ambalo tulikuwa tunalitegemea sana kwa aina ya wanyama wanaoitwa Lesakudu ambao wanapotea sana katika nchi yetu. Kwa hiyo, kuhifadhiwa kwake kwa kiwango cha *National Park*, kutasaidia sana kuwahifadhi wanyama hawa lakini pia na wanyama wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Mkomazi kuna faru, faru wale wako kwenye uzio tofauti na maeneo mengine, kwa hiyo, wanahitaji uangalizi wa karibu sana. Ninapenda Wizara iwe makini katika kuangalia namna ya huyu bwana Fis John kama aendelee au asiendelee. Amekuwa akihifadhi faru hawa kwa sababu uhifadhi wa faru unahitaji fedha nyingi sana. Faru wanalindwa masaa 24, ni gharama kubwa sana kumlinda faru lazima uwe na Askari wa kutosha, lazima uwe na magari ya kutosha, lazima uwe na ndege, ni ulinzi wa hakika. Kwa hiyo, kama umuhimu wa huyu bwana kuendelea kuwepo bado utakuwepo na kwa sababu faru hao wako katika maeneo ya uzio, basi litazamwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema kwa Mkomazi jirani yake iko misitu inayoitwa misitu ya Shengena, msitu muhimu sana kwa ajili ya vyanzo vya maji vya maeneo ya Same Mashariki na Same Magharibu. Tunaomba sana na kuishauri Wizara mbele ya safari iangalie uwezekano wa misitu hii ya Shengena kuwa sehemu ya hifadhi mpya ya Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo ambalo ningependa kulileta mbele ya Bunge ni kwamba badala ya kwenda vipande vipande kama tunavyofanya sasa, tunapandisha hifadhi mbili kuwa hifadhi ya Taifa, ninaomba Serikali iangalie upya

*system* nzima ya maeneo ya hifadhi katika nchi. Tuna maeneo ya Hifadhi ya Bahari ambayo tunayaita *Marine Reserves* na *Marine Parks* haya yapo chini ya Idara ya Uvuvi kwenye shirika linalojitegemea lenye sheria yake, tuna maeneo ya *National Parks*, tuna maeneo ya Ngorongoro, tuna maeneo ya *Game Reserves* ambayo yako chini ya Idara ya Wanyamapori lakini vile vile tuna *Forest Reserves*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba iko haja ya kutizama *system* nzima ya maeneo ya hifadhi ili kila eneo lipangwe mahali linapofaa maana maeneo haya sababu zake nyingi ni za miaka ya 60. Nikitoa mfano tunayo *Serengeti National Park*, *Maswa Game Reserve*, *Kijereshi Game Reserve*, *Gurumeti Game Reserve*, *Ikorongo Game Reserve* na katika mpango wa kukuza utalii katika eneo zima la Serengeti je, kuna sababu za kutosha za kuendelea kuwa na *Game Reserve* zilizozunguka Serengeti? Kwa nini tusiwe na *a larger Serengeti* ambayo inachukua na hiyo Maswa na Igurumeti na kadhalika, ikawa ni *park* moja kubwa ikapangwa vizuri matumizi yake, tukapanga utaratibu wa utalii mzuri zaidi, tukatawanya mahoteli ya kitalii vizuri zaidi na tukavuma fedha nyingi zaidi, kwa nini tuendelee kuwa na vipande vipande hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Hifadhi ya *Seleous Game Reserve.* Wamesema hapa kwamba Ruaha ndiyo itakuwa hifadhi kubwa *Africa*, hifadhi kubwa kwa maana ya *National Park* kubwa lakini Hifadhi kubwa ni *Seleous Game Reserve Africa* nzima. Seleous *Game Reserve* ina kilometa za mraba peke yake elfu hamsini na kitu hivi. Seleous *Game Reserve* ni sawa sawa na Rwanda na Burundi kwa pamoja yaani Rwanda na Burundi kwa pamoja *Game Reserve* moja. Selous *Game Reserve* ina tembo zaidi ya 70,000. Ndilo eneo lenye tembo wengi dunia nzima, hakuna. *Seleou Game Reserve* ni *World Heritage Site. Selous Game Reserve* ndilo eneo ambalo lina faru wengi kuliko pori lingine lolote katika Tanzania. *Selous Game Reserve* ndilo eneo ambalo lina mbwa mwitu wengi kuliko pori lingine lolote. Lina *eco-systems* kadhaa na ni pori lenye *potentials* nyingi sana linaloweza kutuletea fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini pori hili kubwa kiasi hicho lisiundiwe utaratibu wa kuliendesha peke yake kama Ngorongoro? Ikaletwa sheria hapa tukapitisha ikawa na bodi yake, likaweza kujiendesha katika mazingira ya sasa. Mnajua Serikali haiendi sana kwenye kufanya biashara, inayaachia mashirika na watu binafsi, *Seleou Game Reserve* kwa mwaka jana peke yake imeingiza dola karibu bilioni nane za shilingi za Tanzania. Katika fedha hizo, wao fedha za kutumia ndani ya *Seleou Game Reserve* wamepewa bilioni moja tu, bilioni moja kwa eneo la ukubwa wa sawa na Burundi na Rwanda je, ni matumizi mazuri hayo? Bajeti ya Serikali inawaathiri. Iko haja ya maeneo haya ambayo ni urithi wetu sisi Watanzania tukayatazama kipekee, yakatuingizia mapato ya uhakika. Hifadhi hizi ndiyo dhahabu yetu ya uhakika, tukiendelea kulindi hifadhi hizi, kuzitunza vizuri, kuwalinda wanyama hawa wakawa endelevu, tuna uhakika wa kuwa na mapato yatakayosaidia kuendeleza nchi yetu kwa miaka mingi ijayo. Dhahabu siku moja itaisha lakini wanyama hawa na hifadhi hizi tukizilinda zitaendelea daima dumu vizazi vyetu vitakuta rasilimali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusipange vizuri hifadhi zetu hizi kila moja tukaipa *status* inayofaa kwa ajili ya maendeleo yake ya kiuhifadhi lakini pia kibiashara? Ukiacha *Seleou Game Reserve*, ziko *Game Reserve* zaidi ya 30, kwa nini hifadhi hizi 30 zisiundiwe shirika litakaloziangalia peke yake, Tanzania *World of Reserves?* Kwa kuunda shirika jipya itasaidia sana badala ya kuwa chini ya Idara ya Wanyamapori. Idara ya Wanyamapori iendelee kuwepo, iendelee kuishauri Serikali kwa masuala ya sera, kwa masuala ya sheria, kuangalia maeneo ya *WMA's*, kuangalia maeneo ya *game control areas* na kazi nyingine. Lakini liundwe shirika jipya litakaloziangalia hizi *Game Reserves* zilizobaki ambako ndiko kunafanyika uwindaji wa kitalii. Uwindaji wa kitalii unafanywa na matajiri wa dunia, ni biashara ya hakika. Hakuna mtu hivi hivi unaweza kufanya uwindaji wa kitalii, likiwepo shirika likajipanga vizuri, likaendeshwa kibiashara, tuna uwezo wa kupata mapato mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, nimuombe Mheshimiwa Waziri, alipandisha ada kidogo kwa ajili ya uwindaji wa kitalii baadhi ya watu wamepigapiga kelele. Ninawaomba muwe makini msirudi nyuma. Wale wawindaji wenyewe wanaokuja ni matajiri wa dunia, ni matajiri gani wa dunia waliolalamika kwamba ada za Tanzania ni kubwa, ni matajiri wa wapi hao? Ni hizi kampuni za katikati. Tukipata fedha nyingi zaidi, zitatusaidia katika kuhifadhi zaidi na zitatusaidia katika maendeleo ya Taifa kwa kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, tunaunga mkono muendelee kwa utaratibu huo na muendelee kuangalia maeneo mengine kwa kuyaongezea ada ili tuweze kupata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nirudie tena pale nilipoanza ambapo nia yangu ni kuunga mkono hoja ya kupandisha hadhi Pori la Mkomazi na Pori la Usangu na maeneo ya Ihefu ili kuwa chini ya *system* ya *National Parks* za hapa kwetu Tanzania. Kwa Hifadhi ya Mkomazi na Hifadhi ya Ruaha, tunaomba idadi ya watumishi iongezeke na tunaiomba Serikali iangalie mzigo wa kodi ambao *TANAPA* imekuwa ikiubeba kila mwaka kwa kuipunguzia kidogo ili iweze kumudu vizuri mzigo huu wa kuendesha hizi *parks* mpya. Huwezi kutegemea Mkomazi kesho asubuhi ikawa na watalii wengi, itachukua muda wa kuijenga na kuilea wa kama miaka 10 ili iweze kufika mahali pa kuanza kuzalisha vya kutosha. Kwa jinsi hiyo, *TANAPA* inahitaji muda, inahitaji fedha, inahitaji kuwezeshwa ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo napenda kuwapongeza sana wahifadhi wa *Game Reserves* zilizokuwepo tangu mwanzo, waliofanya kazi katika mazingira magumu sana ambapo wamezilinda na kuzihifadhi mpaka leo tumefika mahali pa kuzipandisha hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Maazimio haya mawili ya kupandisha pori la Mkomazi na Usangu kuwa *National Park*.

Mheshimiwa Spika, pia napenda niipongeze Kamati ya Maliasili, kwa jinsi ilivyopitia kwa makini Azimio hili na kuja na Maamuzi waliyoyatoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa mara ya kwanza kufika Mkomazi ilikuwa mwaka 1970 ambapo nimefanya kazi pale kwa muda na kwa kweli tumechelewa kuleta Azimio. Mkomazi *Game Reserve* ilianza mwaka 1951. Huwezi kutenganisha *Mkomazi Game Reserve* kiuhifadhi na *Tsavo National Park* inayotenganisha mpaka wa nchi hizi mbili. Upande wa Mkomazi hali ni nzuri zaidi kuliko hata Tsavo. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na ninaomba shughuli hizi zianze mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkomazi na *Tsavo National Park,* kwa sababu wenzetu Tsavo wana watalii wengi kuliko sisi, ninaomba milango ifunguliwe, iwe ni tofauti na ule upande mwingine ambapo haturuhusu. Kwa kuanzia tufungue milango ili tupate wageni na watuletee fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu ameshasema, Mkomazi kuna mnyama ambaye hapatikani maeneo mengi anaitwa *Lesser Kudu* (Tandala mdogo). Tandala huyu mdogo anapatikana Mkomazi na Pori la Yaeda pekee ambayo yako hapa nchini mwetu. Sasa Pori la Yaeda kwa sababu lilishavamiwa, Tandala wamebaki wachache sana. Nafikiri nalo lifikiriwe kupandishwa hadhi kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkomazi inapakana na maeneo mengi ya wenyeji na maeneo mengi yanayopakana na Mkomazi hakuna *buffer zone*, hakuna mapori yanayotenganisha wananchi na hifadhi. Ukienda kama maeneo ya Kisiwani, yanapakana moja kwa moja na Mkomazi. Ninaomba sana Shirika la *TANAPA* linalochukua pori hili liangalie jinsi ya kuwasaidia kwa karibu sana wananchi wa maeneo haya na kuwasaidia ni kuwatengenezea miundombinu wapate shule, maji, barabara na huduma nyingine ili waache kabisa kwenda kusumbua mapori haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna maeneo ambayo kuna wafugaji. Wafugaji walioko kwenye maeneo haya nao watengenezewe miundombinu ya maji na majosho ili kusiwe na ugomvi kati ya hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya uamuzi wa kufanya Mkomazi kuwa *National Park.* Tumeshaamua lakini kwanza wale watumishi wa Idara ya Wanyama pori waliopo Mkomazi wabadilishiwe ajira na waingie *Tanzania National Park* kwa sababu wao ndiyo wanayafahamu hayo maeneo, wamekaa huko miaka mingi tukisema wale tuwatoe na tulete watu wa *National Park,* kutatokea athari kubwa ambayo itaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba tumeamua kufanya *Mkomazi Game Reserve* iwe *National Park,* nashukuru lakini kuna mwenzetu aliyekuwa anakaa na faru kule ndani na wamezungushiwa lakini mimi napinga huyo mtaalamu kuendelea kukaa humo ndani. Tumeshaifanya *National Park,* tuwaachie wenzetu wa *National Park* waendeshe na kuwahifadhi wale faru kama wanavyofanya Ngorongoro, Serengeti na maeneo mengine. Tumshukuru kwa kazi nzuri aliyofanya lakini atupishe. Tunaweza tukatafuta eneo lingine la wazi tukamwambia akafanya kazi yake kule, mle ndani aondoke na ule uzio uliozungushiwa utolewe kwa sababu hatutakiwi kutengeneza vitu vipya ndani ya *National Park*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija upande Ruaha. Pori la Usanga limeanzishwa mwaka 1998 lakini lilikuwepo miaka mingi na kama walivyosema wenzangu ndiyo chanzo cha mto Ruaha unaotoa maji yanayohudumia wananchi wa Tanzania hii kwa umeme, maji yanayohudumia wananchi wanaokaa maeneo hayo, maji ambayo kwa kiasi kikubwa yanahudumia hifadhi ya Ruaha iliyopo sasa. Miaka ya 1970, Ruaha ilikuwa haikauki lakini nilikwenda miaka sita iliyopita nikakuta mto Ruaha umekauka. Hii ilitokea baada ya Usangu kuvamiwa na wenzetu wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuwahamisha hawa wafugaji. Hawa wenzetu wamehama na wamekubali hilo eneo liwe hifadhi, ni lazima tuangalie sana kule walikohamia, vijiji vinavyopakana na hili eneo la Usangu ambalo litakuwa *Ruaha National Park* mpya, wasaidiwe na wapewe miundombinu na wahesabiwe kwamba ni sehemu ya wahifadhi wa maeneo hayo na ikiwezekana hawa *Village Scouts* na wao wapewe nafasi ya kushirikiana na Hifadhi za Taifa katika ulinzi wa mbuga zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni ile kuwalipa kifuta machozi. Sasa hivi tunapata malalamiko mengi kwamba fedha wanazolipwa ni hela ndogo sana ukilinganisha na hasara watakazozipata. Ninaomba Serikali kwa hapo ijitahidi isijenge chuki na wananchi wa maeneo hayo. Wamekubali kuhama, tutapata faida sana na wao basi wapewe kiwango kinachotosheleza ili waanze maisha yao mapya kwenye maeneo ambayo tunawapeleka. Ikiwezekana yale maeneo yapimwe ili wawe na maeneo yao kabisa kama ni kijiji basi kiwe kimepimwa ili wasije kusumbuliwa mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya hizi hifadhi zetu yaani *Game Reserves*. Mwenzangu aliyetangulia ameshasema. Sisi tunashukuru tunapandisha kutoka *Game Reserves* zinakwenda kuwa *National Parks* lakini hizi *Game Reserves* hatuzitumii kama inavyotakiwa. Nirudie kusema kwamba tunaomba liundwe Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Idara ya Wanyama pori wabaki na sera na utafiti lakini kuwe na shirika la kuendesha hizi mbuga zetu, tunapata mapato. Likiundwa Shirika la kusimamia litasaidia zaidi na tutapata mapato mengi zaidi. Kwa hiyo, bado tunamuomba Waziri walete sheria tuanzishe shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, palepale bado tunaumia sana, huu ni mwaka wa tano tunaambiwa Sheria mpya ya Hifadhi ya Wanyamapori italetwa hapa Bungeni ili tuijadili

lakini mpaka leo hakuna. Wananchi wetu wengi wanaumia kwa ajili ya kutokuleta hiyo sheria na mambo mengi hayaendi mbele. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni kizuizi gani kinasababisha sheria hiyo isiletwe hapa Bungeni? Serikali imeanzisha maeneo ambayo yanawashirikisha wananchi kwenye uhifadhi lakini hayajapata baraka sasa hivi yanaendeshwa kienyeji. Naomba sheria hiyo iletwe ili tuhalalishe mambo na shughuli ziende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kupandisha Mkomazi, Usangu na Ruaha kuwa *National Parks* na nina imani ni kwa faida yetu. Nirudie kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake na Kamati iliyoandaa Azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba ajiandae.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu nami nichangie hoja iliyo mbele yetu ambayo ni Maazimio mawili yanayohusu kupanuka kwa Ruaha na Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wawili waliotangulia ambao ni wataalamu sana katika masuala haya, mawazo yao yamenivuta niunge mkono hoja hii. Nilikuwa nimekusudia kutoiunga mkono lakini kwa jinsi walivyozungumza kitaalamu kiasi ambacho hata mimi nasema mwishoni naweza nikaunga mkono hoja kwani wamezungumza vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba wakati zoezi hili linafanyika la kupanua maeneo haya, naomba sana Serikali ijitahidi na wahusika wote wajitahidi kama walivyosema wenzangu kuhakikisha kwamba haki za wote walio kwenye maeneo hayo zinaangaliwa, wanapewa haki zao, wanapewa fidia na wapewe elimu ya kutosha kwa nini wanahama usije ukatokea tena kama mgogoro ule uliotokea safari iliyopita wakati tunahamisha wafugaji, wengine wakapoteza mali zao wakachukuliwa mkuku na wanaowahamisha. Ni vema wapewe elimu ni kwa nini wanahamishwa kwa sababu inaonyesha Askari wanapokwenda kuwahamisha watu wanawahamisha kwa kutumia nguvu na kusababisha watu kupoteza mali zao. Hili ni wazo zuri na wote tunafahamu tukifika kwenye mbuga za wanyama tunafurahia na tunapata fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ninapenda kuzungumzia ni jinsi tunavyopanua maeneo. Tujaribu vilevile kuangalia maeneo mengine ambayo yana idadi kubwa ya watu lakini yamezungukwa na hifadhi ambazo zimeshatumika, inawezekana siyo hifadhi tena za misitu, watu wanaishi huko, imekuwa ni vurugu na watu wanatamani kuzitumia kwa sababu ya mbanano uliopo.

Naomba Serikali ijaribu kuangalia maeneo hayo ambayo sasa hivi watu wanaishi lakini kwa kuiba na baadaye inakuwa ni kero na ni vurugu hasa kwenye eneo kama la Geita ambapo sehemu nyingine kuna msitu watu wanaishi kule bado wanakuja wanahamishwa lakini ukweli ni kwamba watu wamebanana.

Naomba Serikali ijaribu kuangalia kuna maeneo ambayo watu wanaishi lakini wanaishi kwa wasiwasi lakini hawana jinsi kwa sababu ya mbanano wanakaa kule na baadaye wanaondolewa tena kwa nguvu na wanapoteza mali nyingi sana. Naiomba sana Wizara ijaribu kuangalia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, naomba sana Serikali ijaribu kuangalia ubinadamu katika kuhudumia wananchi wake na ijaribu kuwa na huruma. Namuomba Mheshimiwa Waziri akumbuke kwamba mwaka jana eneo la Matabe ambalo ni la wachimbaji, siyo la wachimbaji...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, kiutaratibu tuna *discuss* Hifadhi ya Mkomazi na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha sasa huko kwenye madini yako? Hatuwezi kuongea juu juu tu, tunaongelea *really*, tafadhali *concentrate* kwenye Maazimio hayo.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa mwongozo wako. Ninapenda kuunganisha hoja hiyo ambayo inafanana na upanuzi wa Mkomazi na Ruaha na maeneo mengine ambayo wananchi wameyaomba. Wao wanatuomba tuwape maeneo lakini kuna wananchi wameomba maeneo hawajapewa majibu, sasa ninataka kuwaunganishia na wao wakati wanaomba maeneo basi na wananchi walichoomba na wenyewe wafikiriwe. Ninaomba Mheshimiwa Waziri alitolee jibu suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani naruhusiwa kuendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rwilomba, endelea!

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, katika maelezo hayo, naomba Mheshimiwa Waziri akumbuke kwamba eneo hilo lilikuwa limeombwa na wananchi na *Barrick* ilipoliachia kwa ajili ya kuwapa wananchi, ikaonekana ni eneo la hifadhi. Sasa wananchi wakawa wameliomba, ni wachimbaji, ikaonekana utaratibu ufuatwe kwa sababu ni eneo la hifadhi na kwa sababu ya mbanano na watu walilihitaji, Waziri wa Nishati na Madini alikuandikia Mheshimiwa Waziri na barua sijui ilipotea mpaka leo hakuna majibu, wananchi wale wanahangaika na watu wengine wamekufa na baadaye wakahamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri, jaribu kuwafikiria wananchi wakati unaombwa eneo hili, wafikirie wananchi wale wamekaa muda mrefu wanahitaji kufanya kazi katika eneo lile. Nadhani wataalamu wako wameshakwenda kama si mara moja basi ni mara mbili na eneo lile sasa hivi sidhani

kama linastahili kuwa la hifadhi hata. Kama ni kwa ajili ya kutunza mazingira, nafikiri wachimbaji wakubwa wanaharibu mazingira zaidi kuliko wachimbaji wadogowadogo. Ukienda kwa mfano sehemu za Geita kwenye mgodi mkubwa mazingira waliyoyaharibu ni makubwa na ni ajabu sana kuliko hawa wachimbaji wadogo ambao wananyimwa eneo.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha ajaribu kuangalia katika hifadhi zake na hizi zilizoombwa basi awafikirie hawa watu. Nakubaliana nao kwamba eneo hili ni vizuri liende lakini kwa wachimbaji hawa na kwa wananchi hawa wanaohitaji eneo la kuishi ajaribu kuwafikiria sana. Nadhani watu hawa kama wangekuwa kama wako Mwanga angeshakimbia haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hukutusaidia kwenye Maazimio haya hata kidogo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba halafu atafuatia Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi kwa siku hii ya leo niweze kuchangia machache. Mimi pia ni Mjumbe wa Kamati hii, mengi tumeyaongea na ufafanuzi tuliupata kwa Mheshimiwa Waziri lakini ni kuongeza tu katika kujaziajazia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitoe salamu zangu za rambirambi, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Tabora, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia, kwa msiba mzito uliotusibu wa Mheshimiwa Salome Mbatia, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema peponi roho yake, amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM kwa ushindi wa kishindo alioupata na Watanzania wote ndani ya CCM wana imani kubwa na yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii. Kwa kweli ningemuomba aendelee kushika uzi ule ule pamoja na watalaamu wake na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo sidhani kama ina utata wowote kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesema kweli, tuingie kwenye suala zima la Azimio tulilokuwa nalo mbele yetu hivi sasa. Naomba nizungumzie suala zima la fidia. Wenzangu waliotangulia wameongea kwa kina sana kuhusu fidia kwa wakazi ambao

wataondolewa kwenye eneo hilo la hifadhi pande zote mbili yaani Mkomazi pamoja na Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumetokea mzozo mkubwa kwenye vyombo vya habari, walikuwa wanaonyeshwa wananchi wanalalamika kwamba wamepewa fidia kidogo na kuna baadhi ambao hawajapewa. Sasa ukiangalia taarifa ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna baadhi hawajapewa fidia na watalipwa polepole. Hawa ni watu aina gani? Kama ni watu wababaishaji, wadhihirishwe wazi kwenye kijiji kile kwamba ni watu ambao hawana makazi katika eneo hilo lakini kama wana makazi na ndiyo sehemu zao.

Ninamshauri Waziri kwenye eneo hili kwa kweli wenzangu wamezungumza sana kiasi ambacho Mwenyekiti amenifilisi. Kwa kweli ni kero kubwa kwa wananchi pale tu ambapo wanasumbuliwa kuondolewa na wao wamekubali. Wanapokubali kuondolewa kwa ridhaa yao na kwa makubaliano yao lakini kinachotokea tena fidia zinakuwa za kusema subiri subiri, ninaomba itangulie fidia kabla wananchi hao hawajaondolewa, kwa sababu kuchangia hapa maana yake ni kuuunga mkono asilima mia kwa mia kwa yale Maazimio ambayo yameazimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* ni Shirika ambalo halina wasiwasi. Sisi kama Wajumbe tumezunguka maeneo yote ambayo wanasimamia kama wahifadhi, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana kiasi ambacho Shirika hili, nina imani kama watapewa kazi hii kwa kweli Tanzania sasa tutaondokana na asilimia kubwa ya umaskini. Lakini *TANAPA* hiyo hiyo ingeweza kutusaidia pia kuhakikisha kwamba miundombinu inakuwepo karibu na vijiji wanayokwenda hao waliohamishwa. Ndio kuna vijiji lakini wao wamekwenda kule ni vema na wao wakaongeza nguvu kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wafuatilie kwa undani kabisa kuona kwamba je, hizi huduma wanazozitoa au wanazopeleka zinafuata utaratibu waliojipangia wenyewe? Kwa mfano, wanaweza wao wakatuma pesa kule lakini zile pesa zisifanye kazi iliyopangwa na kama isipofanya kazi iliyopangwa lawama itakuwa kwenye Serikali, malalamiko yatakuwa kwenye Serikali na siyo *TANAPA* tena. Kwa hiyo, ninaomba wanapopeleka pesa hizo wahakikishe kwamba zinawafikia walengwa ili kuondokana na malalamiko ambayo yanaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tu kidogo kwa ridhaa yako nichangie upande wa *Game Reserves* ambazo zipo kwenye Mkoa wa Tabora. Hivi karibuni kumetokea mzozo kidogo baina ya hawa wawindaji wa kitalii ambao wako kule kwenye vitalu vile. Walikwenda kwenye maeneo ambayo tuseme wamepewa wao kibali cha kwenda kuwinda kule lakini eneo hilo kuna wananchi ambao tayari walishaweka mizinga yao, kwa hiyo, kuna vitu viwili tofauti wao wameingia kama wawindaji lakini pia kuna watu ambao wameweka mizinga yao kule lakini taratibu zao na sheria ni kwamba haimruhusu mtu mwingine yoyote kuingia kwenye eneo hilo.

Kwa hiyo, ninashauri kwamba hao wanaoweka mizinga yao waruhusiwe kuweka mizinga kwenye eneo hilo la *Game Reserve* ili angalau wale wasiweze kuathirika na zao lao ambao wameshalizoea. Sasa hivi wanaogopa kwenda kule lakini nina imani Waziri alishalipata suala hili na alishalifanyia kazi na kama hajalifanyia kazi, nimuombe kwa kupitia Bunge lako Tukufu afuatilie tatizo hili ili ionekana kuna uwezekano gani wa wale watu kuruhusiwa kuingia kuweka mizinga yao ya asali hasa sehemu ambazo ni za bonde la *Central Wembeli* ambayo inapakana na Malongwe na Loya. Eneo hili lina asali nyingi sana na lina nyuki wengi ambao wako kule. Naomba Waziri atusaidie suala hili ili hawa watu tusiwaghasi kwa kazi ambayo wanaifanya kwani vyote tunavihitaji, tunahitaji asali na tunahitaji uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzie kuhusu suala la *Selou*s. Mimi wazo langu nilikuwa nimefikiria kwamba sheria ingekuja leo ya kupandisha gharama za Serikali kwa vitalu hivi ambavyo wamepewa wawindaji. Sisi tumekwenda *Selous* kama Kamati tukaanza kumuuliza yule mwekezaji ambaye yupo pale vipi utaratibu anaoutumia kwa kuingia watalii kwenye vitalu vyake lakini alichosema ni kwamba kila mtalii muwindaji anapofika pale analipa dola 750,000/= kwa kila kichwa. Sasa kama sisi tumepandisha kwa nini wananchi walalamike au wale watu walalamike kama alivyosema Mwenyekiti? Ni watu matajiri ambao wameweka vitalu vyao.

Kwa hiyo, nafikiria sheria hiyo ingefika hata leo ili angalau itumike na gharama ziweze kupanda na Taifa liweze kupata faida kwa sababu hawa walishapata faida siku nyingi. Sasa kama wao walipata faida siku nyingi sisi Serikali kuamua kuongeza imekuwa nongwa? Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri ukimaliza suala hili la Azimio haraka sana kwa Bunge la Januari utuletee tena sheria ya kupandisha gharama za uwindaji kwa vitalu hivyo ili tuende sambamba kuhakikisha kwamba kabla ya 2009 ambapo wanamaliza mkataba basi tuweze kufanya mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika *Selous* hiyo hiyo, tulipata malalamiko makubwa kwa wafanyakazi. Kuna upungufu mkubwa sana wa Askari wa Wanyamapori, hawatoshelezi na ndiyo ilikuwa lalamiko lao kubwa. Sasa tunaomba Wizara na bahati nzuri tulikuwa na Mkurugenzi alilipata hilo, iangalie ni jinsi gani ya kupeleka Askari wa Wanyamapori katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, waliotangulia ni wazoefu, wametufilisi lakini niseme tu kwamba pamoja na kupanua uhifadhi, sheria ambayo inatumika sasa hivi haitasaidia kwani faini zake ni ndogo hazikidhi. Jangili anapopelekwa Mahakamani, anaambiwa alipe Sh.50,000/= au Sh.100,000/=, haitoshi. Kwa hiyo, ninaomba sheria iangalie ni jinsi gani ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, pamoja na kwamba sasa hivi tumepata jedwali ambalo linaeleza maeneo ya kitalaamu lakini ninashauri Bunge lijalo tungepata hata ramani kama tulivyopewa ramani ya Kitulo ili mtu hata anapokuwa hapa ajue ukitoka upana huu unakwenda sehemu fulani au unafika kwenye kilomita ngapi ili kufika kule. Kwa hiyo, ninaomba kama kutakuwa na uwezekano tupate ramani ya eneo hilo la hifadhi ambalo ni Mkomazi pamoja na Ruaha ili ziweze kutusaidia sisi kufanya kazi yetu kwenye Kamati pia na Wabunge kuelewa nini ambacho kimechangia kuunganishwa kwa mapori hayo ili kazi iweze kufanyika vizuri na tuweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa ridhaa yako, nikushukuru sana. Kama nilivyosema mengi wamenifilisi wenzangu lakini ni wajibu wangu kwa sababu nilishaomba kuchangia basi angalau ayasikie na ya Tabora ambayo alikuwa hajayasikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Moja kubwa tu ulilolisema ni kama inawezekana ikapatikana ramani ya Tanzania, tukaiona nchi na hifadhi zake zote, nayo inapendeza.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, halafu Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele ajiandae.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu ya kuridhia hifadhi mpya ya Taifa ya Mkomazi pamoja na ya Ruaha.

Awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kutoa taarifa yake nzuri kuhusu maendeleo ya hifadhi katika nchi yetu na mikakati ambayo Wizara inachukua katika kuhakikisha kwamba nchini mwetu kunakuwa na hifadhi za kutosha na kutunza mazingira na rasilimali zetu katika hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Wizara kwa siku au kwa miezi michache ya nyuma, hatua ambazo imezichukua, kwa kweli ni madhubuti na ni za msingi.

Kwanza suala zima la kuzuia kukata magogo na kuyasafirisha kama yalivyo, hiyo ni hatua moja kubwa kwa sababu tutahifadhi misitu yetu mizuri na tutakuwa tunaivuna kwa utaratibu mzuri kwa manufaa ya nchi yetu na kwa ajili ya kuongeza rasilimali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili linahusu kuongeza ada katika hifadhi za uwindaji, pamoja na kelele nyingi zilizopigwa lakini hajafikia hata nusu. Namwomba

Mheshimiwa Waziri katika bajeti ijayo angalau basi ifike nusu ya *international standard* ya bei ya uwindaji wa Kimataifa. Kwa sababu kumpiga mnyama mmoja kwa kulipa bei kidogo na mnyama yule ni adimu, anapatikana katika nchi chache katika dunia hii Tanzania ikiwa ni mojawapo, ni lazima umnunue kwa gharama ambayo wewe unayewinda itakuwa ni kumbukumbu kwa maisha yako yote na vizazi vyako kwamba uliwahi kuwinda simba. Kwa hiyo, yeye inabaki katika historia lakini historia aliyoijenga na sisi Watanzania tufaidike nayo kwa upande wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yameongelewa mambo mengi ya hifadhi lakini nataka kujaribu ku-*share experience* na Mheshimiwa Waziri kwa maana na mimi Pangani nina Hifadhi ya Saadan na ni hifadhi mpya na toka imeanzishwa kuna mambo ambayo labda Wizara yake au hata mwenyewe amepata taarifa mbalimbali, kwa hiyo tujaribu ku-*share experience* kwa haya yanayojitokeza tofauti na yale yaliyoko Ngorongoro na Serengeti kwa sababu ya mazingira tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya Saadan inakwenda vizuri, nawapongeza *TANAPA* kwa jinsi wanavyoisimamia hifadhi hii. Sasa hivi kumekuwa na *infrastructure* za kutosha, barabara za kutembea ndani ya hifadhi ambapo sasa hivi ni kivutio kikubwa kwa watalii na watalii wameongezeka. Lakini tukumbuke kwamba Hifadhi ya Saadan ambayo itakuja kufanana na hizi hifadhi ambazo sasa hivi tunazipitisha, naomba nijaribu kutoa *experience* yangu kwa kipindi kifupi ambapo sisi wa Saadan tumeyaona. Yapo mazuri na yapo mengine ambayo ni kero kidogo kwa wananchi lakini ni rahisi kudhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Hifadhi ya Sadan inapakana na bahari na wanyama wanapendelea ikifika wakati fulani kufika katika fukwe na kulamba ile chumvi, kwao ni kitu ambacho wanakifurahia sana. Lakini sasa inabidi tufahamu kwamba hifadhi ile inapakana na vijiji moja kwa moja kama wenzangu walivyosema hakuna *buffer zone* kati ya Hifadhi ya Saadan na vijiji vile, ni *straight*, unatoka kwenye hifadhi unaingia katika kijiji. Kwa *experience* ya tembo wa Saadan sasa hivi wameanza kuonja kula nazi ambayo katika hifadhi nyingine yote katika Tanzania hakuna minazi. Huku kwetu sasa wameona kuna tunda tofauti ambalo wao hawajawahi kulionja, sasa hivi limekuwa ni zuri kwao. Wao wanaona ni mti wa kawaida, upo porini lakini umepandwa na binadamu na unamletea mapato. Ni kitu rahisi kulipata tunda lile kwa sababu mnazi ni mrefu, mnazi ule anauwekea kifua, unaanguka kirahisi kabisa kwa sababu hauna mizizi imara ya kumpa kazi kubwa ya kuweza kuung’oa mnazi ule, ukishaanguka anakula zile nazi ndogondogo, sisi tunaita makorokocho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ile nazi ndogo ikiingia inatoka kama ilivyokuwa, *digestion* yake ni ngumu sana lakini *at least* anapata *test* ya yale makumbi pale juu. Lakini kubwa zaidi ni yale makuti machanga ambayo yapo kwenye kilele cha mnazi pale ndipo anapopashughulikia vizuri zaidi kwa sababu kwanza ni laini, pana ladha tofauti

ambayo hajawahi kuionja, mnazi mmoja hauwezi kumtosheleza tembo mmoja anahakikisha anaangusha hata minazi ishirini au thelathini akapata chakula cha siku moja.  Sasa imekuwa ni kero kidogo kwa wakulima wetu wa minazi katika vile vijiji vinavyopakana na Pangani na vijiji vinavyopakana na hifadhi ya Saadan.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa utaratibu wa kulipa kifuta machozi lakini ninaiomba Serikali labda pia katika maeneo mengine yanaweza kujitokeza hayo. fidia au kifuta machozi kinachotolewa ni kidogo kwa maana ya Sh. 100,000/= kwa hekta.  Hekta moja mkulima anapanda minazi 120, minazi 120 kwa wastani mnazi mmoja kwa mwaka au kwa kila miezi mitatu anapata nazi 30, kwa maana ya nazi 120 kwa mwaka.  Kwa bei ya sasa katika hekta moja kwa mwaka anapata Sh. 4,000,000/=. Hicho ni kiwango cha chini kabisa ambapo mnazi unaweza kuzaa kwa maana ya nazi thelathini kwa kila miezi mitatu.  Sasa ukimlipa hekta moja Sh. 100,000/= wakati anapoanza kuupanda ule mnazi mpaka anaanza kuvuna zao la kwanza inamchukua miaka saba, ndio mnazi ulivyo, *East African Tall*, ni hela ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu kule Saadan mlipoanzisha hifadhi, tembo walianza kujaribu kula matunda ya nazi na wameleta uharibifu mkubwa, tunakadiria minazi kama 5000 imekwishaangushwa na tembo na wananchi wanatafuta njia mbadala ya kuona watapata vipi kipato chao kwa sababu tembo wapo karibu, wanashindwa kuwadhibiti.  Ninachoomba vilevile *TANAPA* waweke utaratibu maalum kwa sababu vijiji vile vinapita katikati, kuna barabara kati ya hifadhi na kijiji, kwa hiyo tatizo la *infrastructure* kwa maana ya barabara sio tatizo kubwa, wanaweza kufanya *patrol* za kutosha na kudhibiti hawa tembo wasiingie katika vijiji na wanachofuata kule ni nazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba orodha ya majina ya hao walioathirika ipo katika Wizara yake toka 2004. Niliuliza swali hapa lakini nafuatilia ili tusaidiane tuondoe hii kero ambayo inanikabili kama mwakilishi wao na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo Serikali yao wameichagua, basi wawe na imani na Serikali yao kwamba inawafikiria na kwamba inawasaidia kwa jambo kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa sasa wengi wao hawawezi tena kulima minazi katika maeneo ya hifadhi ambayo wapo jirani nayo kwa sababu ya tatizo la tembo.  Lakini mkiweza kuwadhibiti tembo wanaweza kupata matumaini, mazao mengine sasa hivi hawapandi kama migomba kwa sababu tembo wanachukua na kufanya chakula chao bila kujua kwamba hii ni mimea na wao hawajui nini maana ya mpaka kati ya kijiji na hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa tu Mheshimiwa Waziri *experience* hiyo pengine katika hifadhi hii ya Mkomazi na Usangu huko yanaweza kujitokeza mambo

kama haya. Ni vema na wataalam wakakaa kwa pamoja kuchukua tahadhari mapema kwamba ni kitu gani ambacho kinaweza kutokea kutokana na kuanzisha hifadhi ili muweze kuweka mikakati mizuri pindi yanapotokea matatizo mtakuwa mmekwishajua matatizo haya yatatatuliwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya *Selous*, hapa imezungumzwa na mimi nikubaliane na wenzangu waliotangulia, tuweke utaratibu mzuri. *TANAPA* tayari tumekwishawapa mzigo mzuri sana lakini yapo maeneo kama *Selous* tulivyozungumza, basi ianzishwe chombo kama vile Ngorongoro kuweza *specifically* kutazama maeneo kama ya *Selous* kwa vile ni makubwa basi kugawana madaraka katika kutekeleza majukumu ambayo ni yale yale lakini yenye utaratibu tofauti, hili litaweza kutusaidia sisi kupata mapato mengi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Tanzania peke yake kwa masuala ya utalii ingeweza kutekeleza bajeti ya nchi hii kwa mwaka. Wizara moja tu ya Maliasili na Utalii inaweza kutosheleza bajeti ya nchi hii, tunachohitaji sisi ni mikakati mizuri na uzalendo ambapo wafanyakazi au watumishi wetu katika idara hizi wataweza kufanya kazi kwa uzalendo na kuona uchungu wa nchi hii na kuhakikisha kwamba tunanufaika na rasilimali tulizokuwa nazo.

Sasa hivi tunaongeza hizi hifadhi mbili nyingine, ni *potential* nyingine kubwa kwa upande wa Ruaha na Mkomazi. Kama wengine walivyoshauri tufungue mpaka wa Mkomazi na Kenya, nakubaliana na wazo hilo ili tuwakaribishe na tujenge *infrastructure* ya barabara mpaka kwenye mpaka wa Tsavo na Kenya ili waone kwamba pale kuna geti na kuna *post* ya *immigration*, kuna Polisi na vitu vingine vya *custom* kuhakikisha kwamba wanaweza kuingia Mkomazi na wakaweza kutembelea katika yale maeneo na kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mheshimiwa Waziri tuna-*share common interest* ya Bonde la Mto Pangani ambalo linaingia katika maeneo haya ya hifadhi. Kuna eneo lile la Jipe, ni tatizo katika Jimbo lake, lakini wenzetu wa Kenya tatizo lile hawana kwa sababu tembo wamesaidia kula yale magugu maji ambayo yanaota katika lile ziwa. Kwa kutumia nafasi hii, naomba Wizara iharakishe kuona ni utaratibu gani wa kutatua tatizo la Ziwa Jipe kwa sababu lipo katika Bonde la Mto Pangani pamoja na hii Hifadhi ya Mkomazi inakuwa *included* katika bonde hilo hilo, linaweza kutusaidia kuona kwamba ni jinsi gani tutatatua tatizo la Ziwa Jipe kuondokana na yale magugu maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua analifahamu na Mheshimiwa Waziri ni mhusika mkuu, lakini nasi kama wadau katika bonde lile hatuna budi kumsaidia kwa sababu lile tatizo ni letu kama nchi na Ziwa Jipe likikauka ina maana ni moja ya ziwa limekauka katika nchi yetu. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara yako ukishirikiana na Wizara nyingi zinazohusika na mazingira kuona wananchi wale tunawasaidia vipi ili na wao waweze kujiendeleza katika uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam kwa kuleta Maazimio haya mawili na mimi nakubaliana nayo na nayaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hoja ya kuanzisha Hifadhi mpya ya Mkomazi na hoja ya kupanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, lakini mimi nitajikita zaidi kwenye hii ya Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta hizi hoja mbili kwa wakati muafaka. Nafarijika sana kwa sababu huko nyuma wanyamapori hawa utadhani wana akili, wana mzunguko, wanaanza kutoka Masaimara nchini Kenya, wanavuka mpaka wanaingia Serengeti na pale wanakaa kwa miezi kama minne hivi kwa ajili ya *immigration* na kuzalia huko Serengeti kwa sababu ni *plain* na wanaweza kuwaona wanyama wakali kwa mbali zaidi. Kwa hiyo, wanakaa miezi minne kati ya mwezi wa pili mpaka wa tano. Wanaondoka pale wanaingia Ngorongoro, wanaingia Manyara, *National Park*, wanaingia Tarangire, wanaingia Mkomazi hii ambayo sasa tunaizungumza wakati ikiwa *Game Reserve*, baada ya hapo wanavuka tena *boarder,* wanaingia Tsavo, wanaingia Amboseli *National Park back to* Masaimara. Kwa kweli ni mzunguko ambao unawapa uhuru wa kuzunguka wanavyotaka. Lakini sasa hivi kwa sababu ya kuongezeka kwa idadi ya watu katika maeneo na kuongezeka kwa ujenzi unaofanywa na binadamu na kuanzisha mashamba hata katika *corridor* za wanyama, wanyama hawapo huru tena kutengeneza huo mzunguko kama nilivyokuwa nimeeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi ni wadau muhimu sana katika kusimamia Hifadhi za Taifa na hata *Game Reserves.* Kwa hiyo, wanapoombwa wananchi wapishe ama *Game Reserve* au *National Park*, ni vizuri suala hili likafanyika vizuri kwa kuwashawishi wananchi, kuzungumza nao na kuwapa fidia inayostahili na kuwawekea miundombinu kule wanapotakiwa wapelekwe. Mfano mzuri, ni Watanzania wa jamii ya Kimasai walipokuwa wameondolewa na Wakoloni kutoka huko Moru, Serengeti ili kupisha *National Park* ya Serengeti miaka ya hamsini 1951 hadi 1959. Kabla ya kufanya hivyo, Wakoloni walifanya *negotiation* na uongozi wa jamii hiyo kwa miaka zaidi ya kumi na tatu na ndipo walipokuja kukubali kuondoka. Lakini pamoja na hayo waliwapa masharti kwamba kwa kuwa sisi ni wafugaji tunahitaji miundombinu, tunahitaji mabwawa kwa ajili ya mifugo yetu huko mnakotupeleka, tunahitaji *veterinary centres*, tunahitaji *drug* za mifugo yetu na mambo chungu nzima yanayohusiana na mifugo. Baada ya Wakoloni kukubali kufanya kazi hiyo, waliwaambia hatutahama mpaka twende kuona kwa macho yetu ni wapi mmeweka *infrastructures* hizo. Nafikiri ni jambo jema na ndiyo maana walipokwenda kujionea wenyewe wakahakikishiwa madawa ya mifugo yao, majosho, mabwawa ndipo wakakubali kuhama kutoka Serengeti sehemu za Moru wakahamia *Ngorongoro Highlands*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka katika miaka ya 80 na 90 Mkomazi *Game Reserve* ilikuwa na mgogoro sana. Watu wa jamii ya Kimasai na ndugu zetu wa Mkoa wa

Kilimanjaro kwa maana ya Wachaga na Wapare ndio waliokuwa wanaishi maeneo yale. Kulikuwa na migogoro mpaka ile Tume ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikaingilia kati lakini nafikiri mpaka sasa tunapofikiria kupandisha hadhi Mkomazi, hayo matatizo ya huko nyuma yameshakuwa *sorted out*, yamekwisha na nafikiri wananchi wamelipwa fidia zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Ngorongoro yenyewe ni eneo dogo sana, lina kilomita za mraba 8,300, lakini kule kwenye *crater*, ni kilomita za mraba 250 tu lakini ni maarufu sana duniani na hasa kwa sababu ya faru weusi waliopo katika Bonde la Ngorongoro. Lakini kutokana na matatizo ya ujangili wa Kisomali, hawa faru walikuwa wameuliwa mpaka wakabaki kama wanne tu. Kazi kubwa ya ulinzi wa faru hawa imefanyika na hadi sasa idadi ya faru hawa weusi imeongezeka wanafikia ishirini na tano. Huko Moru walikotolewa hao Watanzania wa jamii ya Kimasai nako kuna faru na wanaendelea kuhifadhiwa na wenyewe. Kama nitakumbuka vizuri wameongezeka, wapo kati ya nane na kumi. *Selous* vilevile tumeelezwa kwamba, ni *Game Reserve* moja kubwa katika Bara la Afrika hivi sasa na ina faru wengi pamoja na tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni nini? Ni kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sasa pengine ni ya tatu katika kuingizia Taifa hili mapato lakini ninavyoona huko tunakoelekea kama tutahifadhi vizuri *Game Reserve* zetu na *National Parks* hizi, nina hakika Wizara hii itashika nafasi ya pili na hata ya kwanza katika kuliingizia Taifa hili mapato. Ngorongoro peke yake, kama nilivyosema ni eneo dogo; lakini kwa bajeti iliyopita peke yake imeingiza shilingi za Kitanzania Sh. 38bn/=. Sasa tukipata *National Park* nyingine kama hii ya Mkomazi, Ruaha na zingine, nina hakika mapato kwa Taifa letu yatakuwa makubwa na kutuwezesha kutekeleza miradi mbalimbali ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa Mkuu wa Wilaya kule Karagwe mwaka 2001 mpaka 2003, mwishoni nilishughulika sana katika kupata *Game Reserve* inayoitwa Kimisi. Kama Mkuu wa Wilaya na kama mtu anayetoka kwenye maeneo ya wanyamapori, nilishawishi sana ingawa nilipata upinzani mkubwa sana kwa Waheshimiwa Madiwani wanasema nchi sasa ni ndogo, tunaongezeka, kwa hiyo tunataka tuongezeke kwenda huko lakini kilichonisukuma ni masuala ya usalama. Katika pori hilo la Kimisi na Burigi huwezi kupita kule ukitokea Karagwe kwenda Ngara bila kusindikizwa na magari ya Polisi, nikaona inaniletea tatizo la kiusalama, tukafanya hivyo. Nafurahi kwamba hiyo sasa imekuwa ni *Game Reserve* kamili na hii ambayo sasa tunaipandisha hadhi, *Inshallah* na yenyewe itafikia mahali ambapo wananchi watakubali, wakielezwa vizuri na mapato ya Taifa letu yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa na huo mchango mdogo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Azimio la Bunge la mwaka 2007 la Kuridhia Kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Mkomazi. Naomba nianze kwa kuunga mkono Azimio hili kwa maana ya kwamba litakwenda kulinda bioanuwai zetu katika mtandao wa hifadhi za Taifa na vilevile kuhifadhi *species* za wanyama zilizopo katika hatari ya kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule kwetu Namtumbo tuna eneo kubwa sana lililo katika hifadhi ya *Selous* ambayo tumepakana na Wilaya ya Ulanga, Tunduru na Liwale. Katika hifadhi ile, wananchi wa Wilaya ya Namtumbo walishirikishwa kwa muda mrefu kuhifadhi maeneo hayo ili kuhakikisha kwamba tunafaidika na maeneo ya maliasili yetu. Kwa kuwa uhifadhi tunafahamu kabisa ni moja ya mapato ya Taifa letu na kwa kushirikisha nguvu za jamii ya wananchi wetu wa Wilaya ya Namtumbo kwa kushirikiana na Shirika la Ujerumani, walianzisha ushirikishi jamii wa kuhifadhi maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka kumi na mbili baada ya kuelimishwa na kutunza maeneo hayo, wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakiomba kupata *Authorized Licence Association* kwa ajili ya kuwa na nguvu ya uhifadhi kamili wa maeneo hayo lakini mpaka leo bado hawajapatiwa leseni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa jamii umetuonyesha kabisa kwamba, una nguvu kubwa za kuweza kusaidia na kusukuma maendeleo ya maeneo husika. Kwa hiyo, kwa nafasi hii, naiomba Wizara iangalie jinsi gani ya kuweza kuharakisha kuwapa leseni hiyo wenzetu ili waweze kusaidia kuhifadhi mazingira ya eneo la *Selous*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria zinakinzana za sekta mbalimbali za Serikali yetu. Sisi kule katika Hifadhi hiyo ya *Selous* ambayo imehifadhiwa kwa muda mrefu sana lakini kwa muda wa mwaka huu tumeona sekta nyingine imeingia ndani ya hifadhi zilizohifadhiwa na ambazo nia na madhumuni ni kulinda bioanuwai na *species* mbalimbali. Lakini sekta hizo nyingine zimepata leseni ya kuja kuingia ndani ya sekta za utalii na kuanza kuchimba madini. Sasa wasiwasi wetu na *associations* zetu hizi za Namtumbo ni kwamba, tuta-*accommodate* vipi uhifadhi wa bioanuwai hiyo na uchimbaji wa madini hayo?

Kwa hiyo tulikuwa tunataka pia Wizara zikae na kushauriana na Wizara za sekta zingine za madini kuweza kutambua kama Serikali imeamua kuhifadhi eneo fulani kwa faida fulani kama ya utalii, basi isiingiliwe na sekta nyingine katika maeneo yake. Kwa maana ya kwamba hifadhi ya *Selous* ambayo sisi tulishirikishwa kuitunza na kulinda maeneo ya mapitio ya wanyama ambapo wanapita tembo wakubwa kwenda katika

hifadhi ya wanyama Niasa kwenda Msumbiji na kurudi, imeingiliwa na kuchimbwa madini ya *uranium*.

Sasa je, uchimbaji ule, tatizo langu hakutakuwa na *radioactive* ambayo itasababisha viumbe hai hivyo vinavyokunywa maji vikaathirika? Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali ikae na kuziangalia pia sheria hizi za Wizara nyingine ili tusiingiliane katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira ya maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sisi katika uhifadhi wa wanyama, kwa kushirikiana *GTZ*, tumekuwa na mradi wa kufuga nyuki. Wananchi wameelimishwa kwa muda mrefu tu na sasa wapo tayari kwa ajili ya mradi huo, lakini bado mradi huo haujatekelezeka na wakati wapo mwishoni ndiyo linatokea jambo lingine la maingiliano ya uhifadhi.

Vilevile kuna wananchi ambao wameishi kwa muda mrefu katika hifadhi bila utambuzi wao na Serikali ikawatambua na ikajenga shule na sasa Serikali za Wilaya mbili zinawahitaji wale watoke na kuna shule ambayo ilishajengwa na nyumba zao na kadhalika. Kwa hiyo, tunaomba pia kama wataondolewa basi Wizara ihakikishe inawasaidia kuwalipa fidia zao na kuwapatia maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu na mchango wangu ulikuwa ni huo, ahsante sana. *(Makofi***)**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Ninapenda kutumia nafasi hii, kwanza kabisa, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kumpa pole kwa kazi ngumu anayofanya ya kuboresha shughuli za Wizara hii. Wizara hii ni ngumu, ina matatizo mengi lakini nadhani Wizara imeshikwa na mtu anayejua wajibu wake na mtu aliyesomea shughuli za Wizara hii, nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kuwaondoa wasiwasi wapiga kura wangu kwa sababu leo toka asubuhi nimekuwa napata simu za pole kwa mikasa iliyonipata kwamba nilipata na ajali na sasa niko hospitali mahututi tokea tarehe 1 Novemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sijawahi kuwa na afya nzuri katika maisha yangu kuliko nilivyo sasa kufuatana na ripoti ya Madaktari. Kwa hiyo, nataka kuwaondoa wasiwasi kwamba kama kuna maneno kama hayo basi ni ya watu walio na nia mbaya na sisi wengine. Mimi ni mzima na nimehudhuria Mkutano Mkuu wa Chama, nimechagua viongozi na nimekuwa hapa, wewe ndiye shahidi tangu mwanzo na wakati wote nimekuwa nahudhuria vikao vyote kama mwakilishi wa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, Hayati Julius Kambarage Nyerere aliona mbali akaamua eneo kubwa la nchi hii liwe na *National Parks* vinginevyo uamuzi huu ambao tunaufanya leo ingekuwa vigumu. Nadhani nchi yetu ni miongoni mwa nchi chache katika dunia ambazo zimetenga eneo kubwa la nchi kwa ajili ya

kuhifadhi wanyama na mimea. Hatua hii anayoifanya Mheshimiwa Waziri leo inakwenda kwenye mstari huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana vilevile nimpongeze kwa kuona mbali kwa sababu katika uchambuzi wa kisayansi wanasema hivi: "binadamu wanazidi kuongezeka na ardhi haiongezeki." Kwa hiyo, kadri tunavyozidi kuongezeka binadamu na wanyama itabidi tuamue eka moja hii tuliyonayo tufugie ng'ombe au tulime nafaka. Kisayansi ukilima nafaka utalisha watu wengi zaidi kuliko ukifuga ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa kisayansi, binadamu *is an essentially vegetarian* la sivyo lazima atafute njia nyepesi ya kupata nyama kwa kufuga wanyama katika eneo ndogo kama vile kufuga kuku, nguruwe, samahani kwa wengine na wanyama wa kufugwa wa *zero grazing*. Lakini huwezi ukatembeza ng'ombe nchi nzima kama tunavyofanya Watanzania na tukadhani ndiyo jibu la matatizo. Sijui kama ni sera yetu hii ya kutembeza ng'ombe nchi nzima ili kutatua tatizo la uhaba wa nyama? Watu wa Kusini wanataka nyama ndiyo lakini sidhani kama wanahitaji kwato za ng'ombe watakaoharibu nchi hii na kuigeuza iwe jangwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatua hii anayoifanya mwenzetu hapa ni ya busara sana kwa kuwa kwa kutunza msitu huo au kuufyeka kabisa na kupanda *malezi* tutapata fedha nyingi sana kuliko tungetumia utalii na kupata fedha ambazo tungenunua *malezi* kutoka mahali pengine, inaitwa *opportunity cost* unaamua lipi lenye faida kwa maisha ya sasa na ya baadaye kuliko vinginevyo. Tukiamua kuwe na *mark value* katika maisha yetu kwamba *the end just the means*, hujali unatumia njia gani mradi unatapata unachokitaka, nadhani tutakuwa tunaisaliti nchi yetu na tutakuwa tunakana wajibu wetu. Ni aina gani ya nchi tutaikabidhi kizazi kijacho?

Mheshimiwa Naibu Spika, napata kigugumizi kidogo kwa sababu moja. Uamuzi huu wa kuunda *National Parks* hauunganishwi na misitu midogo midogo kama ile ya Itoni, Mapara, Iditima na mahali pengine, hii wanataka waiachie vijiji. Wananchi wa kawaida hawaelewi bado thamani ya miti. Nadhani bado kuna haja ya kuoanisha hizi *National Parks* na hiyo misitu midogo midogo vinginevyo tutakuwa tunafanya kazi nzuri kule juu wakati huko chini wanazidi kuiangamiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima mawazo yao bado misitu ni adui, wengine tunazungumzia ku-*reserve* sehemu za mito, lakini bado kuna watu wetu hawaoni umuhimu huo na mito inazidi kukauka, tunazidi kukemea tu na kukemea hivi ni nani anazuia? Naishawishi Serikali itazame uwezekano wa kuoanisha misitu midogo midogo, *forest reserve, game reserve* na hizo *National Parks* ili fedha za *SIDA* ambazo ni nyingi zisaidie ku-*finance* na ku-*support* ili kusudi tuwe na kitu ambacho ni kamili. Kwa watu wa kawaida, misitu hii ya chini ni ya maana zaidi kuliko hii ya sasa, ingawa ni muhimu kwa sisi ambao tunaona mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Wizara kwa wazo hili kwa sababu ni mara ya kwanza sasa inaanza kuona hata umuhimu wa kutunza mimea nyasi. Kitulo wanasema ina maua ambayo hayapatikani mahali pengi katika dunia hii. Ukienda mwezi Oktoba na Novemba unaona uzuri wa mbuga ya Kitulo. Nadhani hilo ni eneo la juu kuliko mahali pengine popote katika Tanzania ambalo lakini ni *flat*. Wakati tuna Serengeti *National Park* kwa ajili ya wanyama, lakini tuna Kitulo *National Park* kwa ajili ya maua na mimea ya aina mbalimbali. Sasa mtindo huu nao wa kuangalia maeneo mengine mazuri yenye mbuga nzuri na mimea ya aina mbalimbali tungeuendeleza ili kusudi nayo tukai-*preserve.*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nisaidie tu, kule Njombe kuna mbuga zile Rugusi lakini zinatoweka kwa sababu tunapanda miti na tunalima, kizazi kijacho kitadhani Njombe ilikuwa ni nchi ya miti tu. Hata zile nyasi hawataziona, zile *grass lands* na *grass roots,* hawataziona kwa sababu eneo lote limelimwa. Kwa hiyo, kuwe na *delibarate strategy* ya Wizara ku-*preserve* maeneo fulani fulani kwa ajili ya kizazi kijacho kiweze kuona mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, nchi yetu imejigawa yenyewe duniani, maeneo kama ya Dakawa, Kilombero, Rukwa, Usangu hayo ni maeneo kwa ajili ya kilimo. Maeneo kama Dodoma hapa ni maeneo ya kufuga ng'ombe. Hata katika nchi kama Marekani, California kote kule *semi-dry* ndiko wanakofuga ng'ombe. Sasa sisi tunapeleka ng'ombe Kilombero, tunasema ni mchanganyiko, watu wanagombana kule. Ghala la Taifa kama Kilombero unapeleka ng'ombe, kwato zinaharibu ardhi na kuua mito na baadaye ni kujuta ulikuwa na Hazina kama ile, nadhani ni *short sightless*. *We must have the courage to speak the truth however bitter*. Kilombero ni eneo nzuri la kutunzwa kwa ajili ya kizazi chetu kijacho na ni ghala letu lile tukipeleka ng'ombe, wakaua, hatutapata Kilombero nyingine tena. Sasa hao wenzetu wanaotembeza ng'ombe hawaelewi ni sisi tulio na *vision* ya kuona mbali tusaidie kuokoa nchi hii kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninapenda kuishauri Wizara vilevile iangalie licha ya ku-*preserve* maeneo hayo, inasemekana miti hii ya kigeni kama Mikaratusi, *breakwater,* inaua vyanzo vya maji na inaua mimea yote inayopatikana katika eneo ilipopandwa. Kwa mfano, ukipanda mpina, Kiswahili nadhani ni misindano, ukipanda misindano, yale majani yanapodondoka yanaua mimea mingine yote iliyopo chini yake, inakuwa ni kama kansa na pale chini hapataota mmea wowote. Katika kufanya utafiti na kudumisha *biodiversity* kwa kupanda mimea ya misindano ambayo sisi watu wa Njombe tunaipenda kwa sababu ni zao la uchumi lakini vilevile ile ina madhara yake kwa kusababisha miti mingine yote kutoweka. Tungekuwa na *deliberate* sera ambayo ingetusaidia kushauri ni miti gani ipandwe wapi au ni miti ya aina gani ipandwe wapi kusudi tutunze *biodiversity* kwa sababu hatujui ni miti gani tunaweza kupata dawa ya kuponya UKIMWI. *Eighty five percent* ya madawa yote yanayotumiwa na binadamu yanatokana na mimea na *fifteen percent* ndio inatokana na *rocks.* Kwa hiyo, ni lazima tuwe na mikakati ya kutunza vitu hivyo. Wenzetu walio na *knowledge* hiyo

Mheshimiwa  Prof. Jumanne Maghembe,  Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya pale, mtumie *knowledge* yenu, msibaki mnaning'iniza *knowledge* zenu kama matunda kwenye mti.

Mheshimiwa Naibu Spika,  ahsante sana.  *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya nakupa nafasi, Mheshimiwa Gosbert Blandes, nimewomba radhi atazungumza baadaye.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama  hapa kuunga mkono Maazimio haya muhimu sana kwa uhai wa Taifa letu na si kwa sasa tu hata kizazi na vizazi vinavyokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu maazimio yote mawili ni sababu za msingi sana.  Lakini vilevile michango mikubwa na mizuri ya Waheshimiwa Wabunge ambayo Mheshimiwa Waziri  wa Maliasili na Utalii atapata nafasi ya kuifafanua na kuitolea maelezo na majibu imesaidia sana kutupa mwanga kuhusu umuhimu  wa Maazimio  haya makubwa mawili ya leo na ni Maazimio ya msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengi ambayo inabidi tuyafanyie kazi. Naamini katika Wizara ya Maliasili na Utalii wenzetu wanaendelea kuyafanyia kazi na moja tu ambalo linaelekea huko ni lile la kuunganisha ikolojia moja lakini ipo katika maeneo mawili ya kiutawala ambayo ni ya Hifadhi ya Kitulo ambayo inaunganisha Milima ya *Livingstone* na Hifadhi ya Misitu ya Mlima Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika taratibu za Kiserikali, Mlima Rungwe unaangaliwa kama vile ni Mlima wa Hifadhi ya Misitu lakini kiikolojia ni Mlima muhimu sana kwa sababu ya vyanzo vya maji, bioanuai na rasilimali kubwa na vilevile litakuwa chimbuko kubwa la utalii katika eneo la Nyanda za Juu Kusini na linatenganishwa na *corridor* ndogo inayoitwa Bunjigijila *corridor* ambayo sasa mchakato umeanza kuwashirikisha wananchi katika Kata mbalimbali zinazozunguka Mlima Rungwe ili hatimaye kuunganisha Hifadhi ya Kitulo na Hifadhi ya Mlima Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani suala hili Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kulifafanua zaidi jinsi Wizara ya Maliasili na Utalii itakavyosaidia kusukuma mchakato huo ili kulinda rasilimali za nchi siyo  kwa kizazi cha sasa lakini hata kwa kizazi kinachokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa  muda huu mfupi tu kuunga mkono Maazimio haya mawili lakini vilevile kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kumpongeza Mheshimiwa Waziri  kwa kazi kubwa anayofanya yeye  na wenzake katika Wizara  hii ya Maliasili na Utalii.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii yeye binafsi pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo pamoja na watumishi wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri sana wanayoifanya na kwa kweli wanaofuatilia utendaji wa Wizara hiyo wanaona kazi nzuri ambayo inafanyika. Nachukua nafasi hii kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kuleta Maazimio haya mawili. Nilipokuwa nayaipitia, kwa kweli yamenifurahisha na hasa kwa kuona kwamba yataweza kuinua kipato cha Taifa letu kwa kupitia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni zuri lakini nadhani inabidi Serikali ijipange vizuri katika utekelezaji wake katika hifadhi hizo mara utakapoanza. Ninasema hivyo kwa sababu tunapotangaza Hifadhi ni kwamba tunakuwa na mkakati wa kuhamisha wananchi wanakuwepo katika maeneo hayo pamoja na mali zao kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba wanyamapori huwa hawajui mipaka kati ya mwananchi na Hifadhi, wao wamezoea kuzunguka, wanakuwa huru na sheria inasema usimuue mnyamapori anapozunguka hata akiingia kwenye shamba lako, sasa tunapotangaza hifadhi hizo tunajua kuna matatizo yatakayojitokeza ya wananchi kushambuliwa na wanyamapori na mali zao kuweza kuharibiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Mkomazi sijui jiografia yake, nitapenda kuizungumzia kwa kutumia mfano tu wa Hifadhi mbili za Kimisi pamoja na Burigi ambazo zipo Wilayani Karagwe kwenye Jimbo langu. Hifadhi hizo kabla hazijatangazwa kuwa hifadhi, wananchi wangu walikuwa wanapata vibali vya kuwinda kitoweo, wanyama wakija wanawafukuza, lakini baada ya kuwa hifadhi pamoja na kufurahia hifadhi lakini hifadhi hii sasa imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Karagwe na hasa hapa nazungumzia Hifadhi ya Kimisi pamoja na Hifadhi ya Burigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Kimisi inapakana pamoja na kijiji cha Nyakakika, kijiji cha Chabuhora, kijiji cha Kayungu, Kijiji cha Nyakasimbi, kijiji cha Nyaishozi, kijiji cha Ihembe, kijiji cha Kahanga, kijiji cha Ruhita, kijiji cha Kibogoizi na kijiji cha Rugu. Kwa upande wa Hifadhi ya Burigi inapakana pamoja na kijiji cha Kibwela pamoja na kijiji cha Mlamba kwenye Kata ya Kihanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu hifadhi hizi zitangazwe, wananchi wa vijiji hivyo wamekuwa wanashindwa hata kupata usingizi, hawalali kwa sababu tembo wamezaliana kupitia kiasi na wanazagaa kama mbuzi. Hata jana wananchi wangu wamenipigia simu kwamba sasa tembo huko wanawamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli mimi sipingi Sera ya Serikali lakini inapokuwa kero kwa wananchi inatupa shida sana. Nadhani Wizara inahitaji kujipanga katika hili kwa sababu baada ya Hifadhi ya Kimisi kutangazwa, Makao Makuu ya Hifadhi hii yamewekwa katika Wilaya ya Ngara lakini Hifadhi hii sehemu kubwa zaidi ya robo tatu, ipo katika Wilaya ya Karagwe. Mara nyingi wanyama hao wanaposhambulia wananchi ni Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ambayo huhangaika kwenda kuwafukuza na kwa bahati mbaya wanakuwa hawana hata silaha za kutosha, hawana hata risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza pale Wilayani Karagwe hakuna hata mtumishi wa wanyamapori. Mtumishi aliyekuwepo alikuwa anaitwa Bwana Rubunga alikuwa peke yake pale na sijui ni kwa nini na juzi amehamishwa nadhani amepelekwa Ngorongoro. Kwa hiyo, pale wamebaki watu ambao hawana ujuzi kabisa na hayo masuala ya wanyamapori. Juzi nilipokuwa kwenye ziara zangu, waliniita kwamba tembo ameshambulia mashamba ya watu, basi ikabidi na mimi nijikakamue nikachukua mkuki na kuanza kufukuzana na tembo lakini sikuweza kusaidia chochote. Sasa nataka kusema kwamba pamoja na nia njema ya Serikali, ni vizuri Serikali ikapanga kulinda wananchi na mali zao dhidi ya hao wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na timu yake kwa ujumla waliangalie suala la wanyama waharibifu hasa tembo katika Jimbo la Karagwe na liwekewe mkakati wa haraka sana wa kuweza kulimaliza. Kama inawezekana basi waje watusaidie wavune wale tembo na vilevile wajenge ofisi katika eneo la hifadhi na pia wapeleke watumishi wa kutosha kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niiombe Wizara kwamba pale inapofikia kugawa vitalu vya uwindaji, nadhani itakuwa vizuri sana wananchi wanaopakana na maeneo hayo kama watakuwa wamepeleka maombi yao kwenye Wizara, basi wapewe kipaumbele. Kwa mfano, kule kwangu Karagwe kuna vitalu vya uwindaji kwenye mapori ya Kimisi na Burigi. Wananchi wangu wamekuwa wakisumbuka sana wananiambia Mheshimiwa Mbunge na sisi tunataka tupate hivyo vitalu. Nikawambia pelekeni maombi Wizarani, nadhani yatakuwa yameishafika. Basi nataka nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba wale wananchi wanaozunguka maeneo hayo kama wana vigezo vya kutosha basi na wenyewe wafikiriwe kabla ya watu wengine wa kutoka maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri atakuwa anafahamu, lakini nataka kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kule Karagwe tunayo chemichemi ambayo inatoa maji moto hata ukienda pale unatengeneza chai ya moto hapo hapo, yanachemka yenyewe. Sasa nilikuwa najaribu kujiuliza kama Wizara inayo taarifa hiyo na kama haina taarifa hiyo, ningependa sana walitembelee eneo hilo

linaloitwa Mtagata lipo katika Jimbo jirani la Kyerwa kwenye Wilaya ya Karagwe. Ni eneo zuri sana kwa ajili ya watalii na vile vile yale maji yanatumika kama dawa kutibu wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nikumbushie ombi langu kwa Waziri hasa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, nilimwomba sana aje Jimboni kwangu Karagwe na tulikubaliana kwamba angeweza kuja mwaka huu. Sasa ninamkumbusha tena naomba aje atembelee aone mashamba ya wananchi yalivyoharibiwa na tembo wametuzidi uwezo, wanaharibu migomba na kibaya zaidi sasa hivi wameanza kunywa pombe ya Rubisi ya wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU PIKA:** Mheshimiwa Fuya Kimbita unafikiri dakika 10 zinakutosha au nikuache utaanza kuchangia jioni, *Okay,* Mheshimiwa Fuya Kimbita.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nisema dakika hizo kumi zitatosha kwa sababu wenzangu wengi wamekwishazungumzia kwa ujumla. Kwa hiyo, niende moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya pale Wizarani akishirikiana na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wa Wizara hii. Lakini pia nitumie nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Waziri kwa kufiwa na dada yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Prof. Jumanne Maghembe kwa kuthubutu kwake kwa yale yote yanayofanyika pale Wizarani ambayo nadhani yatatuingizia kipato kikubwa sana kiuchumi kwa Taifa letu na ni mambo makubwa na mazuri, yahitaji kuthubutu. Wapo wachache waliokuwa wanafaidika, watalalamika lakini tunamuunga mkono asonge mbele. Tutamuunga mkono sana wala asihofu tupo pamoja naye kwa maslahi ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maazimio yote mawili ni mazuri kabisa kwa sababu ya umuhimu wake kwa uchumi wa Taifa letu hili la Tanzania. Mwenzangu, Mheshimiwa Job Ndugai, amekwishalizungumzia, ni mwenyeji kule kwenye hifadhi mbili na wengine wameshataja maeneo muhimu na Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya naye amegusia maeneo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba katika Wizara hii nizungumzie suala hili la Mlima wetu wa Kilimanjaro ambapo pia tulihitaji kuuhifadhi vizuri zaidi. Katika Mlima Kilimanjaro kuna miti imeoteshwa mipakani ili kutenga yale maeneo ya wananchi na

hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Kati ya miti ile iliyooteshwa kuna Mikaratusi. Kwa maoni yangu na kwa kuulizana na wataalam ni kwamba ile miti ni hatari sana, inanyonya maji mengi sana. Taarifa zilizopo za kisayansi ni kwamba mti ule mmoja kwa siku unakunywa karibu galoni 40 za maji. Ili tuweze kuendelea kuhifadhi maji na kutunza mazingira, ningeomba Wizara iangalie jinsi gani tutaweza kuibadilisha ile miti kwa maana ya kuiondoa na kupanda miti mengine ambayo ni *more friendly to the environment*.

Katika kuchangia kipato cha uchumi kwa nchi yetu, Mlima Kilimanjaro unatusaidia sana. Sina takwimu za uhakika sana lakini nadhani kwa mwaka jana Mlima Kilimanjaro katika shughuli za kiutalii uliingiza zaidi ya bilioni 23 au 24, hiki ni kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakuja katika mambo ya kuhifadhi nikimaanisha kwamba mahusiano kwa wale wananchi wanaozunguka Mlima wa Kilimanjaro yasipofanyika, mambo muhimu yenye kuonyesha dhahiri kwamba kwa kuutunza ule Mlima Kilimanjaro nao wanafaidika kwa njia moja au nyingine, watakata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomaanisha ni kwamba nimetoa pendekezo hili na nilishazungumza na Mheshimiwa Waziri siku za nyuma, nilizungumza pia na mtu wa *KINAPA* ambao nadhani wapo na *TANAPA*, kuwepo na utaratibu wa kugawa asilimia fulani kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwenye Halmashauri hizo zinazozunguka Mlima Kilimanjaro ili wananchi waweze kutambua rasmi kwa mfano, ni darasa limejengwa, ni hospitali imejengwa, ni barabara imekarabatiwa kwa fedha zinatokana na kuhifadhi Mlima wetu wa Kilimanjaro. Kinachofanyika sasa hivi ni maombi tu yanakwenda na lile ombi ni sawasawa na hisani tu, kwamba wakikaa wakafikiria, wakiamua kweli watakupa hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho nilizungumza na mtu wa *TANAPA* aliniambia kwamba ndiyo Mlima Kilimanjaro unaingiza mapato mengi lakini fedha ile ile ndiyo inayotumika kwenda kuanzisha kwa mfano hifadhi mpya hizi tunazozizungumzia sasa hivi. Nikamwambia sikatai, ni sehemu ya Tanzania, lakini pia kuna sababu ya hao wananchi wakaweza kufaidika kutokana na Mlima Kilimanjaro. Kwa sababu wenzetu wamejaliwa kuwa na dhahabu zao zipo ardhini, wanapata gawio la *dollar* 200,000 kutokana na machimbo ya dhahabu kila Halmashauri, wenzetu wengine waliopo karibu na maeneo ya kuwinda nao wanapata asilimia 25 sasa na sisi tunaozunguka Mlima Kilimanjaro, dhahabu yetu Mungu aliyotupa ni ule Mlima Kilimanjaro, dhahabu yetu sisi hatuijichimbi ardhini, ukichungulia hivi tu tayari umeishalipa, watu wanaotoka katika sehemu mbalimbali wanakuja kuuona Mlima Kilimanjaro ndiyo dhahabu yetu ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba uwepo utaratibu rasmi kwa maana ya zile Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro tuweze kupata gawio rasmi badala ya utaratibu uliopo sasa wa mambo ya

hisani. Asilimia kadhaa itengwe kwa mfano katika kupata hizo bilioni zote nilizozitaja hapo juu, wakitenga hapo hata asilimia 10 tu kwa maana ya kuzigawia zile Halmashauri zitaenda kufanyika kazi maalum ambayo wananchi wataweza kuitambua na kuithamini na ule moyo wa kuendelea kutunza Mlima Kilimanjaro utaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa moto ukitokea katika Mlima Kilimanjaro ni wananchi hao hao watakaoshirikiana katika kuuzima moto ule. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri suala hili alipe kipaumbele na ikiwezekana hata kwenye bajeti ya mwaka ujao nimwombe awatangazie wale wananchi wa Kilimanjaro kwamba watakuwa wanapata asilimia kiasi gani kutokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro. Hilo ni ombi kabisa na nitaendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri ili kwamba mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza uchumi kwa ajili ya nchi na wale wananchi wa Kilimanjaro bado kuna vivutio ambavyo tukivitumia vizuri tutaongeza mapato makubwa yanayotokana na Mlima Kilimanjaro. Kwa mfano, kwa kufungua njia mpya nyingine ya kupandia Mlima Kilimanjaro ambapo hiyo njia ina vitu vya kipekee zaidi ambavyo *route* zingine hazina. Naizungumzia *route* ya kutoka Kwasadala hadi sehemu ya *Shira One.* Kwasadala Masama, unapita huko kwenda Mula, Nule, Getini kuna sehemu inaitwa Walamungelini, kote huko hiyo ni *route* mpya ambapo watalii wataweza kuitumia siyo ngumu kuipanda inaenda kugusa eneo linaloitwa *Shira One* kwenda *Shira Two* ambako ni kileleni na ni katika kuunganisha ile *route* ya kuuzunguka Mlima Kilimanjaro kuja kupitia kwenye Jimbo la Siha kwenda kuunganisha *Machame route* na *Marangu route.*

Mheshimiwa Naibu Spika, njia hii mpya ninayoizungumzia kuna vitu vingi kule, nimetembelea huko mwenyewe, nimeshaenda huko nimeona, kuna vitu vingi vya kuvutia watalii kwa mfano, kuna sehemu soko lilikuwa linafanyika mlimani kabisa. Soko hili lilikuwa linafanyika kwa ajili ya watu wa sehemu za Masama, Machame, Rombo pamoja na Siha. Lakini pia kuna vitu vingine vya maajabu ya Mungu. Kuna jani ukiligusa mle mvua inanyesha saa hiyo hiyo, kubwa kabisa. Kuna miti mingi ambayo wananchi wanapata dawa, magome ya miti, kuna dawa ya kansa ambayo inasumbua sana wenzetu, lakini hizo dawa zipo kule mlimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hii *route* nimwombe aifungue kwa sababu itatusaidia kiuchumi kwa Taifa letu, itusaidia kiuchumi kwa ajili ya wale wananchi wangu wa Hai. Nilishazungumza kidogo na Mheshimiwa Waziri sasa na lile andiko langu tayari nitaliwasilisha kwake rasmi ili tuweze kushauriana na wataalam wake kwa ajili ya kufungua *route* hiyo mpya ya kutoka Kwasadala hadi *Shira One* kwenda kuunganisha na *Shira Two*. Muda naona unazidi kunitupa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba bei ya mazao ya misitu aliongeza viwango kwa ajili ya mbao za kuuza nchi za nje sawa kabisa lakini kwa mbao za hapa ndani, naomba waangalie hali ni ngumu. Wananchi wanalalamika sana kwamba bei za mbao zimepanda sana. Kwa hiyo, ujenzi unakuwa ni mgumu na kwa upande wa *furniture* hali ni ngumu sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Waziri, naomba kama umekwisha-*revise* lakini labda hujatangaza, niombe bei za mbao kwenda nje zibakie kuwa juu, ni vizuri, sawasawa, lakini bei za mbao za hapa nchini wapunguze kwa ajili ya manufaa ya kuliendeleza Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umekwisha, ninakushukuru. Mchango wangu ulikuwa ndio huo. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba tupo pamoja naye katika vile vita anavyopigana pale Maliasili, tutaendelea kuwa naye na wala asihofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo isipokuwa *party caucus* ya Chama cha Mapinduzi watakutana saa saba na nusu katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Baada ya kusema hilo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tulipoahirisha Bunge nilikuwa na orodha ya wachangiaji wawili na baada ya hapo nitamwita mtoa hoja ili tuendelee na shughuli nyingine.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Azimio la Bunge la Kuridhia kupanuliwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Nasema hili kwa sababu ndipo nitakapozungumzia kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema kwa sababu ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili kusimama, ninaomba nitoe salamu za rambirambi kwa ndugu wa marehemu Salome Mbatia, ndugu yetu tuliyekuwa naye karibu sana, Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin!*

Lakini nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupata kura nyingi sana katika uchaguzi uliopita katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Sitasita kumpongeza sana kwa kuweza kutenga nafasi muhimu za maamuzi katika Chama chetu kuchukua wanawake wengi wa kutosha, kwa maana hiyo tunaendelea kumpongeza sisi kwa nafasi yetu ya jinsia ya akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawishika kuchangia hoja hii kwa sababu mojawapo ni mdau wa sehemu hii ambayo inaongezwa kwenye hifadhi ya Ruaha. Mimi naomba nianze kwa kuunga mkono na kuipongeza Serikali kwa uamuzi huu mzuri wa kupanua. Mimi nasema imepandisha hadhi ya sehemu ambayo ilikuwa ni *game reserve*

sasa inakuwa kwenye nafasi ya utalii. Hifadhi ya Taifa kitu ambacho kilikuwa ni ndoto kwa nyanda za juu Kusini tukawa kila wakati tunalilia kwamba ni lini tunapata eneo sehemu za utalii. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa hilo.

Napongeza kwa sababu tangu zoezi hili kuanza waliweza kutushirikisha kwa ukaribu viongozi wote wa Mkoa wa Mbeya, tulifanya kikao cha pamoja na hata Wabunge wote tunaotoka Mkoa wa Mbeya kiliandaliwa kikao rasmi ambacho tulikaa kwa pamoja tukakubaliana na kuunga mkono Azimio hilo na kukubaliana na sehemu ambazo tungependa ziingie kwenye hifadhi hiyo. Kwa hiyo, naipongeza Wizara hii kwa kutushirikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niseme kitu kimoja kwamba maendeleo mara nyingi yanakuwa na gharama kwamba unaposema unapanua hifadhi maana yake kuna wananchi au kuna eneo ambalo litahusika ambalo lilikuwa linakaliwa na wananchi. Sasa ninapozungumza wakati Azimio hili linaletwa kule Mkoani au pendekezo hili linaletwa Wilayani kwangu vijiji vilivyokuwa vimependekezwa kuingia kwenye hifadhi vilikuwa vinapata vijiji saba na vitongoji vitatu. Sasa leo baada ya Azimio ambalo limeletwa na Mheshimiwa Waziri hapa linazungumzia vijiji kumi na moja. Ukiangalia Azimio lenyewe linaonyesha tu *points* au mpaka, inaniwia vigumu mimi mwakilishi wa eneo hili kujua sasa ni vijiji gani ambavyo tena vitaongezwa kwenda kwenye vijiji saba hadi vifikie kumi na moja.

Unapozungumzia kijiji kimoja kwenye eneo la Mbarali maana yake unazungumzia idadi ya watu wasiopungua elfu tano au sita kwa sababu vijiji vya kwangu ni vikubwa sana. Nikikumbuka nilipoanza zoezi hili tulipewa vijiji saba na tukawashirikisha wananchi, tuliwahamasisha na tukawaambia kwamba Wizara ilileta mapendekezo ya vijiji kama hivi kumi na moja. Lakini tulipitia ramani kwa pamoja na wataalamu ambao walikuja tukakubaliana kwamba kwa sababu sasa Mbarali eneo kubwa ambalo walikuwa wanategemea kulima limebinafsishwa na wananchi wakaanza kutafuta maeneo mengine ya kulima ambapo sasa walianza kuandaa sehemu hiyo ambayo ndiyo sasa inaongezwa kwenye hifadhi. Kwa kikao kile tulikubaliana katika hivi vijiji saba na vitongoji hivyo na ndivyo tulivyokwenda kuhamasisha.

Nimekuwa nikizunguka safari hii wakati hatuko Bungeni, wakati nafanya ziara kwenye jimbo langu nimekuwa nikipata maswali haya kwamba Mheshimiwa tunasikia kijiji fulani kinaingia. Nasema hapana tulikaa kwenye *RCC*, tulikaa na watu wa Wizara, tulikaa na watu wa *TANAPA* tukakubaliana kwamba hivi vijiji ndivyo ninavyoingia kwenye hifadhi. Lakini nikasema haiwezekani ngoja niende kwa Mkuu wa Mkoa nikamwone. Nilipofika kwa Mkuu wa Mkoa kumwuliza akasema mpaka sasa hatujapata taarifa ya nyongeza ya vijiji vingine vyovyote, ni hivi saba na vitongoji hivyo vitatu. Sasa leo nilikuwa nafikiria ingekuwa vizuri Waziri basi akasema ni vijiji gani na kwa barua ya mwisho ilikuwa inasema havitaguswa vijiji vingine vyovyote ambavyo wananchi hawajahamasishwa maana ukisema saba unaleta vinne tayari, ni mambo ambayo yatawasumbua sana wananchi. Kwa sababu ninachowapongeza wananchi wa Mbarali baada ya kupata Azimio la vijiji saba tulivyozunguka walikubali kwa moyo

mmoja na ninapozungumza hapa wengine wamesema kwa kweli tumeambiwa tusilime na wameanza kuhama kwenda kwenye maeneo mapya.

Sasa ukigusa tena vijiji vingine hivi vinne vipya sijaelewa mpango maana yake utakapopitisha Azimio ndani ya Bunge maana yake ni sheria imepita itakuwa sio rahisi tena kuja kurekebisha kwamba hili eneo lipunguzwe. Sasa ningeomba nipate ufafanuzi hivi vijiji vilisahaulika hapo mwanzo au ni vile ambavyo kikao cha *RCC* kiliona kwamba si vizuri vikaingia angalau libaki eneo ambalo litawasaidia wananchi kwa ajili ya kilimo kwa sababu vijiji vilikuwa vinaguswa mpaka yale mashamba ambayo yamebinafsishwa. Kwa hiyo, nitaomba nipate ufafanuzi wa hivi vijiji vingine ambavyo vimeongezeka na vitongoji ambavyo vimeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niipongeze Wizara tuliyokubaliana baada ya kuhamasishwa. Kwa kweli wamefanya jitihada kubwa kuja kufanya tathmini kwa wakati muafaka na kwa sababu walikuwa wameazimia kabisa kwamba msimu huu wananchi wasilime hizo sehemu ambazo wanatakiwa kuhama wakalime kwenye makazi mapya na wananchi wameitikia. Sasa kuna tatizo na malalamiko ambayo yamejitokeza baada ya hii tathmini na malipo kuanza. Tatizo lenyewe ni kwa upande wa viwango ambavyo vimetumika kuwalipa. Sasa unapomlipa mtu shilingi 40,000/= ili asafirishe mizigo kutoka kijiji anachotoka mpaka anakokwenda wanasema tunamlipa yule ambaye ni mmiliki wa makazi yale lakini ana familia na vyombo hawezi kuviacha. Na sisi tutakuwa tunawahamasisha na tuliwaeleza vizuri na tulikubaliana vizuri na kwa uzuri tuliongozana na watu wa *TANAPA* tukakubaliana kwamba mtahamia sehemu ambayo mmeichagua wenyewe, shule, maji kama mna zahanati vyote vitakwenda kujengwa na *TANAPA* wenyewe. Sasa inapokuja kwenye malipo kwa kweli ile fidia imeleta malalamiko sana na tangu nimekuja hapa ni simu tu, Mheshimiwa hivi hela yetu ni lini utakuja kufanya tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kuona malalamiko yamezidi tuliamua kuitisha Baraza la Madiwani kwenye Halmashauri yangu tukakaa pamoja, tukawaita na Maofisa wa *TANAPA* na wale ambao walihusika kufanya tathmini. Inaonekana kuna mambo ambayo yamejitokeza ambayo hayakwenda vizuri. Kwa hiyo, wakaahidi kwamba wangeweza kurudia. Sasa mpaka leo ninapochangia mpaka jana ikawa hili zoezi bado halijakamilika. Sasa kwa sababu watu wanaogopa kubomoa zile nyumba au kubeba bati zao wakajenge
kwenye makazi mapya wanasubiri tathmini, ningeomba tu Mheshimiwa Waziri kwamba atume ujumbe wake au kile kikundi alichokipeleka kwa ajili ya kufanya tathmini na kuwapa fidia wafanye haraka kwa sababu kipindi hiki ni msimu wa mvua. Lakini tulichokubaliana cha muhimu ilikuwa ni mambo ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii alipokuja alisema fedha kwa ajili ya miundombinu tayari zimepatikana. Lakini tulichokubaliana eneo likishaainishwa ni *TANAPA* wenyewe wanakwenda kujenga shule iliyo nzuri zaidi kuliko pale wananchi wamehama kwa sababu zilishajengwa na MMEM zile. Lakini vilevile miundombinu kama barabara angalau barabara zitayarishwe, zahanati zijengwe kwa sababu vijiji vyote hivi ninavyohama vilikuwa na zahanati. Sasa wananchi

wameshatangulia, ningefikiri ingekuwa ni vizuri na Serikali ikaenda sambamba na kasi ya wananchi, zile fedha walizolipwa wakianza kuzitumia vinginevyo maana itakuwa ni tatizo kubwa tena baadaye kuja kuwahamisha tena hiyo sehemu. Lakini mpaka sasa ni bado hilo zoezi halijaanza kufanyika.

Kwa hiyo, ningeomba Serikali iongeze kasi ya kwenda kuwawekea hiyo miundombinu hasa maji kwa sababu mtu huwezi kujenga bila kuwa na maji, hicho ndhicho kitu ambacho walikuwa wanasisitiza. Lakini vilevile na hivyo viwango vipitiwe upya kwa sababu wananchi kwa kweli wanalalamika sana na kumekuwa na tofauti tofauti ambazo haikidhi haya. Hatusemi kwamba umpe thamani kubwa zaidi ya kile ulichokuwa nacho lakini angalau kiendane na wakati. Kwa sababu siku hizi bei ya vijijini na mjini karibu zinaendana. Mfuko wa saruji kijijini ni ghali zaidi kuliko wa mjini, lakini sasa mtu akilipwa laki tatu au mbili kwenye nyumba nzima kwa kweli inakuwa haimsaidii kumfanya ahamie huko tena. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo malalamiko ambayo wananchi naamini kabisa Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwa kasi aliyokwenda nayo tangu mwanzo mpaka sasa atawasaidia wananchi hawa kurudia kufanya tathmini yao lakini vilevile watoe fidia wanazopewa ziwawezesha kwenda kujenga tena makazi mapya ambayo ni bora kuliko ambako wametoka.

Tatizo lingine ni kwa upande wa mashamba. Wanachopewa ni fidia ya makazi na mashamba lakini kule wanakohamia inakuwa ni tatizo kupata mashamba maana yake waliambiwa mnapewa fedha lakini eneo la kulima itabidi mjitafutie. Sasa sijajua makubaliano yalikuwaje, nitamwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi. Lakini baada ya kusema hayo nilisema ni mambo ya kuzingatia, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu ile Ihefu ilikuwa ni hazina kwa Wilaya ya Mbarali. Kwa kweli nyongeza hii na upandishaji wa hadhi wa sehemu hii naamini kabisa utaongeza ajira kwa wananchi wa Mbarali. Lakini cha msisitizo ni hivyo vijiji vinne kwa kweli vimenigusa sana kwamba vitakuwa ni vijiji gani maana yake nikipata picha yenyewe mimi ninayefahamu hilo eneo vijiji vinagusa sehemu ambazo wananchi wanalima kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia mambo mengi Mbarali yametokea kwa miaka hii miwili. Wamehamisha mifugo, mashamba yameuzwa, hifadhi imeongezeka, kwa hiyo, bado wananchi watakuwa wana nyumba, angalau lingezingatiwa hilo. Kwa sababu tunaamini kilimo hakiwezi kuwa *substitute* ya utalii. Wanaolima watalima, watakaopata ajira za utalii watazipata. Kwa hiyo, ningeomba hilo Waziri alizingatie, aangalie vijiji na kama inabidi kweli viongezwe atupe sababu na kama inawezekana basi vijiji angalau vingebaki. Ahsante sana naomba niunge mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Azimio hili na mimi sina tatizo na Azimio hili, naliunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii nina mchango wangu kidogo kuhusu upandishwaji hadhi mapori au Hifadhi za Kitaifa kama ilivyo Ruaha. Hifadhi ya Taifa ya Ruaha inapakana na Tarafa ya Rudi, Wilayani Mpwapwa na

Tarafa ya Rudi kuna *game controlled area* ambayo ni ya muda mrefu na kuna wanyama wengi na nitaomba Mheshimiwa Waziri atafute siku yoyote aweze kutembelea pori hilo ili aweze kutushauri. Lakini naomba pamoja na kufikiria kupandisha hadhi ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha vilevile nilikuwa nashauri hii *game controlled area* ya Rudi ingepandishwa iwe *game reserve.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo. Kwanza kama nilivyosema kuna wanyama wengi na mimi nina hakika kama itapandishwa hadhi kwa *game reserve* itatusaidia sana wananchi wa Mpwapwa, kwanza, watalii watafika maeneo hayo na watalii wakifika kutembelea eneo hilo *game reserve* ya Rudi basi watakuza uchumi wa nchi yetu na ukishakuza uchumi tuna uhakika wa kuboresha maisha au kuboresha maeneo yale yanayozungumza *game controlled area* ya Rudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nina hakika kwamba Rudi *game controlled area* ikipandishwa kuwa *game reserve* tutapata fedha kwa sababu sasa hivi Serikali haitengi fedha kwa ajili ya kuangalia pori lile. Lakini kama ikipandishwa hadhi nina hakika kabisa kwamba itatenga fedha kwa ajili kusimamia au kuangalia pori hilo. Vilevile itasaidia sana kukuza ajira maeneo yale, pamoja na kukuza ajira nina hakika tutaboresha miundombinu kama vile barabara. Wananchi wa Tarafa ya Rudi wana matatizo makubwa sana ya mawasiliano, kwa hiyo, ukishapandisha hadhi watalii watakuwa wengi, tutapata kwa hiyo, tutaboresha miundombinu lakini Tarafa ya Rudi tutaboresha huduma za kijamii kama vile shule, kuboresha vituo vya afya pamoja na zahanati. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atafute nafasi ili aweze kwenda kutembelea eneo hilo ili tuweze kumpa maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwamba tunapopandisha maeneo haya tunakuza uchumi wa nchi yetu na kuboresha miundombinu, huduma za kijamii na kuboresha maisha ya wananchi wetu. Nilikuwa na mchango mfupi tu nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, bahati yako Prof. Mwalyosi kwa sababu nilikwishafunga orodha. Sababu huyu mzee amezungumza dakika tano basi unazo zingine na wewe 10 tu. Nakushukuru sana Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hata kama ni kidogo na mimi nichangie kwenye Azimio hili. Nataka nichangie kwenye maeneo mawili, kwanza kiujumla halafu ya pili kuhusu Mkomazi na Ruaha kila moja peke yake. Katika mambo ambayo nataka kuzungumzia kwa ujumla ni kwamba hifadhi nyingi ambazo tumezianzisha miaka iliyopita hazikuwa endelevu. Hifadhi hizi nyingi hazijakuwa endelevu kwa sababu wakati mwingine utaona ni ndogo sana kiasi kwamba hazitoshelezi mahitaji ya viumbe wanaokaa au kutumia hifadhi kwa kuwawezesha kusafiri, kuondoka au kutumia eneo lao kikamilifu wakati mbalimbali wa mwaka. Kwa mfano,wakati wa kiangazi ambapo labda maji ni haba kama ni wanyama wanatakiwa waende kwenye maeneo ambayo yana maji ya kutosha au labda maeneo mengine yanakuwa na wadudu. Wanyama wanaweza wakahama waache

maeneo ambayo hayafai wakati wa kipindi hicho. Hivyo, hifadhi nyingi ambazo zinakuwa ndogo zinakuwa na matatizo hayo ya kutokuwa endelevu.

Kwa hiyo, tunazungumzia mambo ya kutenga mazingira ambayo yanajitosheleza kwamba viumbe wanaoishi mle wanaweza kupata kila kitu, huduma, chakula, maji kwamba eneo lile linawatosha kabisa bila kuwataka watoke nje ya hifadhi ile. Sasa kitendo hiki cha kuongeza hifadhi hizi kuwa kubwa kinachangia sana kwenye kuboresha na kuzifanya hizi hifadhi ziwe endelevu, hivyo ni kitendo kizuri sana ambacho kinatakiwa kipewe kiungwe mkono.

Vilevile kuna suala la kuwa na uhakika kwamba uhifadhi wenyewe unajitosheleza kwa maana kwamba ilipokuwa *game reserve* au *game controlled area* maeneo haya hayana kinga ya kutosha kuhakikisha kwamba viumbe wanaoishi humo kwenye hifadhi wana kinga ya kutosha. Kwa sababu aina nyingine za hifadhi zinaruhusu kwenda kuvuna lakini hifadhi ya namna hii yaani *National Park* hairuhusiwi kuingiza kitu au kutoa kitu, kwa hiyo tunasema ni *maximum protection*. Ni hali ya ngazi ya juu sana ya kuwahifadhi viumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupandisha hadhi kutoka *game reserve* kuwa *National Park* tunachofaidi ni kwamba tuna uhakika viumbe waliomo mle wanahifadhiwa vilivyo, hatuwi na mashaka kwamba wanaweza kuathirika. Lakini nitoe maombi kwamba hebu tuangalie maeneo mengine ambayo aidha hifadhi ni ndogo sana kiasi kwamba sio endelevu. Kama kuna uwezekano wa kuzipanua kwa kuhusisha maeneo mengine yaliyo nje kusudi yahusishwe kwenye hifadhi basi tufanye hivyo kabla hatujachelewa sana na kabla viumbe wengi hawajaathirika au kupotea; na hapa ningependa kushauri kwamba mpango wa Milima ya Livingstone kutaka kuongeza kwenye Hifadhi ya Kitulo pamoja na Milima ya Rungwe ni mizuri. Nadhani wazo kama hilo lingekuja upesi kabla watu hawajazagaa, na kuchukua maeneo yote halafu inakuwa ni gharama lakini vilevile viumbe waliomo mle wanazidi kupotea. Kwa hiyo, ni vyema tukalishughulikia hili kama tuna nia kweli ya kuendeleza maeneo hayo kuhifadhi viumbe na mazingira ya kule basi tufanye hivyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuzungumzia kuhusu suala la Mkomazi la kupandisha hadhi kutoka *game reserve* na kuwa *National Park*. Kwa sababu kati ya malalamiko tuliyokuwa tunayapata kwa majirani zetu wa Kenya mara nyingi kwa kuwa mimi ni mtu wa *conservation* kwamba wakati tukiwa upande mmoja wa mpaka na *game reserve* wenzetu wana *National Park.* Kwa hiyo, kunakuwa na tatizo kwa kuwa sisi tunahifadhi wanyama nusu nusu na tunaruhusu kuwinda wakati jirani zetu ng’ambo ya mpaka hawaruhusiwi kuwinda. Kwa hiyo, ujangili unatokea wakati mtu anamfukuza mnyama mpaka anaingia kwenye hifadhi upande wa pili wa mpaka anamfuatilia kule na anavunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunasema sisi sote tukiwa na hifadhi zinazofanana pande zote mbili za mpaka inaondoa ugomvi kati ya Kenya na Tanzania kwa sababu aina ya hifadhi ambazo tumeziweka kwenye mpaka zinafanana. Kwa hiyo, nataka kumsifu na kumpongeza Waziri kwa kitendo hiki kwamba kitatuondolea ugomvi

uliokuwa unatokea kati ya majirani zetu wa Kenya na sisi kuhusiana na matatizo ya upande mmoja kuwa na hifadhi tofauti na upande mwingine wa mpaka.

Kwa upande wa Ruaha nataka nizungumzie suala la, sitajua Kiswahili chake ni nini lakini tunasema Ihefu na Mto Great Ruaha mkubwa na mdogo ndio uhai wa Tanzania. Kuhusu umeme, samaki na *prawns* hadi kule kwenye Bahari ya Hindi inategemeana na vitu gani uhifadhi wa mahali kama Ihefu ambako maeneo mengine ni ya mazalio. Kwa hiyo, ni *strategic* kuweka eneo lile lihifadhiwe kwni linasaidia bonde zima la Mto Ruaha kuwa limehifadhiwa kwa namna fulani. Kwa hiyo, ni kitendo kizuri sana kupanua hifadhi ile na kuliweka eneo kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa hifadhi ya Ruaha peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ya pili na kama alivyozungumza Mbunge mwenzangu aliyetangulia kwamba mapato yanayoongezeka kwa kupanua ukubwa wa hifadhi kwani Wilaya nyingi zinazunguka hifadhi hiyo na vijiji vingi zaidi kwa hiyo hata kile kinachotolewa *TANAPA* kupitia utaratibu wa ujirani mwema kama ujenzi wa mashule, mahospitali na kadhalika, vijiji na Wilaya nyingi zitafaidika na mchango unaotolewa na hifadhi kwenye Halmashauri. Lakini kikubwa zaidi ni kwamba tunazungumzia Wilaya na vijiji vya eneo la Kusini kwa sababu mara nyingi tumesema wenzetu wanaofaidi na hifadhi walikuwa ni wa Kaskazini ambako ndiko kulikuwa na hifadhi nyingi. Kwa hiyo, mapato yanayogawiwa kwenye Halmashauri walikuwa wanafaidika wenzetu zaidi pengine kuliko watu wa Kusini na sisi tukiongezewa ukubwa wa hifadhi, Halmashauri zetu zinaweza kupata chochote kutokana na uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nilitaka niunge mkono Azimio hili tulikubali ili hifadhi hizo zianze kufanya kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante nakushukuru sana tuko *within the time*. Kwa hiyo, nitamwita mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo yaliyozungumzwa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kutenga muda huu na kunipa nafasi niweze kujibu hoja chache ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa michango yao katika kuboresha hoja ya Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Kuanzisha Hifadhi Mpya ya Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niwatambue wale ambao wametoa michango yao ya kuongea humu ndani ya Bunge na halafu nitawatambua wale ambao wametoa michango yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasemaji 16 wamechangia hoja hii. Nao ni Mheshimiwa James Lembeli, Msemaji wa Kamati ya Mazingira na Maliasili, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Kaika

Telele, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi.

Waheshimiwa Wabunge ambao walitoa michango yao kwa maandishi ni Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wametoa michango mingi na michango mizuri sana. Michango hii imehusu uhifadhi wa maliasili zetu na hasa wanyamapori kwa ujumla, uhifadhi viumbe na baionuwai mbalimbali ikiwa pamoja na viumbe, wanyama na mimea pamoja na uhifadhi wa misitu na rai kwa Serikali ni kuangalia kwa ujumla hivi ni maeneo gani ambayo kwa sasa tungeyaunganisha pamoja au tungeyapandisha hadhi ili kuleta uwiano mzuri na kulinda maliasili ambazo Mwenyezi Mungu ametupa kwa ajili ya kizazi hiki na kwa ajili ya wajukuu zetu na vizazi ambavyo vitafuata. Mawazo haya na michango ambayo imetolewa leo ni michango mizuri sana na sisi katika Wizara tutaifanyia kazi tukishirikiana na Bunge lako tukufu ili kuweza kuhakikisha kwamba Tanzania nchi ambayo imepewa na Mwenyezi Mungu viumbe vya aina nyingi sana na katika eneo la wanyamapori, wanayama wengi zaidi kuliko nchio yoyote Duniani, basi inafaidika na rasilimali hii kwa sasa na kwa wajukuu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yametolewa maelezo ya jumla kuhusu sheria ambazo zinahusu uhifadhi na hasa sheria ya wanyamapori. Ningependa kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba sheria hiyo sasa inapitiwa baada ya kurekebisha na kurudufu sera ya wanyamapori kuruhusu ufugaji wa wanyamapori katika mashamba madogo na kuwepo kwa ranchi za wanyapori, kuingiza maeneo oevu katika sera ya wanyamapori. Sasa Sheria inapitiwa kwa makini na kwa undani sana kulingana na mawazo ambayo tunayopewa Bungeni ili tuweze kuileta hapa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa upya kulingana na hali tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitaanza kuangalia na kupitia maeneo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyapendekeza na kuyatolea maelezo kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kwamba Wizara na Wabunge wa Wilaya ya Rungwe tusaidiane kufafanua mipaka ya Kitulo upande wa Magharibi kuhusiana na *Beacons* mpya. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya. Ninapenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu kupitia *TANAPA* tutatuma wataalamu katika eneo hilo ili washirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Mbeya Vijijini kuangalia mipaka ya Pori la Kitulo ili kuhakiki na kuhakikisha kwamba mipaka hiyo inajulikana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imetolewa hoja kwamba wakati umefika kuangalia uwezekano wa kuunganisha Hifadhi ya Misitu ya Rungwe pamoja na Hifadhi za Misitu katika Safu za Milima Livingstone ili kuweza kunusuru viumbe ambavyo ni vya pekee vinavyopatikana katika maeneo hayo. Zoezi hili limekwishaanzishwa katika Halmashauri zinazohusika na Wizara yangu inangoja mapendekezo kutoka kwenye *RCC* na itashirikiana na Halamashauri pamoja na *RCC* ya Mkoa wa Mbeya ili kuhakikisha kwamba Azimio hili linafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko katika ulipaji fidia kwa wanaohamishwa Usangu. Ulipaji fidia hata Mkomazi uangaliwe ili kupunguza malalamiko hayo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa James Lembeli na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Ulipaji wa fidia unafanyika kwa awamu katika Wilaya ya Mbarali. Vijiji vilivyothaminiwa ambavyo tathmini ilikwishafanyika mwanzo, vimekwishalipwa jumla ya shilingi bilioni 2.75. Uthamini unaendelea kwa vijiji vilivyosalia na wananchi watalipwa kila baada ya hesabu kukamilika. Kama nilivyoeleza katika maelezo ya awali ya maazimio ambayo nayapendekeza, Serikali imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya malipo hayo. Tunategemea kwamba tathmini hii na malipo yatakamilika katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Aidha, Serikali iko makini kuhakikisha kwamba hakuna udanganyifu katika zoezi zima la ulipaji fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamejitokeza watu amabo wanatoka katika maeneo ya miji wakija na pikipiki zao kudai kwamba nao wana mashamba au mali katika maeneo hayo. Serikali inahakiki madai hayo kwa karibu sana ili kuhakikisha kwamba kila mtu anayedai ni kweli ana mali katika eneo hilo. Mchakato wa kuazisha na kupanua hifadhi uliambatana pia na kutoia elimu kwa vijiji husika kwa kusaidiana na Halamashauri za Wilaya na Mkoa. Hivyo, ni mategemeo yetu kwamba wananchi wengi wanaelewa ni kwa sababu gani wanahamishwa na ni kwa sababu gani wanalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya viwango vya ada za uwindaji ifikishwe Bungeni mapema mwezi Januari ili Serikali ipate mapato zaidi. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba ada na viwango vya uwindaji vilipandishwa kama hatua ya mapato ya bajeti na kwamba ada mpya za uwindaji zilitangazwa katika katika Tangazo la Serikali Na. 158 la tarehe 29 Juni, 2007. Tangazo hilo halitabadilishwa katika kipindi hiki cha bajeti. Aidha, ada hizi zitaangaliwa upya kama tunavyokwenda na katika hatua nyingine wakati wa kipindi kingine cha bajeti tutaangalia ni maeneo gani ambayo yanaweza kuhusika yakatupatia mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya kifuta machozi kwa wanaoumizwa au kuharibiwa mali zao na wanyamapori viwe sawa nchi nzima na vipandishwe. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. Viwango vya kifuta machozi viko sawa kwa nchi nzima. Viwango hivyo viliongezwa mwezi Juni mwaka huu kutoka shilingi 50,000/= hadi shilingi 100,000/= kwa uharibifu wa mazao kwa kila hekta moja ya mazao na shilingi 200,000/= kwa watu wanaouawa na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tembo wa Saadani wamekuwa kero, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Rished Abdallah. *TANAPA* itashirikiana na Halamashauri ya Wilaya ya Pangani kuangalia kwamba ni namna gani wanaweza kushughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa *Natural Reserve* katika Wilaya ya Kilombero, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Castor Ligallama. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *Natural Reserve* imekwishaanzishwa na Tangazo la Serikali Na. 182 lililotolewa katika mwaka huu wa fedha katika eneo la Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya Hifadhi ya Udzungwa ipitiwe ili kuzingatia huduma za jamii, si rahisi kurudisha ndani mipaka ya Hifadhi ya Udzungwa kwa sababu mpaka unapita kwenye gema la mlima. Hata hivyo, kama ni lazima sana mipaka hiyo irekebishwe, utaratibu uliotumika wa kuanzisha hifadhi hiyo, ni ule ule ambao unatakiwa kutumika katika kurekebisha mipaka hiyo. Pendekezo kama hilo limetolewa na Mheshimiwa Felix Kijiko, limetolewa na Mheshimiwa Rwilomba, na kwa kweli msingi wa jibu ni huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetolewa hoja kwamba kuwe na udhibiti wa vitendo vya ujangili, ukataji wa magogo na kadhalika. Aidha, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Janeth Massaburi wametoa hoja kwamba kukuza utalii wa ndani na utamaduni wa Watanzania kutembelea katika Hifadhi zetu za Taifa uwekewe msukumo. Wizazra inazingatia suala hili na tayari kuna Programu ya kuhamasisha Watanzania na wananchi kwa ujumla kutembelea Mbuga zetu za Wanyama. Katika hatua hiyo, wakati was Maonyesho ya Saba Saba kunakuwa na magari yanayopeleka Watanzania kwenda kutembelea Mbuga zetu za Mikumi na zingine na katika mwisho wa wiki katika miji ya Arusha wananachi wanahamasishwa kutembelea Hifadhi za Taifa za Tarangire na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke mikakati ya usimamizi thabiti eneo la Hifadhi kubwa ya Ruaha. Haya ni mapendekezo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani na Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Magdalena Sakaya. *TANAPA* inafanya juhudi za kuajiri ili kuziba mapengo ambayo yanaanzishwa na Hifadhi hizi na mapema mwezi huu tumetangaza kuongeza askari 100. Aidha, katika Azimio ambalo nimelipendekeza, tumependekeza kuongeza wafanyakazi 120 wa ziada ikiwa ni pamoja na askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya pekee ya Pori la *Selous* imepokelwa na ilipendekezwa na Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Izumbe Msindai. Hoja hii kwa kweli tumeipokea na tutaijadili na kuangalia ni namna gani itaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaozunguka Hifadhi washirikishwe ikiwa ni pamoja na kuwapatia vijana ajira ya kuweka miundombinu kwa ajili ya wananchi na mifugo. Hoja hii imetolewa na Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, imetolewa pia na Mheshimiwa Izumbe Msindai na Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

Wizara ina mpango maalumu wa ushirikishwaji wananchi katika uhifadhi na kwa *TANAPA* ni kupitia programu ya ujirani mwema. Wizara itaendeleza programu hizo kwa msukumo zaidi pale ambapo matatizo yatajitokeza. Nigependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba katika bajeti ya Shirika la Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)* kwa mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza programu ya ujirani mwema katika vijiji ambavyo vinazunguka na vile ambavyo vinahamasishwa uhifadhi wanayamapori na baioanuai muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwe makini kulinda Faru wa Mkoamazi na hata Faru hawa ambao wanatunzwa kwenye uzio. Pia iangalie upya msitu wa Shengena uwe sehemu ya Hifadhi inayopendekezwa ya Mkomazi, kuwekwe geti la Utalii kati ya Hifadhi inayozunguka Mkomazi kwa upande wa Kenya. Hoja hizi zimetolewa na Mheshimiwa Izumbe Msindai, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Rished Abdallah na wengine ambao wamezungumzia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuweka geti la kuunganisha geti mbili katika *Parks* zetu ambazo moja iko Kenya na nyingine Tanzania, itategemea vigezo mbalimbali. Aidha, tungependelea watalii wanaoingia Tanzania kutokea Kenya wasije tu kupitia kwenye utalii wetu wakila *packed lunch* zao katika mapori yetu na halafu kurudi Kenya kulala. Tungependa watalii wakiingia Tanzania waweze kuingia na kutumia huduma za Tanzania pamoja na huduma za usafiri, huduma za hoteli na huduma zingine ili tuweze kufaidika na utalii kama ambavyo wanafaidika wenzetu. Kwa hiyo, hoja ya kuweka na kufungua geti katika eneo hilo itafikiriwa kuzingatia kigezo hicho ili tuweze kufaidika na pori hili, lisiwe tu linakuwa *extension* ya *Tsavo National Park. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba watu wanaweza kuhamishwa katika Hifadhi ya Mkomazi na hoja hii imetolewa na Mheshimiwea David Mathayo David. Ningependa kueleza kwamba hivi karibuni ulifanywa mkutano wa wadau katika Mkoa wa Kilimanjaro ukiwahusisha Wabunge, viongozi wa Wilaya na Madiwani ambao Kata zao zinazunguka Hifadhi hiyo. Kumekuwa na mapendekezo ambayo yameletwa wizarani kwangu, mapendekezo hayo yatazingatiwa na Wizara yangu. Hivyo hakuna watu walio nje ya mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ambao watahamishwa kama ambavyo watu wengine wamekuwa na hofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja hapa kwamba Wawindaji wa Utalii wanakataza watu wasiwekeze mizinga katika maeneo hayo. Ni nia yetu katika Wizara ya Maliasili na Utalii kukuza sana biashara na *industry* hii ya kufuga nyuki, kutengeneza asali na nta na mazao mengine ya asali. Tunaamini pia kwamba ufugaji wa nyuki ni kichocheo kikubwa cha kuzuia wananchi wasichome misitu, wasichome mapori na maeneo mengine kwa sababu kama wana misitu yao ndani ya mapori hayo na wenyewe wamewekeza, wanakuwa ni wadau muhimu katika suala hili. Kwa hiyo, tutakuwa tunaendelea kuzungumza na wenye vitalu na kuwahimiza wananchi kuwekeza mizinga katika maeneo hayo na maeneo mengine ya mapori ili kupunguza moto ambao unawaka kila mwaka katika mapori yetu ya kuhifadhi wanyamapori katika misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Mabarali ameeleza kwa kirefu kidogo kuhusu kazi ya uhakiki ambayo ilifanywa awali na ile ambayo imeonekana katika maazimio yetu. Aidha, pendekezo lililokuwa mwanzoni lilikuwa kwa vijiji 7 ndivyo vingehama na vitongoji 3 vya ziada. Aidha Azimio linahusu vijiji 11 na vitongoji 5. Hii ilitokana na vijiji hivyo vilivyo kwenye Azimio kutokuonekana kwenye ramani wakati wa awali na baadaye wakati wa kuhakiki mipaka kwa kuzingatia mpaka uliopitishwa na *RCC* ya Mkoa wa Mbeya. Vijiji 4 zaidi na vitongoji 2 vya ziada vilionekana kwamba vitaguswa na hatua hii, hivyo Azimio hilo lilijumuisha eneo lilohusu vijiji hivyo. Baada ya kuona hayo, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa pamoja na Wilaya ya Mbarali, iliandaa ratiba ya uhamasishaji na umefanyika katika eneo hilo na hasa katika vijiji vya Msanga na vitongoji vyake na tathmini pia inaendelea kwa vijiji hivyo kuthamini mali za wananchi wa vijiji vya Luhanga, Madundasi, Iyala na vitongoji vya Mwanavala na Ifushiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu, tayari Shirika limetenga shilingi milioni 114 kwa ajili ya kuhudumia miundombinu. Fedha hizi zitapelekwa kwenye Wilaya ya Mbarali hivi karibuni. Aidha, katika makubaliano ambayo tunayo na Mkoa wa Mbeya pamoja na Wilaya ya Mbarali, Serikali itahakikisha kwamba huduma za jamii zinazotolewa na miundombinu inayojengwa ya shule, zahanati na barabara itakuwa bora zaidi kuliko zile ambazo zilikuwa zimejengwa na vijiji na tutahakikisha kwamba hatua hizi za kujenga miundombinu hiyo zitakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kutoa maelezo kwa kirefu kama nilivyoweza kutokana na muda ambao tunao. Labda limebaki suala moja tu ambalo limetolewa na Mheshimiwa Prof. Mwalyosi kuhusu hiki kinachoitwa *Trans - Boundary Eco Systems -* matumizi ambayo yanatofautiana katika maeneo ambayo yametenganishwa na mpaka wa kimataifa kama ilivyo Mkomazi na *Tsavo National Park*. Utafiti uliofanywa katika eneo hili kwa miaka mingi umeonyesha kwamba ni bora kwa Mkomazi kupandishwa hadhi kuwa *National Park* ili uendelezaji na usimamizi wa maeneo haya uwe sawa sawa. Hatua hii ambayo tutaichukua hapa kama Bunge lako Tukufu litakubali mabadiliko haya, litaweza kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba maelezo haya pia nitayachapisha vizuri na kuwagawia wote ambao wametoa hoja zao. Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuanzishwa Hifadhi Mpya ya Taifa ya Mkomazi na Azimio la Kupanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yote mawili yaliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la kukibadilisha Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji**

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha Azimio la Kubadilisha Chuo cha Ufundi Arusha Kuwa Chuo Kinachojitegemea Kiutendaji *(The Arusha Technical College)*, naomba niungane na wenzangu walionitangulia ili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kilolo, nitoe rambi rambi kwa kifo cha Marehemu Salome Joseph Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amin. Aidha, napenda kutoa pole zangu za dhati kwa Waheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Mchinga kwa ajali walizopata. Namwomba Mwenyezi Mungu awape nafuu ya haraka ili waungane na Watanzania wengine katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baaada rambi rambi hizo na kwa namna ya kipekee, napenda kumpongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi - Taifa. Napenda pia niwapongeze wana-CCM wengine waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizi, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa maoni na mchango wao mkubwa ambao umechangia sana kuboresha Azimio la kugeuza Chuo cha Ufundi Arusha na kuwa Chuo cha Ufundi kinachojitegemea kiutendaji na kuwezesha Azimio hili kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuridhiwa. Aidha, natoa shukrani zangu kwa wataalamu wetu kwa jitihada zao katika hatua zote na matayarisho ya Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha Azimio, naomba kutoa taarifa ama utangulizi. Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1999 inatamka kuwa: "Ili kuviwezesha Vyuo na Taasisi za Ufundi kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi, ni vema vikajitegemea kiutendaji (*Autonomous*). Kwa kuzingatia Sheria Na.9 ya mwaka 1997 iliyoanzisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(The National Council for Technical Education – NACTE)* hususan kifungu 6(i), Waziri mwenye dhamana ya Elimu ya Juu, Sayansi na Technolojia, amepewa mamlaka ya kutoa tangazo *(Establishment Order)* katika Gazeti la Serikali ili kukiwezesha Chuo au Taasisi yoyote ya Ufundi ambayo imepata Ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kuwa Chuo au Taasisi inayajitegemea. Aidha, kifungu Na. 6(iii) cha sheria hiyo, kinamtaka Waziri muhusika kuwasilisha Azimio mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuridhia tangazo la kuanzisha Chuo au Taasisi ya Ufundi inayojitegemea kiutendaji.

Kwa kuzingatia matakwa ya sheria husika, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, amekamilisha taratibu zote za msingi za kukigeuza Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji ikiwemo kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali na kuandaa Azimio ambalo nitaliwasilisha hivi punde katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ufundi Arusha kwa sasa kinasimamiwa na Wizara moja kwa moja kupitia Baraza la Ushauri na Mkuu wa Chuo ambaye huteuliwa na Wizara. Hata hivyo, Baraza hilo halina nguvu zozote za kisheria kuliwezesha kutekeleza shughuli zake. Lengo la Wizara ni kutekeleza maelezo ya Sera ya kuwezesha Vyuo na Taasisi za Ufundi kujitegemea kiutendaji na hivyo kuwa huru na kubuni na kusimia mipango yao ya maendeleo. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Mawasiliano na wadau mbalimbali likiwemo Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Taasisi mbalimbali, kuhusu kuboresha hoja ya kukigeuza Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji.

(ii) Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Machi, 2007 ilijadili *Establishment Order* ya kugeuza Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji na kutoa mapendekezo ya kuboresha.

(iii) Tangazo (*Establishment Order)* kuhusu Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji limetolewa katika Gazeti la Serikali Toleo Na. 78 la tarehe 30 Machi, 2007. Waraka kuhusu Azimio hili umepitishwa na Baraza la Mawaziri katika kikao chake kilichofanyika tarehe 7 Novemba, 2007 mjini Dodoma.

(iv) Kama nilivyoeleza hapo awali, Azimio (*resolution)* la kukigeuza Chuo Cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji liko tayari na litawasilishwa hivi punde.

Rasilimali zinazohitajika kukigeuza Chuo Cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji zimekadiriwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 1/- ikiwa ni kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa Chuo chenyewe. Kiasi hiki cha fedha kimetengwa katika Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2007/08. Matokeo ya utekelezaji iwapo Chuo cha Ufundi Arusha kitageuzwa kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji yatakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Chuo kitaimarisha uhuru na uwajibikaji kiutendaji katika kuamua kutekeleza na kusimamia majukumu yake.

(ii) Maslahi ya Walimu na watumishi wengine katika chuo yataboreka, hivyo kuongeza tija na ufanisi zaidi katika utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo nchini.

(iii) Chuo kitaweza kubuni mipango mbalimbali inayolenga kukipatia mapato ya nyongeza ambayo yanaweza kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama za uendeshaji .

(iv) Chuo kitaweza kupanga na kutoa programu za mafunzo mbalimbali zenye kulenga kupata wataalamu wenye kukubalika katika mfumo wa sasa wa ujuzi wa kitaifa na kimataifa.

(v) Chuo kitakuwa na uwezo wa kushirikiana na vyuo rafiki ambapo vitaweza kubadilishana uzoefu na matumizi ya rasilimali mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo ya pande zote zinazohusika.

(vi) Kitakidhi mahitaji muhimu ya kupata wataalamu wa ngazi ya kati walioiva kivitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, sasa naomba kuwasilisha Azimio la kugeuza Chuo cha Ufundi Arusha kuwa chuo kinachojitegemea kiutendaji kama ifuatavyo:-

KWA KUWA katika mikakati ya kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania Serikali imeweka kipaumbele katika kuendeleza na kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia nchini;

NA KWA KUWA bado kuna mahitaji makubwa ya wataalamu katika nyanja za ufundi sanifu na teknolojia, ambapo Chuo cha Ufundi Arusha kitaendelea kutoa mafunzo yanayotolewa kwa sasa na kubuni programu mpya zitakazokidhi mahitaji katika ngazi za cheti na Stashahada zinazolenga katika kutoa wataalamu wenye ujuzi wa vitendo kuliko nadharia;

NA KWA KUWA Elimu ya ufundi na mafunzo ya mwaka 1995 inatamka bayana kuwa taasisi na vyuo vya ufundi nchini viwezeshwe kujitegemea ili viweze kubuni na kutoa maamuzi ya haraka na utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa lengo la kupanua na kuboresha utoaji wa elimu;

NA KWA KUWA katika kuimarisha Chuo Cha Ufundi Arusha kiweze kujitegemea kiutendaji Serikali imeelekeza nguvu katika ukarabati wa majengo, mitambo na vifaa mbalimbali na kununua vifaa vya kufundishia kama vile mashine, kompyuta na vitabu vya kiada na rejea na kwamba kwa sasa Serikali inasomesha baadhi ya Walimu mbalimbali ili kupata elimu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili *(Masters)* na Uzamivu *(Ph.D)*;

NA KWA KUWA Chuo Cha Ufundi Arusha kitawezesha kupanua na kuboresha elimu inayotolewa kwa kuendeleza na kuanzisha programu mpya za mafunzo mbalimbali katika ngazi za Cheti na Stashahada;

NA KWA KUWA katika fungu la 6(1) la Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129, Waziri wa Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia amepewa mamlaka ya kutangaza katika Gazeti la Serikali, chuo chochote kinachotoa elimu ya ufundi kuwa chuo kinachojitegemea baada ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kuzingatia mambo mbalimbali;

NA KWA KUWA Baraza limezingatia mambo mbalimbali muhimu ya Chuo cha Ufundi Arusha ikiwa ni pamoja na uwezo wa utoaji elimu, uwezo wa kudhibiti viwango vya elimu, vifaa vya kufundishia, watumishi na kwamba Baraza limethibitisha kuwa

Chuo kinafaa kujitegemea na nimepewa ushauri kukitangaza kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji na kwa kuzingatia misingi hiyo Chuo kimetangazwa katika Gazeti la Serikali, Tangazo Namba 78 la 30 Machi, 2007;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia masharti ya kifungu 6(3) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129, Bunge hili katika Mkutano wa Tisa sasa linaridhia Chuo Cha Ufundi Arusha (*Arusha Technical Collage*) kubadilishwa kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHESHIMIWA OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii uliyoipa kazi ya kufikiria Azimio la Bunge la kuridhia kubadilishwa kwa Chuo Cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji (*The Arusha Technical College).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilikutana na kupata maelezo ya kutosheleza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kuhusu uamuzi huo wa Serikali na Serikali kuchukua hatua muhimu inayofaa kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi katika kuendeleza Elimu ya Ufundi na pia kukiwezesha Chuo cha Ufundi Arusha kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanya maamuzi na kupanga mipango ya maendeleo ya Chuo bila kuchelewa kwa kusubiri uamuzi kuoka Wizarani.

Kamati inapongeza Serikali kwa uamuzi huo ambao unaonyesha wazi kutekeleza Sera ya Elimu ya Ufundi ya mwaka 1995 ambayo inaelekeza kuwa ili kuleta ufanisi katika Vyuo vya Ufundi, vijitegemee kiutendaji katika kuboresha utoaji wa Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inafahamu kuwa Chuo hiki kilikuwa chini ya Idara ya Elimu ya Ufundi katika Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na kuwa wakati mwingine baadhi ya shughuli za Chuo zilizohitaji maamuzi ya haraka zilichelewa kutekelezwa kutokana na maamumzi ya utekelezaji kufanywa Wizarani jambo linalojenga urasimu usio wa lazima.

Aidha Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaelewa kuwa kuwapo na ongezeko kubwa la shughuli za kiuchumi hapa nchini zinazohitaji mafundi katika nyanja za ujenzi wa miundombinu kama vile majengo, barabara, kufunguliwa migodi mipya ya madini nchini, mahitaji ya wataalamu kama vile wahandisi, mafundi sanifu na mafundi stadi katika nyanja mbalimbali yamezidi kuwa makubwa. Mafundi Sanifu (*technicians)* katika

mgawanyo wa kazi za ufundi ndio wasimamizi na wachapa kazi wakisaidiwa na mafundi wa kawaida (*artisans).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kuwa kiutendaji mhandisi mmoja anatakiwa asaidiwe na mafundi sanifu 5 na kila fundi sanifu anatakiwa asaidiwe na mafundi stadi 25. Kamati ilipata takwimu kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam *(DIT)* mwezi Juni, 2007 kuwa Mwaka 1996, kwa kila Mhandisi mmoja hapa nchini kulikuwa na mafundi sanifu 2 badala ya 5 na mafundi stadi 14 badala ya 25. Hivi sasa uwiano huo haufiki hapo kwa sababu mafundi sanifu waliopo ni wachache mno ukizingatia kwamba udahili katika Vyuo Vikuu umeongezeka ukilinganisha na udahili wa vyuo vya ufundi sanifu. Hivyo hatua hii ya Serikali inalenga kurekebisha uwiano huo wa mahitaji ya kada ya mafundi sanifu na mafundi stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ufundi Arusha kina uzoefu wa kutosha katika kutoa mafunzo ya ufundi sanifu na katika fani za Uhandisi. Kinazo programu nyingi za Teknolojia ya kisasa katika ngazi ya Ufundi Sanifu ambapo wahitimu hupata diploma katika mafunzo ya kompyuta, uhandisi wa elektroniki na mawasiliano ya anga, uhandisi migodi, uhandisi mitambo, uhandisi ujenzi, uhandisi umeme na sayansi na yeknolojia ya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, fani hizo zilizotajwa hapo juu mahitaji yake katika nchi ni makubwa sana, hivyo hatua ya kukiwezesha Chuo cha Ufundi Arusha kujitegemea katika maamuzi kutawezesha Uongozi wa Chuo kujipanga vizuri na kutumia raslimali za Chuo kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanachuo kufuatana na uwezo wa miundombinu ya Chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifahamu kuwa kubadilisha Chuo cha Ufundi Arusha kwa tamko tu hakutasaidia, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuwa Chuo hiki kipewe kipaumbele katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao na kukiwezesha kupata nyenzo za kisasa za kufundishia na hatimaye kupata wahitimu wa kutosheleza mahitaji ya soko waliobobea katika fani za Ufundi Sanifu zinazofundishwa Chuoni. Aidha, Kamati inashauri Chuo kuweka malengo na programu zinazozingatia mabadiliko katika matumizi ya sayansi na teknolojia ya kisasa ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inafahamu kuwa majengo ya Chuo cha Ufundi Arusha yanahitaji ukarabati mkubwa. Ni vema Serikali ikatoa kipaumbele katika kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu ya Chuo ili mabadiliko yanayotazamiwa yaanze vizuri, na hapa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kukiri kwamba Serikali imetenga karibu bajeti ya shilingi bilioni moja katika Mwaka wa Fedha wa 2007/08.

Mheshimwa Naibu Spika**,** kuhusu taaluma, Serikali inashauriwa kuwa katika kuinua hadhi ya Chuo hiki ni muhimu kuhakikisha kuwa walimu watakaofundisha waendelezwe ili wawe na taaluma ngazi ya Shahada ya Uzamili (*M.SC*) na Uzamivu (*Ph.Ds*) ili Chuo kiweze kuanzisha programu mpya za mafunzo mbalimbali katika ngazi zote zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizingatia kwamba upanuzi wa Elimu ya Sekondari na *VETA* ambao utaleta wahitimu baada ya Elimu ya Sekondari wengi wao watakosa nafasi za kutosha kuendelea na elimu ya juu, vijana watakaokosa kuendelea na Elimu ya juu wanaweza kupewa ujuzi na utaalamu wa ufundi sanifu na kuweza kujiajiri au kuwa watendaji wazuri endapo tutakiwezesha Chuo cha Ufundi Arusha kuwa na uwezo wa kupanua udahili kwenye programu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya tatizo la ongezeko la wanafunzi, nchi hii vilevile inahitaji teknolojia mpya katika nyanja mbalimbali ili tuweze kuhimili ushindani wa kimataifa kiuchumi. Hivi sasa Serikali inajitahidi kuboresha miundombinu kama vile barabara, reli, bandari, na inajenga madarasa na nyumba za walimu kupitia mpango wa MMEM na MMES na viwanja vyetu vya ndege na kadhalika. Mambo yote haya yanahitaji wataalamu wa ngazi za ufundi sanifu, ufundi stadi na wahandisi ili tuondokane na athari zinazotokana na udhaifu katika ubora wa majengo barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji katika nyanja hizo ni wahandisi, mafundi stadi na mafundi sanifu ambao hawatoshi kwa sababu Taasisi mama ya Elimu ya Ufundi *(DIT)* ikisaidiwa na Chuo cha Ufundi Arusha na Taasisi ya Ufundi Mbeya hazikidhi mahitaji halisi ya mafundi na wahandisi nchini, na zaidi nchi yetu haina Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia.

Tunaishauri Serikali iwe na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia kama ilivyoshauriwa mara kwa mara hapo nyuma. Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuikumbusha Serikali katika kuhakisha kuwa kila Wilaya inakuwa na Chuo cha Ufundi na ujenzi wa Vyuo vya kisasa vya *VETA* katika mikoa ya Pwani, Lindi na Manyara uharakishwe kwa lengo la kupanua mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** ni muhimu pia kwa Serikali kuangalia upya utaratibu utakaowezesha wahitimu wa Vyuo vya Ufundi na *VETA* kujiendeleza hadi kufikia ngazi ya Stashahada na Shahada kwa sababu utaratibu wa sasa hautoi nafasi ya kujiendeleza kwa masomo ya kitaaluma wakiwa Chuoni ili kupata sifa ya kuendelea na Stashahada au Shahada mara baada ya kupata Vyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Waziri wa Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, (Mb), akisaidiwa na Naibu wake Mheshimiwa Gaudensia M. Kabaka, (Mb), kwa ushirikiano na ufafanuzi waliotoa kujibu hoja mbalimbali za Wajumbe wakati Kamati ikijadili Azimio la Bunge Kuridhia Kubadilishwa Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji (*The Arusha Technical College).*

Aidha, nawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa michango na hoja zao katika kufikiria Azimio hilo na sasa kwa ajili ya rekodi naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Janet B. Kahama,

Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mheshimiwa Khadija S. Ngozi, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Mwanakhamisi K. Said, Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim, Mheshimiwa Omari S.Kwaangw'.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti na matakwa ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Sura ya 129, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii inakubali na kuunga mkono hoja ya Serikali na kuliomba Bunge likubali kuridhia Chuo cha Ufundi Arusha **'***Technical College Arusha'* kuwa Chuo cha kinachojitegemea kiutendaji na kwamba kiitwe Chuo cha Ufundi Arusha (*The Arusha Technical College)***.**

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante, sasa nitamwita msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu hoja hii.

**MHE. SUZAN LYIMO – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza naomba kutoa shukrani zangu kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bunge lako Tukufu kuridhia Azimio la kukifanya Chuo cha Ufundi Arusha kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji (*Arusha Technical College),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5) (c ), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kuleta Azimio la Kubadili Chuo Cha Ufundi Arusha kuwa chuo kinachojitegemea kiutendaji. Uamuzi huu unalengo la kukipa mamlaka ya kujiendesha chenyewe ili maslahi ya wafanyakazi yaboreke hii ikiwa ni pamoja na waendeshaji na Walimu, lakini zuri zaidi ni kwamba Chuo kitabuni miradi mbalimbali hivyo kukiingizia kipato zaidi

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya yatasaidia sana katika kujiimarisha kwa mfano, kitapata walimu wenye elimu katika ngazi ya Shahada za Uzamili (*Masters*) na Uzamivu *(Ph.D).* Lakini pia Chuo hiki kitaweza kuwa na programu mpya za mafunzo mbalimbali katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada. Pamoja na kupongeza hatua hii ya kubadilishwa kwa chuo hiki Kambi ya Upinzani haina pingamizi lolote ila inaiomba Serikali ihakikishe mabadiliko hayo pia yanaenda sambamba na ongezeko la fedha *(financial resources*) kwani uzoefu unaonyesha kwamba vyuo vikibadilishwa au vikapanuka basi bajeti inakuwa ile ile au nyongeza inakuwa ndogo sana hivyo kupoteza kabisa ile dhana nzima iliyokusudiwa. Mfano ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo pamoja na ongezeko kubwa la wanafunzi bado mabweni ni yale yale na bwalo la chakula ni lile lile, idadi ya vyoo ni ile ile na kadhalika. Kimsingi miundombinu imebakia kuwa ile ile hivyo kufanya watumiaji wake kupata matatizo makubwa ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba tayari wametenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya ukarabati, huu ni mwanzo mzuri na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wahadhiri na wale waendeshaji ni vyema pia mabadiliko haya yaende sambamba na kuajiri wahadhiri wenye shahada za uzamivu *(Ph.D.)* na zile za uzamili ili waendane na programu mpya. Litakuwa jambo la ajabu kwa wanafunzi kufundishwa na wenye shahada ya kwanza au ya pili tu, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Wizara itazingatia hili ili waweze kuwa na Wahadhiri ambao wana digirii mbalimbali ikiwa ni pamoja na za Uzamivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taaluma ya ufundi ni muhimu mno kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Nchi kama Kenya, Zimbabwe, Nigeria, Australia, Cuba na zile za Ulaya Magharibi, zimepata mafanikio makubwa kwa kuwa na vyuo vya ufundi. Umuhimu wa Chuo kama hiki ni kutoa nafasi kwa wanafunzi wengi na vinatoa uzoefu kazini, kitasaidia wafanyakazi wengi kupata nafasi ya kuendeleza taaluma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi katika vyuo vya ufundi wanajiunga wakiwa wamepata alama za daraja la kwanza na daraja la pili. Lakini wanashindwa kuendelea na elimu ya vyuo vikuu kulingana na utaratibu mbovu uliopo, masharti magumu, mfano ni lazima afaulu masomo yote tena kwa wastani wa alama ya B. Lakini kibaya zaidi mtihani hutungwa na Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)* na wote tunakumbuka matatizo yaliyojitokeza katika Chuo cha Ufundi cha Dar es Salaam miaka iliyopita. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Wizara italizingatia hili ili wanafunzi hao waweze kuendelea na ngazi nyingine ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utaratibu uliopo ubadilishwe na waweze kutahiniwa kulingana na mitaala ya taasisi husika la sivyo tutakuwa tunapoteza vijana wengi wenye uwezo kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Ni muhimu watakaotoka kwenye Cheti wapate Stashahada na baadaye Shahada na kadhalika, kuendana na uwezo wao kitaaluma.

Pamoja na juhudi za Serikali kuwa na mpango kamambe wa kuwa na vyuo vya ufundi *(VETA)* katika kila Wilaya, bado kama mfumo wa mitaala na mitihani utaendelea kama ulivyo, vijana wengi wa *VETA*, hata wenye uwezo mkubwa kitaaluma watashindwa kusogea hatua nyingine ya elimu hivyo kubakia na cheti tu. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ione ni jinsi gani Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia inavyoweza kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili waweze kurekebisha mitaala na mitihani. Yaani mitihani ya *VETA* ipelekee watahiniwa kuweza kuendelea na elimu ya juu na vilevile wale wanaotoka vyuo vya ufundi (*Technical Colleges)* waweze kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya ufundi vinalenga zaidi watu au wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne na sita ambao hawatakuwa na sifa za kuingia vyuo vikuu au kuendelea na masomo zaidi. Vyuo hivi uendeshaji wake hauna gharama kubwa sana hali itakayopelekea wanafunzi wengi zaidi kudahiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yetu ni kwamba, nchi yetu itaendelea sana endapo tutakazia sana wanafunzi wetu wapate hii elimu ya wastani yaani ya ufundi ambayo kwa muda mwingi mwanafunzi anakuwa anajifunza kwa vitendo zaidi kuliko katika Vyuo Vikuu ambavyo wanafunzi hufundishwa nadharia zaidi kuliko vitendo. Pia tujue kuwa nchi yetu haina viwanda au makampuni makubwa yaliyo na teknolojia ya hali ya juu sana kiasi kwamba mwanafunzi akiajiriwa pale anapata fursa ya kufanya utafiti wa kuboresha kiwanda au kampuni. Kinachofanyika ni kwamba mwanafunzi akiajiriwa anapewa majukumu yake kama ni ununuzi, operetta, usimamizi, na kadhalika wakati amefundishwa nadharia na namna mbalimbali za kukokotoa maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika leo hii Japani ina Vyuo Vikuu vingapi lakini ninachojua kilichoifanya Japani kuwa nchi iliyoendelea kiviwanda ni Vyuo vya ufundi/*colleges* kuwa vingi kiasi kwamba *technicians* ni wengi kuliko watafiti kutoka vyuo vikuu. Naomba tuelekeze macho yetu katika elimu hii ya kati ili tuweze kwenda na mazingira, uwezo wa nchi (Serikali) na uwezo wa wananchi mmoja mmoja hasa wale waishio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano, mwaka juzi wanafunzi walioingia chuo kikuu udhamini ulikuwa ni kwa wanafunzi waliokuwa na *division one* tu (wanaume) na *division two* (wanawake). Je, *division two*, *three* na *four* kwa wanaume na *three* na *four* kwa wanawake walikwenda wapi? Kama siyo vyuo vya ualimu kuna mtu anajua walipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mifano mingi ya wanafunzi waliokata tamaa baada ya kukosa udhamini wa Chuo Kikuu na wamebaki majumbani lakini tukiiwezesha hii elimu ya kati tutawezesha kundi kubwa la watu kuelimika tena kwa vitendo. Vyuo hivi (*FTC*) ni muhimu sana na hivyo ni matumaini yangu kubadilishwa kwa chuo hiki ni mwanzo tu wa kubadili na vyuo vingine vya aina hii ili viweze kujitegemea na kuchukua vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu vyuo hivi tuviingize katika mfumo mzima wa elimu na tutoe kipaumbele kwa kuviwezesha na hata tukiomba msaada basi tuelekeze zaidi katika eneo hili. Tulenge kutoa wahitimu ambao wakipata mitaji tu basi waweze kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kampuni ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru wewe mwenyewe Naibu Spika, kwa kunisikiliza na Waheshimiwa Wabunge wote. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ya Azimio la kubadilishwa kwa Chuo cha Ufundi Arusha (*The Arusha Technical College*) Asanteni sana.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana kwa maoni yenu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi ambayo kwa hakika nimekuwa nikifikiri ni lini

nitakuja kupata fursa ya kutoa mchango wangu katika eneo hili ambalo kwa kweli linanihusu sana na ningependa tu nitamke kwamba mimi ni *product* ya *Arusha Technical Collage,* nimesoma pale na kwamba nina maslahi makubwa sana na chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze tu kusema kwamba utashangaa leo hii ninasimama kama Mbunge wa Kibakwe nikiwa mwanasheria na sio fundi, hii inatokana na mazingira yaliyopo ya mfumo wa elimu ya ufundi katika nchi yetu. Leo kwa mafundi wenzangu niliosoma nao na ninashukuru hata hapa katika watumishi wa Bunge walioajiriwa juzi ni mafundi watupu na ninakiri mmeajiri mafundi wazuri kwa sababu ninawajua nimesoma nao. Kuna wahandisi wako hapa nimesoma nao kwa kweli tumeajiri mafundi wazuri sana na mambo mtaona yatakavyokuwa tofauti na siku za nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa elimu ya ufundi katika nchi yetu nataka niseme kwa kuletwa hii *Establishment Order* ambayo Waziri anaileta hapa ili kukifanya Chuo hiki kijitegemee. Lakini pia *content* iliyopo katika hii *Establishment Order* yenyewe kwa kweli ni nyota mpya ambayo mafundi wote katika nchi hii na hasa tuliosoma katika Chuo cha Arusha *Technical College,* Chuo cha Mbeya na Chuo cha Dar es salaam *Technical College*, inatuletea sura mpya na matumaini mapya na mimi napenda niwatie shime wenzangu kwamba bado hawajapotea, fursa imerudi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo uliokuwepo wa ku-*mis handle* mafundi umepoteza vipaji vingi sana na *resource* kubwa katika eneo hili, nataka nikuhakikishie kwamba hakuna mtu anayejua hesabu zaidi ya fundi, kwa sababu ufundi ni hesabu tupu. Mimi kwa mfano nimesoma Shule ya Sekondari ya Mazengo.

Shule hiyo ilikuwa ya ufundi, ukitoka pale unakwenda *Arusha Technical College* kama umefaulu daraja la kwanza au la pili, ukifika daraja la tatu wanakuangalia kama unafaa kwa ajili ya *PCM,* ukionekana unafaa unachaguliwa kwenda *form five*. Nataka nikuhakikishie kwamba wale waliokuwa wanakwenda *form five* baadaye wakamaliza *form six* kwa *PCM* ndiyo leo hii wahandisi na wale tuliokwenda *FTC* tukiwa ndiyo *pure* mafundi tuliosoma *bolt* na *nut* kwa miaka minne Sekondari leo tuko mitaani tunahangaika tukiwa tumekosa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wetu kwa kweli haukuwa sawasawa na ninakiri kwamba hata sasa jitihada kubwa zinatakiwa zifanyike ili kubaini kwamba kuna vipaji vingi. Wengi niliosoma nao wanajua sana hesabu, mimi nashangaa hapa wanasema hakuna Walimu wa hesabu! Hivi kuna Walimu wanaojua hesabu kuliko waliomaliza *FTC?* Hapa kuna *engineers* kama Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Engi. Lous Mhina, ni mainjinia kweli kweli kwa sababu wana-*trend* ya ufundi tangu wameanza *O-level Education* mpaka Digrii. Lakini uhandisi unatofautiana, mhandisi aliyemaliza *form six* akaenda kuchukua digrii ya uhandisi hawezi kulingana na Mhandisi aliyepitia mchepuo wa ufundi kutoka *O-Level* akaenda kuchukua Shahada ya ufundi. Ndiyo maana nasema hoja imeletwa katika kipindi muafaka na

nimpongeze sana Waziri ambaye naamini ataleta mabadiliko makubwa katika sayansi na teknolojia katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisoma hii *Establishment Order* yote lakini mawazo yangu naomba yawe ya jumla sana, hata kwa wenzetu Nchi Zilioendelea kisayansi na teknolojia, wanaanza na *Technical Institute,* halafu wanakuja *poly-technic*, halafu wanakuja *Technical Universities*, katika mtizamo huu sasa nadhani hapa Mheshimiwawaziri anachotaka kutuambia ni kwamba tunakuwa na mtizamo wa aina hiyo, tunam-*train* mtu ufundi kutoka shule ya msingi, sekondari, anakwenda anafanya Diploma, baadaye anakwenda kuchukua shahada anakuwa mhandisi *pure,* huyu ndiye anaweza kugundua mtambo. (*Makofi*)

Mimi kwa mfano ile *research* niliyoifanya nikiwa namaliza *FTC* Arusha *Technical College* nilitengeneza baiskeli ya mlemavu inayotumia nguvu ndogo sana. Ujuzi ule leo hii umepotea, leo hii mimi ni mwanasheria kwa sababu ya kuwa *frustrated* na *system*. Wako marafiki zangu ambao leo hii ni wahasibu wametoka kule wakaenda kufanya tena *IFM* baada ya kuona mfumo huu umetunyanyasa bure, masomo ni magumu. Mtu aliyemaliza *FTC* akienda Chuo Kikuu *Engineering* miaka miwili ya kwanza yuko likizo kwa sababu aliyoyasoma kule ndiyo anayoyasoma pale. Uwezo wangu wa mahesabu na mafundi wenzangu tuliosoma *FTC* ni mkubwa kuliko hata aliyemaliza *form six* hafikii, lakini tunaambiwa hakuna walimu wa hesabu. Walimu wapo lakini hatujui wako wapi kwa sababu siku zote tuna tabia sisi ya kutengeneza kitu halafu tunakiachia njiani hatujui kiko wapi. Sekondari zetu hapa zinakosa walimu wa hesabu. Mimi nina marafiki zangu wengi ni mafundi pale gerezani kwa sababu ya kuwa *frustrated* na mfumo wakitafutwa wale watafundisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo ambalo nataka kulisema hapa kuhusiana na hili ni kwamba kwa kweli mfumo huu ulirudi nyuma na ugeuke nyuma sasa na ningemwomba Waziri awatambue kwamba anao mafundi wengi ila wako tu mitaani *frustrated*, wana elimu ya kutosha. Wanajua mambo wanaweza wakagundua kwa sababu wanajua hesabu. Mimi tukileta hesabu moja tu ya *machine element* hapa na nimeisoma nikafundishwa na mwalimu mama Mafupa sijui kama yuko hai, ambaye shahada aliyokuwa nayo Tanzania walikuwa wawili au watatu tu wenye shahada ya *machine element* ambayo alikuwa anatufundisha sisi. Lakini leo ujuzi wangu na wenzangu umepotea, ule ujuzi ni wa kiugunduzi siyo ujuzi wa kuungaunga vitu, ni kugundua mashine lakini umepotea. Mimi nasema jambo hili limekuja katika wakati mzuri japo limechelewa, turudi tujue namna tunavyoweza kusaidia sayansi na teknolojia katika nchi yetu, siyo kwa nadharia bali kwa vitendo. (*Makofi*)

Nina marafiki zangu nimesoma nao, Mazuki amegundua *ignition timing* ya *engine* ameletwa Arusha kusoma pale kamaliza na ujuzi sijui aliishia wapi? Lakini ile *ignition timing* imepotea ambayo hata Wajapani wenyewe hawajaweza kugundua kitu cha namna hiyo. Lakini imepotea. Sasa mimi nasema tuendelee na hili lakini tukiwa na mtazamo kwamba tunakokwenda kwa kweli tunatakiwa twende katika mfumo kama kweli sisi tunataka kuleta mapinduzi ya sayansi na teknolojia ili tusogeleane na wenzetu walioko

katika dunia iliyoendelea. Mimi nadhani kuna haja ya kuunga mkono hoja na kwa kweli naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia nikiamini madhumuni yake ni haya ya kutupeleka huko kwenye *technical university* ya watu wagunduzi waliosoma mambo ya kifundi tangu wanazaliwa. Ufundi ni *talent* toka mtu anazaliwa ana *idea* ya ufundi. Ukimlea huyu mpaka akapata digrii lazima atagundua na ugunduzi ni *business*, sasa akishagundua ndiyo tunaweza kujivunia kwamba Tanzania tumetengeneza kitu cha namna hii. Lakini huku hatutafika tutabakia ku-*service* magari na kumwaga *oil* na kadhalika, ndiyo tutaishia hapo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme tu kwamba tatizo ni mfumo. Kinachopelekea mafundi wasithaminike mitaani au kwenye ajira, maana ukimchukua fundi mchundo, kwa mfano, mimi nimesikia wanasema mafundi sanifu lakini najua *FTC* ni fundi mchundo sasa Kiswahili chake sijui, kama ni sawa na fundi sanifu. Lakini sisi tunajua kwamba sisi ni mafundi mchundo, sasa sijui kama ni sawa na fundi sanifu kwa sababu wako wale wa *VETA* na wenyewe ni mafundi. Sasa mfumo wa Chuo hiki, tatizo langu linakuja kwamba nani achukuliwe kupelekwa kwenye chuo hiki. Yaani ni yupi anaye-*qualify* kupelekwa kwenye hiki chuo ambacho kinakuwa kinajitegemea na cha ufundi tupu.

Mimi nadhani kwenye hili sijaona lakini nadhani ningeshauri tu kwamba ni vizuri wakachukuliwa pamoja na wale waliotoka kwenye shule za ufundi ambazo sasa hatuna. Nafikiri zaidi ya *Moshi Technical* sijui kuna ipi maana yake Mazengo ndiyo hiyo kwa heri, Ifunda sijui bado inaendelea, ipo inaendelea basi wale ndiyo wapewe *priority* ya kupelekwa kwenye chuo hiki. Lakini pia hata wanaomaliza *VETA* wakafaulu vizuri, kuna mafundi wazuri sana wanafaa kabisa, wanaweza wakaingia pale na wakawa mafundi wazuri wakaja kuwa wahandisi baadaye. *VETA* siyo kitu cha kudharau ni watalaamu wakubwa sana. Wakubaliwe kusajiliwa na chuo hiki kama mafundi ambao wamepitia elimu ya sekondari na baadaye kwenda kwenye chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kitu ambacho nafikiri mafundi wenzangu wanaonisikiliza watakifurahia. Nini tatizo la mafundi? Tumekwishaanzisha hiki naamini kwamba kitafanikiwa na naamini kitaleta mafundi wazuri. Sasa tatizo ni mfumo au nchi au *system* inawapokeaje hawa wakishakuwa mafundi hapo ndipo tatizo linapokuja. Utamkuta fundi akiwa kwenye taasisi yoyote anaonekana *as if not a staff but a supporting staff* yaani awepo, asiwepo hakuna matatizo.

Siku hizi mtu yeyote anataka mtoto wake asomee uhasibu, kwa sababu kwenye fedha ndiyo wanaofanya *decision* huyu fundi anatengwa kabisa hashirikishwi kwenye maamuzi. Lakini pia mfumo wa Serikali yenyewe kwamba unaweza kukuta kwa mfano ukichukulia hapa *institution* yetu hii kubwa ya Bunge, *transport officer* ndiye anayekuwa *technical advisor*. Mme-*displace* fundi yule amesomea ku-*allocate* magari, *service time*, na kadhalika. Lakini kuna mtu anayetakiwa kuwa *technical advisor* wa magari ya Bunge, hapo tungetoa ajira kwa fundi magari na kazi yake ingekuwa kushauri kwamba gari hii inaweza ikatengenezeka au haiwezi ikatengenezeka na ipelekwe wapi.

Mimi nilitembea ile Barabara ya Pugu miaka mitatu sipati kazi, nikaamua kuwa mchuuzi kwa kuwa *frustrated* na mfumo na wenzangu hivyo hivyo. Kwa hiyo, nasema tumebana mno, Serikali ifungue watu ujuzi wao uwape ajira. Sasa tunawasomesha watu lakini kwenye ajira tunawaletea tunawa-*displace* ndiyo maana watu wanakuwa *frustrated*. Unakuta mahali kuna magari karibu 70 lakini unaambia gari hii inatengenezwa gereji fulani, anayesema ikatengenezwa kule nani si anatakiwa awe fundi? Sasa unamkuta *administrative officer* ndiye anayeamua hatima ya gari. *Administrative officer* anayesema mtambo huu umeharibika, nani kakuambia umeharibika? Serikali inapata hasara kubwa kwanza kwa kupewa ushauri ambao haufai, ushauri wa *dili*, ushauri wa kutengeneza maslahi yao pengine mngekuwa na fundi huyu angesaidia kusema hiki hapana. Mimi nadhani mafundi wanahitajika, ajira zifunguliwe na Serikali yenyewe ifungue ajira hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kama chuo hiki kinaanza kama *kuna Board of Engineers why not Board of Technicians?* Kama kuna *Board of Engineers* wanakaa na kulinda maslahi yao, wanakaa na kulinda *welfares* zao kwa nini kusiwe na *Board of Technicians*? Naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kuweka *Board* ya *technicians,* wako wengi, naamini hata sisi wengine tunaweza tukaacha uanasheria tukarudi kwenye u-*technician* kwa sababu ni kazi tunaipenda mradi tu kukiwa na chombo ambacho kinalinda na kuthamini mchango wetu katika taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nishauri tu kwamba hizi *technical colleges* basi ziwekwe angalau katika *zone*. Kwamba kwa mfano, Kanda ya Ziwa wanaweza wakawa na *technical college* moja, Kanda ya Kati moja, pengine Kusini, Kaskazini hivyo hivyo kuweko na *technical colleges*. Maana hivi vyuo sasa kama unakitoa hiki Chuo cha Arusha katika mtazamo wa sasa maana yake kinaendelea kwenda mbele. Sasa tujue huku nyuma tuna watengenezaji mafundi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri haya kwa leo yanatosha. Lakini kama Waziri atahitaji msaada wangu, mimi mwathirika mkubwa na nimeambiwa kuna bodi hapa akiniona nitamsaidia sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nadhani sisi tulianza kuona *sympathy* kwamba kuna watalaamu ambao wanakosa kazi kumbe wapi! Nadhani hiyo ndiyo *message* kubwa tuliyoipokea. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii nami kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Lakini baada ya hotuba nzuri sana ya Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Simbachawene, ambaye ni fundi ambaye kati ya safari amegeuka kuwa mwanasheria sasa nimebakia na machache kweli kweli ya kuongea kwa sababu mengi ameyagusia kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunaelewa kwamba maendeleo ya dunia ya leo na ya kesho yanategemea elimu, yanategemea Sayansi na Teknolojia na kwa kweli bila nyenzo hizo muhimu tutakiwa tu wasindizaji wa maendeleo ya wengine, ndiyo kwa kweli naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Msolla kwa kuja na Azimio hili mbele yetu. Ni Azimio la kutuongezea uwezo kama nchi kielimu, linatuongezea uwezo kama nchi kisayansi na kiteknolojia, hatuna budi kuliridhia kuliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya watalaamu katika nyanja za ufundi sanifu na katika technolojia na utafiti yanaongezeka kadri tunavyoendelea. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo kwa kweli litatufanya wengi tulishabikie na kuomba Wizara iendelee na jitihada zake. Nimeguswa kipekee na mchango wa Mheshimiwa Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kutamka kwamba nchi yetu inahitaji kwa kweli Chuo Kikuu sasa cha Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, na mimi nataka niiombe Wizara baada ya kukihangaikia Chuo cha Ufundi cha Arusha, sasa ielekeze nguvu zake kukipandisha hadhi Chuo cha Ufundi cha Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia kama tulivyokuwa tumekwishapanga siku zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kikishapanda hadhi yake Chuo Kikuu cha Sayansi Teknolojia cha Mbeya, kitaendelea kutoa cheti, kitaendelea kutoa Shahada, kitatoa stashahada. Sasa kitaanza kutoa Shahada na vilevile Shahada za Uzamili bila kuleta mabadiliko yoyote lakini kwa kweli itakuwa ni msaada mkubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache sana ningeomba tu niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie kidogo tu kuhusu hoja hii. Mimi nakubaliana na hoja hii lakini nilikuwa na wasiwasi katika sehemu mbili au tatu hivi ambazo naomba Mheshimiwa Waziri anitoe wasiwasi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza katika Azimio ambalo Mheshimiwa Waziri alisoma katika ukurasa wa pili, *paragraph* ya mwisho ilisema kwamba Chuo kimetangazwa katika Gazeti la Serikali, Tangazo la Serikali Namba 78 la tarehe 30 Machi, 2007.

Sasa kama Chuo kimetangazwa katika Gazeti la Serikali, tarehe hii na halafu leo Mheshimiwa Waziri analeta hoja ya kuridhia, nilikuwa najiuliza na naomba anifahamishe ni kitu gani ambacho kinakuja mwanzo, ni kutangazwa katika Gazeti la Serikali na baadaye turidhie au kwanza tunaridhia halafu baadaye kinatangazwa katika Gazeti la Serikali? Ikiwa hivyo ndiyo basi nahisi kuna matatizo hapa kidogo kwa sababu ikiwa Serikali ndiyo imetangaza halafu kuomba kibali cha Bunge nafikiria kama Serikali sasa inakwenda kinyume na ule utaratibu wa *concept* ya *Separation of Powers* kwamba ina-*dictate over the parliament* ili iweze kufanya shughuli zake. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nilikuwa natazama *functions* za *college* katika ukurasa wa 4 wa hii *Establishment Order*. Katika ukurasa wa 4 wa ibara ya 4(2) inasema: *functions of the college* itakuwa *to conduct examination and grant awards of the college as approved by the National Council for Tanzania education*. Sasa hii ukisoma na ibara ya 32 ya *Establishment Order* ambayo ibara ya 32(1) inasema: *the governing board may with the approval of the minister make regulations for the better carrying out of the purposes of this order and without prejudice to the generality of this paragraph may make regulations: (a) prescribing awards which may be conferred or granted by the college*. Sasa hii nahisi kama kwamba kuna mgongano mdogo kwa sababu huku ni kitu kingine ambacho kinaweza kika-*award* hizo shahada na huku ni kitu kingine kabisa. Sasa naomba ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu katika ukurasa wa 9 ibara ya 12 inasema: *the governing board may on such terms and conditions as may determine, approve the Vice Principal academic who shall* halafu kuna (a) na (b). Sasa (b) huyu anatakiwa a-*act* kama ni *Principal where the Principal is enable to perform his function by reasons of illness, infirmity or absence from the college.* Lakini ibara ya 14 vilevile inasema hivyo hivyo kwa *Vice Principal administration*, maana yake kuna *Vice Principals* wawili, mmoja ni *academic* na mmoja ni *administration*. Sasa na huyu *Vice Principal* wa *administration* ikiwa *Principal* hayupo vilevile ata-*act as the Principal where the Principal is unable to perform his functions*. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba *Vice Principals* hawa wawili ambao kwa wakati mmoja ikiwa *Principal* hayupo wata-*act* vipi kama ni *Principal* au hapatatokea ugomvi wowote hapa? Kwa hiyo, mimi nahisi kwamba *Establishment Order* hii ingeliweza kurekebishwa kidogo ili ijulikane ni *Vice Principal* gani ambaye ata-*take precedence over the other* ikiwa *Principal* hayupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwamba suala hili ni zuri na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, nafikiria kwamba kuna haja sasa katika nchi yetu angalau kuwe na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, wakati umefika wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Na mimi pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mufundi Kusini, ningependa kutoa pole kwa familia, ndugu na Waheshimiwa Wabunge wote wa Viti Maalumu kwa kifo cha Mheshimiwa Salome Mbatia.

Pia ningependa kutoa pole kwa ndugu yetu Mudhihir Mudhihir kwa kupata ajali ya gari na hatimaye kukatwa mkono. Pia nitoe pole kwa ndugu Prof. Juma Kapuya kwa kupata ajali ambayo ilisababisha vifo vya wanachama wenzetu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii, kwanza kabisa, ningependa nijirejeshe kidogo katika historia ya ufundi katika nchi yetu. Nadhani sote tunafahamu

kwamba wakoloni hawakupenda kabisa sisi watu weusi tupate ufundi. Waliingiza katika vichwa vyetu kwamba ufundi ni kazi ya watu wasio na akili nyingi, watu wanaofeli shule. Mimi nimepitia mkondo wa ufundi hapa nilipo ni Mhandisi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lakini nilipitia katika *technical schools* nikaenda kusoma Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, toka pale nikaenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ni kwa sababu nilipata madhara na matatizo ya kupitia njia hii, sikujielekeza sana. Kwa hiyo, ninao uzoefu wa kutosha kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tutapendekeza vijana hao wawe wanapata vyeti na diploma peke yake. Lakini baada ya hapo wanakwenda wapi au baada ya hapo tunakuwa tumewafungia ndani ya chupa hawawezi kutoka tena kuendelea na Elimu ya Juu? Maana yake Sheria tunayoipitisha hapa haielezi kinagaubaga kwamba hao vijana wakishapata Stashahada wanaendelea vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua hao vijana ni watoto wetu na kwa sababu hili ni Bunge ndilo linalotunga Sheria ni vizuri tunavyotunga Sheria, tutunge Sheria ambayo inaeleweka, Sheria ambayo itawapa vijana hao imani kwamba baada ya kupata Stashahada wanaendelea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe amesema kitu kizuri kwamba sasa kile Chuo cha Ufundi Mbeya, kiwe Chuo Kikuu, na mimi ninaunga mkono kabisa Mbeya kiwe Chuo Kikuu. Lakini Chuo hiki tunachokitungia Sheria napendekeza kiwe Chuo Kikuu Kishiriki. Kwa sababu angalau hao vijana wanaosoma baada ya kupata diploma Arusha watakuwa na uhakika kwamba baada ya kupata diploma mhitimu anaweza kuchukua *Masters* sehemu yoyote duniani. Lakini Sheria hii imekaa kimya kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipindi nilikuwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Usajili ya Wahandisi Tanzania. Vijana wanaohitimu katika hivi Vyuo vya Ufundi huwa wanaitwa *Technician Engineer*, sasa huyo *Technician Engineer* duniani anajulikana wapi? Duniani anayejulikana ni *Engineer* hakuna *Technician Engineer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Sheria hii naamini kabisa inawaingiza vijana hawa ndani ya chupa na itakuwa ni vigumu sana kutoka kwa Sheria ambayo tunawatungia sasa hivi, tunawaingiza katika mpenyo ambao kutoka kwake itakuwa ni vigumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo nitamwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake atoe ufafanuzi wa kutosha kabisa ndani ya Bunge hili ili kila mmoja ajiridhishe kwamba kwa kweli Sheria hii tunayoitunga itawapa mwanya vijana wetu waendelee na masomo kwa kadri ya uwezo wa akili zao. Yaani wasome mpaka mwisho wa uwezo wao ikiwezekana wapitie njia hii mpaka wapate *PhD* kwa sababu Elimu ndani ya nchi yetu ni haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu mimi ndiye msemaji wa mwisho napenda kuunga mkono hoja hii. Lakini nitaiunga mkono hoja hii mno iwapo Mheshimiwa Waziri atanieleza namna vijana hao baada ya kupata Shahada wataendelea wapi na elimu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo mafupi, napenda kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema huyo ndiye alikuwa msemaji wetu wa mwisho. Bahati nzuri wasemaji wote walikuwa ni mafundi, mainjinia wa ufundi. Kwa hiyo, tumepata faida kubwa sana ya ufundi wao na *experience* yao mbaya mpaka wakaona waje wagombee Ubunge tu na pengine wapate nafuu. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja!

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa wote waliochangia kwa kuzungumza na vilevile kwa maandishi. Hoja zilizotolewa ni nzuri sana na zimezidi kuboresha yale ambayo nilikuwa nimeyawasilisha.

Ningependa kuwatambua wale ambao wamechangia kwa kuzungumza hapa ndani nao ni sita. Ninapenda kumtambua Mheshimiwa Omar Kwaangw’, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na Mheshimiwa Benito Malangalila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao wamechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Napenda kuwashukuru sana kwa michango ambayo wameitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumza kwa ujumla tu, kwamba historia ya Elimu ya Ufundi hapa nchini si ngeni hata kama mfumo ulikuwepo haukuridhisha. Wote mnakumbuka na kama wengine walivyoeleza hapa kwamba tulikuwa na Vyuo vya Ufundi vilivyojulikana sana na si ajabu ile *generation* ya wale wataalamu hatunayo tena, kama wamebaki basi ni wachache sana. Tulikuwa na Chuo cha Ufundi Ifunda ambacho sasa katika mabadiliko imekuwa *Secondary School* ya kawaida, tulikuwa na Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, Dar es Salaam *Technical College* na chenyewe kimezidi kupanda hadhi na kuwa Dar es *Salaam Institute of Technology* na ambacho kwa wale ambao wamekuwa wakijiuliza sasa hivi kwamba wahitimu wale wa stashahada wamekuwa wakienda wapi? Nitatoa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Moshi *Technical College* leo haipo. Lakini vilevile Tanga kulikuwa na *Technical College*. Kwa hiyo, masomo ya Ufundi na hasa hao wa kati yalikuwepo toka awali, lakini katika mabadiliko ya mfumo wa

Elimu hapa katikati ikaonekana kwamba hili hatukulitilia maanani na mimi ninashukuru kwamba sasa hili linarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kubwa sana kati ya Vyuo vya Ufundi na Vyuo Vikuu. Hata kama vyote viwili vinatoa Shahada, *Masters*, na Uzamivu, Vyuo Vikuu zaidi vipo kwenye nadharia, vitafundisha, vitafanya utafiti, na vilevile vitatoa huduma kwa wananchi. Utafiti ndiyo kitu ambacho kidogo ni tofauti na Vyuo Vikuu vya Ufundi. Kumbe kwenye Vyuo Vikuu vya Ufundi msisitizo ni ile *skills development, hands on training.* Lakini na zaidi ya hapo kunakuweko na ubunifu.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Simbachawene hicho ndicho kitu ambacho kina tofauti kubwa sana. Hawa wanaotoka kwenye Vyuo vya Ufundi ni watu ambao wakitoka kwa kweli wamekamilika, wanaweza kujiajiri na kuajiri watu wengine. Kwa sababu *they have the necessary skills,* kinyume na Vyuo Vikuu ambako wao wanakuwa kama *think tanks* na siyo wabunifu na wenye uwezo wa kufanya kazi ya vitendo kama hawa wanaotoka katika hizi Taasisi za Ufundi.

Baada ya kueleza haya ya jumla naomba nitoe maelezo kwa kifupi katika maeneo yaliyotajwa kwa ujumla. Kwanza Mheshimiwa Omar Kwaangw, na Mheshimiwa Susan Lyimo, wote wamesisitiza sana umuhimu wa kutokubali tu Chuo kinachojitegemea lakini vilevile iende na bajeti. Nafurahi mmetambua kwamba tayari hili tumekwishaliweka na imeanza na kadri ya uwezo wa Serikali hili litaweza kuboreshwa mwaka hadi mwaka. Vilevile kumetolewa ushauri kuweko na ubunifu wa *programmes* zinazokwenda na wakati. Ni kweli na katika maelezo yangu ya msingi nimesema baada ya kukifanya kuwa Chuo cha Ufundi kinachojitegemea, moja ya matokeo yake ni kwamba wanaweza kubuni mitaala ambayo itakwenda na wakati.

Kuna maeneo mengi sana tumesikia, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Omar Kwaangw, alivyoeleza upungufu mkubwa, uwiano kati ya Mhandisi kuja kwa Fundi Sanifu na kuja kwa Mafundi Stadi. Kwa hiyo, mahitaji hayo ni makubwa sana na kuna upungufu mkubwa. Moja ambalo limeleta upungufu mkubwa ni kwamba vile vyuo vilivyokuwepo havipo tena na ndiyo maana kumetokea hii *gap* kubwa ambayo ipo. Amezungumzia pia juu ya umuhimu kuwa waendelezwe, walimu waendelezwe wafikie *Masters* na *PhDs,* tayari katika taarifa yangu niliyokuwa naitoa nimeeleza kwamba hili tayari linafanyika na siyo hapo tu, hata *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* wako ambao wanasomea *Masters* na *Ph.D*. Ukienda *Mbeya Institute of Science and Technology* ni sawa hivyo hivyo.

Imezungumzwa sana juu ya umuhimu wa ujenzi wa Taasisi za ufundi hadi Wilayani, hili litategemeana na uwezo wa Serikali. Lakini linalowezekana sasa ni zile Kanda kama alivyoshauri Mheshimiwa George Simbachawene, lakini kwenda mpaka Wilaya itachukua muda, maana yake tungesema pengine tuanze kila Mkoa nayo hiyo ni ngumu, hata hivyo tutakwenda kadri ya uwezo wa bajeti ya Serikali unavyojitokeza na vilevile suala la kusema hawa waliomaliza wakimaliza Stashahada wanakwenda wapi? Hawa waliomaliza Stashahada wanakwenda kufanya kazi, hiyo ni njia mojawapo lakini

kuna wengi ambao wanapata nafasi ya kujiunga na elimu za juu hawapiti huo mkondo moja kwa moja.

Pale nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa *Advance Diploma*, kwamba akitoka kwenye *Diploma* kama amefaulu vizuri anakwenda *Advanced Diploma* lakini neno hili *Advanced Diploma* limeonekana kwamba lilikuwa ni la kwetu tu Watanzania haliko mahali pengine. Katika kuweka hizi sifa sawa sawa imeonekana kwamba lazima tuje kwenye kitu kinachoitwa *Higher Diploma,* kwa hiyo, akienda nako aka-*perform* inaonekana kama njia ndefu hatimaye atajiunga na elimu ya chuo kikuu. Nafikiri kwa kuelieza hili nimeshamjibu Mheshimiwa Malangalila aliyekuwa anasema hawa watu wanakwenda wapi.

Lakini halikuishia hapo juu, ni kwamba kuna hili swali la kwamba Chuo, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya iwe Chuo Kikuu. Mimi sidhani kama kuna ugomvi mkubwa, kila kitu kinakwenda na wakati wake na inapofika ngazi husika kunafanywa tathmini, hata ripoti iliyokuwepo ilikuwa inatamka juu ya tathmini kwa wakati unaofaa bila ya kuathiri zile kozi zilizokuwepo kwa sababu bado kuna wahitimu. Kwa hiyo, wakati ni muhimu sana. Nafikiri tarehe 20 Julai, 2007 nilipokuwa natoa maelezo hapa nilisema kwamba inaelekea tunagombania jina. Kwa sababu hata katika kauli yangu nilisema tutakwenda mpaka shahada ya kwanza, shahada ya pili, mpaka ya Uzamivu. Lakini neno lililokuwa linagomba ni hilo neno la *Institute vis-a-vis University* na nikatoa mfano wa *Institutes* nyingi duniani ambazo zinatoa shahada mzuri sana kuliko hata vyuo vingine.

Kwa hiyo, nafikiri hili jambo la kupanda kuwa Chuo Kikuu ni jambo linalozungumzika ilimradi tathmini katika wakati unaofaa iweze kufanywa. Lakini watu hawa watakuwa ni zaidi katika mafunzo ya vitendo, wawe na *necessary skills*, asiwe injinia anayetoka *Mbeya Institute of Technology* ambayo *Mbeya University Science and Technology*, yeye afanane na yule anayetoka pengine Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambako kuna nadharia zaidi kuliko mafunzo ya vitendo. Kuna pendekezo ambalo limetolewa kwamba kuweko na ushirikiano zaidi kati ya Wizara mbili ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Elimu ya Juu. Hili ni jambo jema, tayari kuna ushirikiano lakini pengine tulipe umuhimu zaidi katika maeneo ambayo yanahusika.

Mheshimiwa George Simbachawene amezungumza mengi sana na kwa uchungu kwamba ilibidi kuacha taaluma yake akaenda kwenye Sheria. Bado kuna nafasi ya kurudi katika hili tena baada ya mfumo huu mpya na kwamba siku hizi hata mtu anayechukua *Medicine* anaweza kuchukua *Law as a sideline* na ni jambo la kawaida tu sehemu zingine. Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa George Simbachawene asipoteze kabisa taaluma hii ambayo alikuwa nayo, bado kuna nafasi ya kuweza kuendelea nayo. Vilevile alizungumzia kwa makini sana kuhusu umuhimu wa kuendelea mpaka kwenye shahada, hili nafikiri nimekwishalieza.

Lakini ningependa kuchukua nafasi hii kuwaeleza tu kwamba Wizara hii imekuwa ikishughulikia Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, hata hivyo, kwa muda mrefu Sayansi na Teknolojia imekuwa haionekani, *it is not vissible.* Kwa sababu

imegubikwa na Elimu ya Juu ambayo imekuwa na matatizo mengi sana na hususan baada ya kuanzisha mikopo. Lakini nashukuru kwamba hili jambo la mikopo linazidi kueleweka miongoni mwa jamii na sasa hivi tunashughulikia kwa nguvu sana juu ya *Science, Technology and University*. *(Makofi)*

Nashukuru kusema kwamba nafurahi kuwaeleza kwamba Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amemwandikia Mkurugenzi wa *UNESCO* kumwomba atume wataalamu watusaidie kwa njia yoyote ile ili tuweze ku-*review science, technology and University system* na hiyo kazi imekwishaanza na nafikiri a tutakuwa mahali pazuri zaidi.

Vilevile Mheshimiwa Simbachawene alisema akumbukwe katika Bodi ya kule *Arusha Technical College* ili akatoe mchango mkubwa. Akisoma ile *Establishment Order* itamwelekeza mahali ambapo anaweza kuingilia.

Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, yeye hakutaka kuzungumza mambo mengi kwa sababu hata Julai alilwishalizungumza hilo. Amelirudia na nafikiri nimetoa jibu. Kuhusu wasiwasi wa Mheshimiwa Abubakar Khamis, kwa bahati mbaya, wakati ule sikuwa na *Establishement Order* naona sasa ndiyo umeniletea. Lakini hata bila kuangalia hii, pengine ni namna ilivyoandikwa tu. Kwenye Vyuo Vikuu hata kwenye hizi *Technical Colleges* ama *Institutes* kunakuwa na *Principal* anasaidiwa na *Vice Principals* wawili, mmoja anakuwa wa *Academic*, mwingine wa *Finance and Administration.* Pale ambapo anakuwa *Principal* hayupo kwa namna moja au nyingine anayekaimu ni *Vice Principal Academic.* Lakini pale ambapo hata huyu *Vice Principal Academic* anakuwa hayupo, basi *Vice Principal Finance and Administration* ndiye anayekaimu. Inawezekana huku kumewekwa kwa makosa kidogo, sijaichambua hata kuiangalia vizuri mahali ambapo ulikuwa unafanya *reference.* Lakini tunalishughulikia hili.

Vilevile ulizungumzia majukumu ya Bodi, nafikiri ulisemea *Section 32*, ipo ukurasa wa 13, inasema: *The governing Board may, with approval of the Minister make Regulations for better carrying out of the purposes of this Order and without Prejudice to the generality of this paragraph may make Regulations.* Sasa hii ulikuwa umefanya *comparison* na nyingine, siikumbuki vizuri, lakini kwa ajili ya kuokoa muda mimi ningeshauri baada ya kikao hiki pengine tukae, tueleweshane ili kusudi mambo yaweze kueleweka vizuri zaidi. *(Makofi)*

La mwisho ambalo alisema Mheshimiwa Malangalila, na ningependa nilijibu kwa uhakika zaidi, kwamba *Arusha Technical College* iwe Chuo Kikuu kishiriki. Nafikiri wakati ukifika hilo litafikiriwa kwa sababu watu hawakai pamoja, wanazidi kubadilika kutokana na mazingira na *challenges* nyingine.

Kuhusu vijana wanaopata stashahada wanakwenda wapi nafikiri nimekwishalijibu. Lakini kulikuweko na ushauri mzuri kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala. Anasema Chuo hiki kama cha Arusha kisichukue wahitimu wa Kidato cha Nne na cha Sita tu lakini vilevile kichukue wahitimu waliotoka Vyuo Vikuu ili

wapate *hands* na *experience.* Ushauri huo ni mzuri, tayari katika nchi zingine hili linatokea.

Canada kuna kitu kinaitwa *Canada Community Colleges.* Watu wanaotoka Vyuo Vikuu vya kawaida wamechukua *Engineering* ama masomo mengine, hurudi kule wakatumia muda wao pengine wa mwaka mmoja ili waweze kupata *hands on experience*. Lakini maeneo mengine kama nilivyopata ushauri ambayo tayari yapo yametoka kwa Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi kwamba hawa watu lazima tu-*diversify* maeneo ambayo watachukua mafunzo. Kwa mfano, leo hii katika uchimbaji wa madini hapa nchini hakuna hata chuo kinacho-*train.* Wako vijana Dodoma *Mining School*, hawa kwa kweli ni wale *artisans.* Wako chini kabisa, lakini hasa *mining engineers*, na mambo ya *exploration* hakuna!

Imebidi kuleta watu kutoka Nigeria, hawa wenzetu wanaokuja kuwekeza, wamechukua watu kutoka *South Africa*, wametoka Australia. Vyuo hivi tulivyonavyo ndiyo vinatakiwa vifanye kazi hiyo. Chuo Kikuu cha Dodoma kitaanza na *College of Earth Sciencies* ambayo baadhi ya mafunzo yatakuwa katika maeneo haya. Lakini Chuo cha Mbeya vilevile kuna *potential* kubwa ya kuingia katika maeneo haya. Leo hii naona tunazidi kuimarisha hata *flight* yetu ya ndege, hakuna hata chuo kimoja kinacho-*train* hata *engineers* wa ndege wala *pilots* hapa nchini. Kwa hiyo, kuna maeneo mengi ambayo *they are technically based* ambayo kwa kweli hatuna uwezo na tunalazimika kuwapeleka hawa watu kusoma katika vyuo vingine nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nafikiri nimejaribu kugusa maeneo yote yaliyoulizwa na wasemaji na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Chuo cha Ufundi Arusha Kuwa Chuo kinachojitegemea kiutendaji liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Kwa hiyo, Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Ufundi Arusha kuwa ChuoKinachojitegemea Kiutendaji limepita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zetu za leo naona zimeishia hapa. Kesho bila shaka tutaingia suala la kupitia Kanuni zetu za Bunge. Ni vizuri mkawepo na Miswada mingine tutakayopitia pale.

Lakini ninalo tangazo moja, leo hii mwenzetu Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, amefiwa na mtoto wake hapa Dodoma. Kwa hiyo, shughuli zote sasa ziko anakoishi *Area D.* Kwa hiyo, watakaopata nafasi wanaweza kupita kule kwenda kumfariji. Maelezo ya ziada tutaweza kupewa kesho. Kwa hiyo, tunasikitika kwa haya yote yaliyotokea.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.17 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 15 Novemba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*